ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nane – Tarehe 31 Januari, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe leo tumejaaliwa kupata wageni katika Baraza letu tukufu, wageni hao ni kundi la kwanza ni baadhi ya Wabunge wa Bunge la Vijana la Zanzibar, miongoni mwao ni vijana wetu 60 walioshiriki katika Bunge la Vijana Zanzibar mwisho wa mwezi uliopita. Jumla yao waliokuja hapa ni 25 ambao wanaongozwa na makatibu Ndugu Amina Feisal na Ndugu Masoud Salum. Ningeomba Wabunge wa Vijana msimame, msalimiane na Waheshimiwa Wawakilishi wenu. (*Makofi)*

Kundi la pili ni Mabingwa wa Kombe la CCM Wilaya ya Mjini 2014. Hii ni timu ya *soccer* ya Jimbo la Kikwajuni inaitwa Kikwajuni Team, wamechukua ubingwa huu baada ya kuifunga Jang'ombe 2 kwa 1 hapo juzi, jumla yao ni 26, msafara unaongozwa na Mwenyekiti wa Timu Ndugu Hija Mchao. Katibu wa Timu ni Ibrahim Haji, wakifuatana na kocha wao Bwana Omar Iddi Masoud. (*Makofi)*

Waheshimiwa wageni hawa ni wageni wa Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa. Sasa mabingwa wetu nawaomba msimame ili msalimiane na Waheshimiwa Wawakilishi wenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny: Mhe. Miundombinu na Mawasiliano): Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na naomba kuweka hati mezani juu ya Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi inayohusiana na shughuli za Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu. Kwa heshima naomba kuwasilisha.

Mhe. Marina Joel Thomas (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha hati mezani ya Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

TAARIFA ZA SERIKALI

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya mwaka 2012/2913

(*Majadiliano yanaendelea)*

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii na kabla ya kueleza yale ambayo nataka kueleza, naomba niipongeze Timu ya Vijana ya CCM iliyoshinda mashindano ya mpira wa miguu. Lakini zaidi nimpongeze Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni kwa juhudi kubwa alizozifanya kuilea timu hii mpaka ikaishinda Timu Kabambe sana ya Jimbo la Jang'ombe. Naomba niwapongeze sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujaalia kukutana tena katika kikao hichi tukiwa wazima wa afya, pia nchi yetu ikiendelea kuwa na amani, utulivu na mshikamano. Aidha, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi kwa mara nyengine tena kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu na kuwasilisha utekelezaji wa maagizo mbali mbali yaliyotolewa na Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu nitoe shukurani za kipekee kwa Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Mlinde Mabrouk Juma na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa msaada, maelekezo na mashirikiano makubwa wanayoendelea kuipa wizara yangu. Ushauri, mawazo na maelekezo yao tumekuwa tukiyapokea, tunayathamini, tunayafanyia kazi na yanatusaidia katika kutekeleza vyema majukumu ya wizara yetu.

Napenda kuwahakikishia kwamba daima ushauri, mawazo na maelekezo yao tutayapokea na kuyafanyia kazi katika kutekeleza mipango, mikakati na sera za serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kuweza kuchangia hotuba na hoja zetu ambazo

huwa tunaziwasilisha hapa Barazani na kutoa miongozo yao iliyo sahihi. Aidha, michango na ushauri iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu imekuwa chachu kwa wizara yangu katika kutekeleza mipango ya serikali kwa wakati na kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, pia nachukua fursa hii adhimu kukupongeza Spika, Naibu Spika, wewe Mwenyekiti na Mwenyekiti mwenzako, Katibu wa Baraza, Maofisa na wafanyakazi wote wa Baraza kwa kuliendesha Baraza hili kwa hekima na busara kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Utekelezaji wa Maagizo 28 yaliyotolewa na Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari katika taasisi zifuatazo. Taasisi zenyewe ni:-

1. Shirika la Utangazaji
2. Shirika la Magazeti ya Serikali
3. Kamisheni ya Utalii
4. Chuo cha Maendeleo ya Utalii
5. Shirika la Utalii
6. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale na
7. Baraza la Taifa la Michezo.

Mhe. Mwenyekti, agizo la kwanza serikali iweke vigezo madhubuti vya sifa za kujiunga na Chuo cha Maendele ya Utalii ili kiweze kutoa wahitimu bora watakaomudu ushindani wa soko la ajira na kukijengea sifa chuo hicho.

Utekelezaji. Agizo limetekelezwa, katika usajili uliofanyika mwaka huu wa masomo 2013/14, Chuo kimetekeleza agizo hilo. Wanafunzi wameingizwa kwa sifa zifuatazo:-

i) Mafunzo ya msingi awe na Cheti cha *Form IV* angalau divisheni 4 chenye pasi katika masomo ya Historia, Jiografia, Hesabu, Kiingereza na Kiswahili au awe amepata cheti cha msingi cha *NTA 4* cha fani anayoomba.

ii) Mafunzo ya utembezaji wageni awe na cheti cha *Form IV* angalau divisheni ya nne chenye pasi katika masomo ya Historia, Kiingereza, Jiografia na Kiswahili.

iii) Mafunzo ya Diploma awe na Cheti cha *Form VI* chenye angalau pasi 2 za masomo ya Sayansi ya Jamii hususan Jiografia, Historian a lugha ya Kiswahili na Kiingereza na pasi ya somo la Hesabu.

Agizo jengine, ili kukifanya chuo chetu kiende sambamba na ulimwengu wa leo, Kamati inashauri serikali kukipatia fedha za kushiriki mikutano ya kanda na ile ya kimataifa kwa nia ya kujifunza na kupata uzoefu.

Utekelezaji wake ni kwamba, uongozi wa chuo umepanga kwenye bajeti yake ya makusanyo 2013/14, fedha za kufanya ziara angalau moja nje ya nchi na moja ndani ya nchi kwa lengo la kupata maarifa. Pia, hivi karibuni mnamo mwezi wa Mei na Juni, 2013 chuo kiliomba fedha katika Mradi wa Elimu Mbadala unaofadhiliwa na Mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika na viongozi wawili wa Chuo na walimu wanne walifanya ziara kwenye Chuo cha Utalii cha Kenya kilioko Nairobi na Vyuo vya Utalii nchini Mauritius.

Agizo jengine ni tatizo la mmong'onyoko wa ufukwe kwenye eneo la chuo linahitaji juhudi, nguvu na maarifa ya pamoja kwa taasisi zote zinazohusika, kwani imebaini kuwa nguvu za chuo pekee hazitoshi kupambana na janga hilo. Hivyo, kamati inatoa wito kwa serikali kuingilia kati suala hili kwani linahatarisha mustakamali wa Chuo.

Utekelezaji. Hatua zimechukuliwa kwa kuwaandikia barua Mkurugenzi wa Idara ya Mazingira ya kumuomba aitishe kikao cha pamoja na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Mkurugenzi Mazingira na Uongozi wa Chuo kujadili suala hili kwa sababu suala hili haliwezi kutatuliwa na Uongozi wa Chuo peke yake, ni suala linalohitaji utaalamu wa kisayansi zaidi. Aidha, katika sherehe za uzinduzi wa jengo la ghorofa moja, changamoto hii iliwasilishwa kwa mgeni rasmi Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais ambaye alisema ataitisha mazungumzo baina ya Ofisi yake, Wizara ya Habari na Chuo kujadili suala hilo.

Agizo la nne mauzo ya vyakula vinavyowekwa oda katika Chuo cha Maendeleo ya Utalii, ni chanzo kimoja wapo cha mapato ya Chuo, Kamati inapendekeza kufanyika kwa *package* nzuri ya kitaalamu ili kupata soko zaidi na kukuza pato la Chuo.

Utekelezaji. Chuo kinazingatia agizo hilo na kujaribu kubuni mikakati ya kuongeza mapato zaidi kama vile mpango wa kuutumia mkahawa kibiashara, uwekaji na uuzaji wa mikate maalum katika jamii ni miongoni mwa mikakati hiyo.

Agizo jengine, Chuo kupatiwa gari ili kiweze kuendesha shughuli zake vizuri na pia kukijengea hadhi Chuo hicho muhimu kwani hadi kamati ilipotembelea mwezi Mach, 2013 Chuo hicho kina gari moja tu.

Utekelezaji. Chuo kimeongeza gari nyengine aina ya *"TOYOTA HILUX, Pick Up double cabin"* kutokana na makusanyo yake. Aidha, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo imeomba Wizara ya Fedha mabasi mawili yaliyokuwa ya Shirika la Utalii kupeleka Chuo cha Maendeleo ya Utalii kwa lengo la kutumika kwa shughuli za Chuo.

Agizo jengine Kamati inaitaka wizara kulivalia njuga suala la msigo mkubwa wa madeni unalolielemea Shirika la Utangazaji, kwani dhahiri kuwa maendeleo ya shirika hili ambalo ndio kwanza limo katika hatua za awali hayatopatikana bila ya kuchukuliwa hatua za dharura za kuyalipia madeni hayo.

Utekelezaji. Ni kweli Shirika la Utangazaji la *ZBC* ambalo limeanzishwa kwa mujibu wa sheria iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi hivi karibuni lina mzigo mkubwa wa madeni hasa la umeme. Shirika la Umeme na Uongozi wa Shirika la *ZBC* tayari limekaa pamoja kujadili deni hilo kubwa na kubuni mbinu na mikakati ya kulipa deni hilo la Shilingi 489 milioni.

Agizo jengine, ipo haja kwa serikali yetu kuwa na mpango wa muda mrefu hususan katika Sekta ya Elimu, kwani Kamati imebaini kuwa kwa hivi sasa Zanzibar hatuna mtaalamu mzalendo mwenye sifa ya kuwa mshauri wa mambo ya dijitali.

Utekelezaji. Pamoja na Kamati kubaini kuwa hakuna mtaalamu mzalendo mwenye sifa ya kuwa mshauri wa mambo ya dijitali. Shirika la Utangazaji linajaribu kujenga uwezo wa wataalamu wa masuala ya dijitali kwa kutoa mafunzo na utaalamu mbali mbali kupitia vyombo kadhaa vya habari vya ndani na nje ya nchi kwa njia ya semina, makongamano na warsha za ndani na nje ya nchi ambazo kwa kiasi kikubwa watumishi hawa wameweza kujiamini katika kutekeleza wajibu wao.

Agizo jengine, wizara iandae utaratibu utakaowezesha wafanyakazai husuan kwa Shirika la Utangazaji *ZBC* kupima afya zao ili kubaini athari za kiafya zinazoweza kuwakumba kutokana na matumizi ya vifaa vyao vya kazi ikiwemo mitambo na mashine mbali mbali.

Utekelezaji. Shirika la Utangazaji limepanga kuanzisha utaratibu wa kuwapatia huduma ya kuwapima wafanyakazi wa taasisi hii, kutokana na hofu ya kuathirika na mionzi ya mashine mbali mbali. Aidha, hadi hivi sasa shirika halijapata ushahidi wa kidaktari unaoonesha kwamba kuna mtumishi aliyeathirika kutokana na matumizi ya mashine mbali mbali.

Agizo jengine, serikali iandae mpango maalum wa kutafuta fedha za kutosha kwa ajili ya uimarishaji wa Mradi wa Dijitali kutokana na umuhimu mkubwa wa mradi huo kwa serikali na wananchi wote kwa ujumla.

Utekelezaji. Serikali tayari imewekeza fedha nyingi katika mradi mkubwa wa kuweka miundombinu na vifaa vipya vya kisasa katika studio za *ZBC* Unguja na Pemba, ili kuwafanya wananchi wa Zanzibar kupata habari za matukio kwa hakika. Jumla ya dola milioni moja naomba pafanyiwe usahihi hapo, zimewekezwa na vifaa hivi vimenunuliwa kutoka Kampuni ya *On Air System Limited* na vinaendelea kuwekwa katika *studio* za *ZBC.*

Mhe. Mwenyekiti: Samahani Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe naomba utulivu minong'ono imezidi. Naomba tumsikilize Mhe. Wazir, akitoa taarifa yake.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, agizo la 10, wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Zanzibar iandae utaratibu utakaowezesha upatikanaji wa uhakika wa huduma ya umeme katika Shirika la Utangazaji Zanzibar.

Utekelezaji. Hatua zimechukuliwa na baada ya kukamilika kwa awamu ya pili ya mradi wa uwekaji umeme kutoka Dar-es-Salaam huduma za umeme hivi sasa ni za kuridhisha sana.

Agizo jengine, Kamati inapendekeza kuwepo kwa sera ya uhariri pamoja na mfumo wa upangaji wa utoaji wa habari kwa maendeleo ya *ZBC*.

Utekelezaji. Shirika la Utangazaji *ZBC* tayari limefanikiwa kuanzisha sera ya uhariri yenye kufuata maadili, utaalamu na yenye kukuza mvuto kwa wasikilizaji na watazamaji wa *ZBC*. Aidha, mfumo wa upangaji wa utoaji wa habari unakwenda vizuri kwa kuzingatia miiko na maadili na kutekeleza sera ya serikali, kutangaza maendeleo endelevu yanayohusu wananchi.

Agizo jengine, Kamati inashauri mara tu baada ya Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa Shirika la Utangazaji utakapotiwa saini na Mhe. Rais na kuwa sheria, Shirika la Utangazaji lifanyiwe uhakiki na kuwa na mabadiliko ya kiutendaji ambao utaliwezesha kupanga hatua za kimaendeleo na kumudu ushindani wa vyombo vyengine vya habari vya ndani na nje ya nchi.

Utekelezaji. Baada ya kuanzishwa Shirika la Utangazaji Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein, hivi karibuni amemteuwa Naibu Mkurugenzi Mkuu ikiwa ni pamoja na mikakati ya kuleta mabadiliko ya kiutendaji na kuimarisha uajibikaji. Aidha,

upatikanaji wa vifaa vya kisasa vilivyoanza kuwasili hivi karibuni ni moja ya mkakati wa kukabiliana na ushindani wa vyombo vyengine vya habari vya ndani na nje ya nchi.

Agizo jengine ili kukidhi ipasavyo azma ya kuanzisha Shirika la Utangazaji la Zanzibar, ni muhimu kwa serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuliimarisha na kuliendesha kwa ufanisi zaidi shirika hilo.

Utekelezaji. Jitihada za kulipatia shirika fedha zinaendelea ikiwa ni pamoja na kutoa matangazo ambayo yatalipiwa kwa ajili ya kuliongezea fedha shirika. Aidha, Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari imedhamiria kukaa pamoja na Wizara ya Fedha na Wizara ya Habari ili kujadili suala hili.

Agizo jengine ni kwamba *ZBC* itekeleze vyema dhima yake ambayo ni kutoa habari na vipindi vyenye lengo la kuwaunganisha Wazanzibari wote.

Utekelezaji umefanyika kwa shirika kuanza kutoa habari zenye lengo la kuwaunganisha wananchi.

Agizo jengine, uongozi na watendaji wa Vyombo vya Habari hususan wa Gazeti la Zanzibar Leo wawe makini zaidi kwa kuandika taarifa za uhakika na kuzipitia kwa kina taarifa zinazotaka kuchapishwa katika gazeti hilo, ili kuepukana na upotoshwaji wa taarifa mbali mbali kwa jamii.

Utekelezaji. Hatua zinachukuliwa kwa magazeti kupitiwa na safu ya wahariri wasiopungua watatu, jambo ambalo limesaidia kupunguza makosa ukiondoa yale ya kibinadamu. Aidha, viongozi wa vyombo vya habari hususan wa Shirika la Magazeti wamechukua maoni na maagizo ya Kamati kwa uzito wake na kuongeza nguvu na umakini kwa kupitia taarifa zinazochapishwa katika magazeti yake ili kuepukana na upotoshwaji wa taarifa zinazochapishwa.

Agizo la 16, Kamati imeitaka wizara kuihakiki vizuri *proposal* ya kuunda chombo chengine chenye nguvu na uwezo zaidi wa kuendeleza vitegauchumi vya utalii, ambavyo Shirika la Utalii limeshindwa kuviendeleza ili tusiunde chombo ambacho hakitokuwa na mafanikio.

Utekelezaji. Serikali imezingatia agizo hilo, lakini imetaka kwanza kukamilisha taratibu za kuvunjwa shirika na baadae iwapo tutaona kwamba kuna umuhimu wa kuunda chombo chengine ndipo tuwasilishe pendekezo la kuundwa chombo hicho. Aidha, hivi sasa wizara imo katika hatua za mwisho za kuzikabidhi mali za shirika kwa Kamisheni ya Mitaji ya Umma. Tunaahidi

baada ya hapo tutajadiliana tuone namna ya kupeleka mapendekezo Serikali Kuu juu ya kuundwa chombo chengine.

Agizo jengine, wizara ichukue hatua za makusudi za kufanya mazungumzo na Idara ya Uhamiaji ili kupatiwa takwimu sahihi za watalii wanaoingia na wanaotoka nchini kwa nia ya kudhibiti mapato ya taifa.

Utekelezaji. Katika suala la upatikanaji wa takwimu sahihi za wageni wanaoingia na kutoka Zanzibar, Kamisheni ya Utalii imeshakutana na wadau wa Sekta ya Utalii kuzungumzia suala hilo katika vikao tofauti. Katika kikao cha mwisho cha kujadili suala hilo kiliongozwa na Mhe. Waziri wa Fedha na taasisi zilizohudhuria katika kikao hicho ni Kamisheni ya Utalii, Idara ya Uhamiaji, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Mamlaka ya Bandari, Bodi ya Mapato, Tume ya Mipango na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu.

Uamuzi uliofikiwa ni kwamba kuanzia tarehe 1 Januari, 2014 katika Uwanja wa Ndege kutakuwa na *desk* maalum kwa ajili ya ndege za ndani na kwa Bandarini wauzaji wa *ticket* za boti walioko Dar-es-Salaam watatoa fomu maalum za uhamiaji kwa wageni na kuwataka waziwasilishe wanapofika Zanzibar.

Agizo la 18, Kamati imeiagiza wizara kufanya tathmini ya visiwa vidogo vidogo viliopo Unguja na Pemba kwa ajili ya uwekezaji ili hatimaye wavipangie matumizi bora kwa maendeleo ya taifa.

Utekelezaji. Kamisheni imeshindwa kufanya tathmini ya visiwa kwa ajili ya uwekezaji katika Sekta ya Utalii kutokana na sera ya maeneo hayo ambayo iko chini ya Wizara ya Arfhi, Makaazi, Maji na Nishati, ya kuwa visiwa visiekezwe kiutalii, ila vile ambavyo tayari zimeshawekezwa. Visiwa vilivyowekezwa kiutalii hivi sasa ni Kisiwa cha Chumbe, Kisiwa cha Bawe, Kisiwa cha Changuu, Kisiwa cha Mnemba na Kisiwa cha Pwani. Wizara inayohusika na ardhi inaendelea na kazi ya kuufanyia mapitio mpango mkuu wa matumizi ya ardhi katika ngazi ya kitafa.

Kumalizika kwa kazi hiyo kutapelekea kutengenezwa kwa mipango midogo midogo ya matumizi ya ardhi kwa ajili ya utalii, ambapo utajumuisha matumizi ya visiwa vidogo vidogo. Wakati zoezi hilo likisubiriwa kukamilika, Kamisheni ya Utalii inaendelea kufanya utafiti kubaini vivutio vya utalii viliopo Zanzibar, zoezi hilo linatarajiwa kubaini aina ya utalii unaoweza kufanywa katika visiwa vidogo vidogo hapo baadae.

Agizo la 19, Kamisheni ya Utalii kwa kushirikaina na wizara ichukue hatua ya makusudi kuchapisha majarida, vipeperushi, *DVD* kuvitangazia vivutio vya Zanzibar na kuvisafirisha kwa njia za uhakika.

Utekelezaji. Kamisheni ya Utalii inaendelea na jitihada za uchapishaji wa vielelezo vya utangazaji utalii na kusambaza katika masoko yetu. Kazi hii inafanyika kwa kushirikiana na taasisi tofauti zikiwemo Ofisi za Balozi Tanzania kama vile kuchapisha vipeperushi vya lugha ya Kirusi na kuvipeleka Urusi kwa madhumuni ya kuitangaza Zanzibar kikamilifu katika soko hilo, ambalo Ubalozi wa Tanzania uliopo Urusi ulisaidia kufanya kazi hiyo.

Aidha, mazungumzo yanaendelea baina ya Ubalozi wa Tanzania uliopo Falme ya Kiarabu kuhusu uchapishaji wa vipeperushi kwa lugha ya Kiarabu. Kazi kubwa inayohitajika kufanywa na Kamisheni ya Utalii ni kuvichapisha vipeperushi hivyo na kuvipeleka Dubai jambo ambalo kwa kiasi fulani linawezekana.

Sambamba na hilo, Kamisheni ya Utalii imepeleka picha mbali mbali za vivutio vya utalii vya Zanzibar huko Paris kwa ajili ya kutengeneza kadi ambazo zitatumika katika kuvitangaza vivutio vya utalii vya Zanzibar katika nchi hiyo. Kamisheni ya Utalii imechapisha vipeperushi kwa lugha ya Kichina ambapo mara tu tutakapomaliza malipo, kamisheni itaamuru mchapishaji kuvipeleka vipeperushi hivyo katika Ubalozi wa Tanzania uliopo China. Changamoto inayotukabili katika suala hili ni ufinyu wa bajeti ya utangazaji ambapo vielelezo hivyo huchapishwa kulingana na uwezo wa kifedha uliopo na sio kulingana na mahitaji ya soko.

Agizo la 20, wizara itoe kipaumbele maalum katika kuyaenzi, kuyatunza na kuyadumisha magofu mbali mbali yaliyopo nchini, kwani ndio kielelezo muhimu cha historia ya nchi yetu.

Utekelezaji. Katika kuyaenzi, kuyatunza na kuyadumisha maeneo ya kihistoria, wizara inatekeleza mradi wa ukarabati na ujenzi wa sehemu za kihistoria na mambo ya kale. Ambapo maeneo 22 yamepimwa na kupatiwa hatimiliki, Unguja manane na Pemba 14. Aidha, maeneo saba ya Unguja na saba Pemba yamefanyiwa matengenezo. Vile vile, ukaguzi wa awali wa maeneo ya kihistoria Salhia, Bustani ya Salme, Nyumba ya Wareno Bambi, Pango la Kiwengwa, Kiwanda cha Sukari Cheju na Pango la Wareno umeshakamilika.

Kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014 mradi huu unategemewa kuingiziwa jumla ya shilingi 280 milioni na miongoni mwa maeneo yaliyomo katika

mradi huu ni Mkumbuu, Chwaka, Tumbe, Mkamandume Pujini, na Ungujaukuu.

Agizo la 21. Katika kuepusha taarifa potofu kuhusu maeneo mbali mbali ya kihistoria yaliyopo hapa nchini, wizara iandae mkakati maalum utakaohakikisha kuwa maelezo sahihi ya kihistoria. katika maeneo hayo yanaandikwa na kutunzwa vizuri.

Utekelezaji. Wizara imefanya utafiti wa maeneo muhimu ya kihistoria ambayo yanatembelewa na wageni ili kupata taarifa sahihi za maeneo hayo. Kwa sasa ukusanyaji wa taarifa umeshafanywa na kazi ya kuzifanyia uchambuzi taarifa hizo inaendelea. Upatikanaji wa taarifa hizi utasaidia watembezaji wa wageni kutoa taarifa sahihi zinazohusiana na historia ya maeneo hayo.

Agizo la 22, Kamati inaishauri wizara kufanya upembuzi yakinifu ili kufahamu sababu halisi zinazokifanya kituo cha michezo kuwa katika hali isiyoridhisha hadi sasa. Aidha, Kamati inaona kuna haja ya wizara kufuatilia zaidi katika mamlaka husika ili kujua fursa zinazostahiki kupatikana kutokana na kuwepo kwa kituo cha *academia* ya michezo Dole.

Utekelezaji. Wizara imefanya upembuzi yakinifu juu ya hali ya kituo hicho. Miongoni mwa sababu zilizopelekea kudhorota kwa ustawi wa huduma za kituo hicho ni kumalizika kwa fedha za awali zilizotumwa kutoka ***Olympa*** Africa kabla ya hatua ya ujenzi iliyotakiwa kufikiwa. Aidha, kuchelewa kutumwa fedha za kumalizia shughuli za ujenzi pamoja na mambo mengine muhimu, ndio iliyochangia kukifanya kituo kisiwe katika hali nzuri, kwa sasa fedha hizo tayari zimetumwa na kazi zinaendelea vyema.

Wizara imefuatilia upatikanaji wa fursa zaidi kutoka *TOC* na kugundua baadhi ya upungufu katika baadhi ya maeneo kama vile mafunzo, mashindano ya kimataifa, misaada kutoka nje, uwakilishi wa Tanzania kimataifa. Wizara inayafanyia kazi mambo haya ili kuyapatia ufumbuzi.

Agizo la 23, Kamati inataka Baraza la Taifa la Michezo kukitupia macho kituo hiki kila hali inaporuhusu, hasa wakati zinapotokea safari za watoto nje ya nchi, kwani tumebaini kuwa wafadhili wa *Olympa* Africa huishia kwenye nauli tu za watoto hao pamoja na walimu wao bila ya kupatiwa fedha za kujikimu wanapokuwa safarini.

Utekelezaji. Katibu wa Baraza la Taifa la Michezo kwa mashirikiano ya Rais wa Kamati ya Olympic Tanzania (*TOC)* na Mkurugenzi wa kituo hicho wameandaa andiko maalum linalolenga kuimarisha shughuli za michezo na

mandhari ya kituo hicho na kukiwasilisha kwa washirika wa maendeleo. Aidha, Baraza la Taifa la Michezo kwa makusudi limetengewa fedha katika bajeti ya mwaka huu kusaidia shughuli za *academia* hiyo.

Agizo la 24, wizara iandae utaratibu wa kutafuta hatimiliki ya eneo la *academia* ya michezo Dole ili kulinda lisivamiwe.

Utekelezaji. Kituo cha *academia* ya Dole tayari kimepata hatimiliki ya eneo hilo, hatimiliki ilikuwa ndio miongoni mwa sharti la msingi la mdhamini ambaye ni Olympa Africa katika ujenzi wa kituo hicho.

Agizo la 25, Wizara iwe karibu zaidi katika kukiendeleza kituo cha *Academia* cha michezo Dole. Ikiwa ni pamoja na kukipatia kituo hicho maji, umeme vyoo, uzio na njia ya kufikia kituo hicho kwa urahisi zaidi. Kamati ya *Olympic* Tanzania ndio wamiliki wa kituo hicho kupitia taasisi hii ya *Olympic* Afrika. Waliodhamini ujenzi wa kituo wanaendelea na hatua za kukipatia huduma muhimu kama vile maji, umeme, vyoo na njia kwa mujibu wa matakwa ya mradi wa ujenzi wa kituo hicho.

Aidha wizara kupitia Baraza la Taifa la Michezo imeendelea kusaidia na kufatilia kwa makini utekelezaji wa masharti ya mahitaji ya mradi huo pamoja na fursa nyengine kutoka *TOC*.

Agizo 26, Kamati unautaka uongozi wa redio jamii Micheweni kupanda miti kwenye mizunguko ya eneo lao ili kulidhibiti vizuri katika kipindi hiki cha kusubiri kupatia hatimiliki. Utekelezaji jitihada za kupanda miti katika eneo la Radio ya Jamii Micheweni huwa zinaendelea kila siku ingawa miti hiyo huwa inakufa kutokana na jua kali liliopo katika ukanda huo wa kisiwa cha Pemba.

Agizo 27, Kamati imeagizwa kujengwa tena kwa nguzo za misikiti pamoja na kuyafukua maeneo yaliyojifukia katika ngome ya Mkamandume. Utekelezaji ujenzi wa nguzo za msikiti upo katika mradi wa uhifadhi wa maeneo ya kihistoria ambapo sasa fedha hizo hazijapatikana na ujenzi huo utafanyika mara tu baada ya kuingiziwa fedha hizo.

Agizo la 28, Wizara ifanye juhudi za kuimarisha Uwanja wa Gombani Pemba kwa kutia rangi na kuuweka katika hali ya usafi muda wote. Utekelezaji hatua ya kuezeka bati *VIP* tayari imefanyika na utiaji rangi umeanza. Lakini haujakamilika kwa sababu fedha hazijapatikana za kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha mawasiliano yangu na Mwenyekiti, aliokuwa akiongoza kikao jana kwamba nilihitaji dakika 40 kuwasilisha hoja.

Lakini kwa sababu hali yangu kuwa nzuri leo asubuhi imeniwezesha kutumia muda kasoro ya ule niliouhitaji jana.

Sasa kabla ya kumaliza kuwasilisha utekelezaji wa maagizo ya kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi, naomba tena kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti wa kamati ya Mifugo na Wajumbe wake kwa namna ambavyo wanavyoishauri kuielekeza kwa ufanisi wizara yangu jambo ambalo kwa kweli limesaidia kutatua changamoto zinazoikabili wizara yangu mara kwa mara.

Kwa kweli kamati hii imekuwa ikinisaidia sana mimi kama msimamizi wa wizara na kwa kweli imekuwa inanishauri. Ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza tukufu wataendelea kushirikiana na wizara yangu katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

Mhe. Mlinde Mbarouk Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (*Subhana Wataala*) kwa kutujaalia neema zake na kutuwezesha kuendelea kua hai tukiwa wazima wa afya njema.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 108 (14) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2012, naomba kuwasilisha taarifa ya shughuli za Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari imepewa majukumu ya kusimamia wizara zifuatazo:-

1. Wizara ya Habari, Utamaduni , Utalii na Michezo
2. Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2013/ 2014 , Kamati ilitekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Kanuni ya 115 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi. Majukumu hayo yalitekelezwa kupitia ziara mbali mbali katika Wizara na Taasisi zinazosimamiwa na Kamati hii pamoja na kujadili taarifa za utekelezaji na utendaji.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, kamati ilifanyakazi zake kwa muda wa wiki sita hapa Unguja kuanzia tarehe 09/09/2013 hadi tarehe 20/09/2013, tarehe 18/11/2013 hadi tarehe 29/11/2013, na kuanzia tarehe 30/12/2013 hadi tarehe 10/1/2014. Hata hivyo, kabla ya kuanza kwa

mwaka wa fedha wa 2013/2014 , kamati ilifanyakazi huko Pemba kwa muda wa wiki mbili kuaanzia tarehe 15/5/2013 hadi tarehe 24/5/2013 kwa lengo la Kufuatilia utekelezaji wa bajeti katika Taasisi za Serikali kwa kipindi cha Aprili- Juni 2013.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu Kimsingi imeridhika kiasi na utendaji wa wizara zote mbili tulizozitembelea . Kamati inawapongeza watendaji wote wa wizara hizi kwa juhudi kubwa wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao licha ya mazingira magumu wanayokabiliana nayo.

Mhe. Mwenyekiti,, naomba sasa kwa heshima niwasilishe mbele ya Baraza lako Tukufu, muhtasari wa taarifa ya utekelezaji wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa mwaka huu wa fedha wa 2013/2014 kama ifuatavyo;-

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ina dhamana ya kusimamia sekta kuu nne (4) ambazo ni Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) linaendelea na majukumu yake vizuri na hivi sasa liko katika hatua za kuziimarisha *studio* zake kwa kuziwekea vifaa vya kisasa. Hadi Kamati inapokea taarifa hii (mwanzoni mwa Januari 2014) , awamu ya pili ya utiaji wa *tiles* katika jengo la *Karume House* ilikua imekamilika na awamu ya tatu ilitarajiwa kuanza wakati wowote ambapo kwa upande wa Pemba matengenezo ya awali yalikuwa yanaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, imesikitishwa na matumizi ya Jengo la zamani la *ZBC Radio* liliopo Rahaleo ambalo limebadilishwa matumizi yake na kufanywa kuwa nyumba ya starehe, ambapo hivi sasa linakodishwa na kufanyiwa shughuli mbali mbali za kijamii zikiwemo harusi, *birthday* n.k na kupoteza haiba au makusudio ya jengo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi , *Studio* mbili za *ZBC Radio* nazo hivi sasa zinatumiwa na Shirika la Magazeti la Zanzibar leo. Hali hii inachangia kwa kiasi kikubwa kudhoofisha utekelezaji wa mipango na kujiimarisha kihabari kwa *ZBC*. Hapa Kamati inaishauri serikali kuangalia upya uamuzi wa matumizi haya ambao hauendi sambamba katika kurithi na kuthamini kwa kiasi kikubwa. Mchango wa wafadhili waliojenga *Studio* hizo kutokana na kwamba zinatumika kinyume na madhumuni yaliyokusudiwa.

Aidha, Kamati inaitaka serikali kuharakisha upatikanaji wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mradi wa *Sony* kwa lengo la kuimarisha vifaa vyake ikiwemo ununuzi wa *Microwave* kwa upande wa *TV* pamoja na *Link* kwa Upande wa *Radio* ili kuiwezesha *ZBC* kuweza kurusha moja kwa moja matangazo yake na kuacha kutegemea vituo vingine wakati wa kurusha Matukio Makubwa ya Kitaifa.

Shirika la Magazeti Mhe. Mwenyekiti, kamati imebaini kwamba , Shirika hili linaendelea na majukumu yake vizuri ingawa linaendelea kujibana Katika jengo la *ZBC Radio*. Kamati imegundua kwamba Shirika limeweza kuchapisha magazeti kama ilivyopangwa na kuyasambaza katika maeneo mbali mbali ya Unguja, Pemba na Tanzania Bara:

- Kamati imegundua kwamba ukosefu wa fedha ni kikwazo cha kukiendeleza kiwanja na Michoro inayokusudiwa kujengwa Ofisi na Kiwanda cha magazeti ya Shirika hilo huko Tunguu.

- Kutokuwepo Mitambo ya kuchapishia magazeti ya rangi Zanzibar kunapelekea mzigo mkubwa wa gharama Shirika hilo. Kamati imegundua kwamba Shirika hilo linatumia asilimia 73.29 % ya ruzuku pamoja na asilimia 50% za makusanyo yake kuchapishia magazeti huko Tanzania Bara.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inashauri kwamba Mradi wa Ujenzi wa Ofisi na Kiwanda cha Kuchapishia Magazeti ya rangi hapa Zanzibar uingizwe katika Miradi ya maendeleo katika bajeti ya Maendeleo ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa Kazi za Kamati, pia tulitembelea baadhi ya Vituo Binafsi vya Matangazo ya *Radio* na *TV* ikiwemo *Zanzibar Cable*, *Coconut FM*, *Radio Al-nour FM* na kuangalia shughuli za Utendaji wa Taasisi hizo ambapo kwa kiasi Kamati imeridhishwa na Utendaji wa Vyombo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa ujumla Kamati imegundua kwamba katika vyombo vya habari vya watu binasfi kumekua na ufanisi wa kazi na vimejipanga vizuri na hivyo, Kamati inawasiwasi kwamba kutokana na mwenendo uliopo hivi sasa, vyombo vya serikali vinaweza kukimbiwa na wasikilizaji na watazamaji.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imefurahishwa na mwamko wa jamii mbali mbali kwa kuanzisha vituo vya Redio jamii hapa nchini. Kamati inaamini kwamba

vituo hivyo ni muhimu na vinasaidia kushajihisha jamii husika katika masuala mbali mbali ya kimaendeleo, burudani , michezo na ustawi wa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kamati pia inaipongeza Tume ya Utangazaji Zanzibar kwa kukamilisha kuzinduliwa kwa Redio jamii huko Tumbatu na pia kwa kuendelea kuzingatia maombi ya jamii ya watu wa Mkoani kuhusiana na uanzishwaji wa Redio jamii ya watu wa Mkoani Pemba.

Redio Jamii- Mtegani *FM*, Mhe. Mwenyekiti, kamati ilitembelea Kituo hicho mnamo tarehe 31/12/2014 na iliarifiwa kwamba Redio Mtegani *FM* ni Kituo cha Redio jamii ambayo imeazishwa rasmi na Ndugu Ramadhan Bilali Jihadi aliyekua na umri wa miaka 14 baada ya kuunganisha mabaki ya Redio chakavu na kufanya utundu wa mabaki hayo na kuvumbua mawimbi ya sauti yaliyoruka umbali wa kilomita 8 mwaka 2010.

Kutuo hicho kinaendesha shughuli zake kwa msaaada mkubwa unaotoka katika shirika la *UNESCO* na hivi sasa kinaimarika na inasikika takriban sehemu zote za Mkoa wa Kusini Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, kijana aliyeanzisha Redio hiyo ni hazina kubwa kwa taifa. Hivyo, ni vyema kwa serikali kumuendeleza kitaaluma kijana Ramadhan Bilal Jihadi ili kukuza kipaji chake.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba Sheria za *UNESCO* zinakataza Redio jamii kuwa na mikono ya serikali, lakini hata hivyo ni vyema kwa serikali kuandaa utaratibu utakofaa ili iweze kuziendeleza Redio kama hizi ambao zinaonekana kua ni muhimu na zina nafasi kubwa katika jamii husika.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu haikuridhika na utendaji wa Kampuni ya *Zanzibar Multiplex* (*ZMUX*) inayoshughulikia na kazi ya kusimamia miundombinu ya matangazo ya *digital* hapa Zanzibar. Aidha mradi huo wa *Digital* unaosimamiwa na wawekezaji wa *AGAPE* bado unajikongoja mno.
Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko mengi na shutuma mbali mbali kutoka kwa makundi tofauti ya jamii kuhusiana na uendeshaji wa mradi huu. Kamati inasikitishwa sana na Mikataba ya usimamizi na Uendashaji kati ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na Wawekezaji wa *AGAPE* kwamba haifahamiki vizuri. Aidha Kamati imegundua kwamba Shirika la Utangazaji Zanzibar halikushirikishwa kikamilifu katika maamuzi na pia mapato yanayopatikana katika mradi huu wa *Digital*.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia imegundua kwamba Mradi huu unaitia hasara serikali kwa kuwa unatumia wataalamu na rasilimali za serikali na pia umeshindwa kukidhi mahitaji ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kamati inaamini kwamba Wawekezaji wa *AGAPE* wameshindwa kazi na wanaitia hasara serikali, Kamati inaitaka serikali kupitiwa upya Mikataba ya Ujenzi wa Miundombinu na Uendeshaji wa *Digital* kati ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na Kampuni ya *AGAPE*.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inasikitishwa na kasma ndogo inayotengewa Sekta ya Utalii katika bajeti ikizingatiwa kwamba hii ni sekta kiongozi ya uchumi wa taifa. Kamati inaiomba serikali iangalie na kulizingatia suala hili kwa vile Utalii ndiyo Sekta kuu inayoongoza katika kukuza pato la Taifa.

Aidha**,** upatikanaji wa Takwimu sahihi za watalii wanaoingia nchini na Suala la Ulinzi na Usalama wa wageni na wawekezaji pamoja na mali zao, bado ni tatizo kubwa linaloikabili Kamaisheni hiyo na Taifa kwa ujumla.

Kamati inaipongeza wizara kwa kuufanyia matengezo makubwa Uwanja wa Amani, ambapo kazi za uwekaji wa Nyasi Bandia pamoja na kuimarisha miundombinu mengine uwanjani hapo imekamilika.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaiomba Kamisheni iendelee kukitunza kiwanja hicho cha Amani na kukiendeleza zaidi na pia inashauri Kiwanja hicho kiimarishwe zaidi ili kiendane sambamba na viwango vya *FIFA*.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inalenga kuongeza ajira , Pato la Taifa, lishe bora na kupunguza umasikini kwa wananchi na kuwepo uhakika wa chakula kwa kila kaya hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa kazi za Kamati, tulitembelea Miradi mbali mbali pamoja na vituo mifugo. Tatizo kubwa tulilolibaini ni ugonjwa wa Mahepe unaoshambulia kuku, njiwa na bata mzinga hasa kwa wafugaji wa Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, kupanda kwa gharama za uzalishaji wa mifugo na ongezeko kubwa la bei za vyakula na madawa ya mifugo, nalo ni tatizo kubwa kwa wafugaji na wananchi wetu na kupelekea kushindwa kuingia katika biashara ya ushindani.

Mhe. Mwenyekiti, kamati pia ilipata nafasi ya kutembelea vikundi mbali mbali vya wafugaji, Wafugaji na Wajasiriamali wa Mazao ya Mifugo pamoja na Mfugaji maarufu wa Kandwi, ndugu Ame Khamis Ame.

Aidha Kamati ilikutana na Wafugaji wa Wilaya ya Magharibi na Wilaya ya Kati kwa lengo la kufahamu Mafanikio na Changamoto zinazowakabili.

Mhe Mwenyekiti, kamati imebaini kwamba Maafisa wa mifugo hawafanyi ziara za mara kwa mara kwa wafugaji na badala yake husubiri kupelekewa matatizo ya wafugaji maofisini. Hili ni tatizo sugu ambalo linahitaji ufumbuzi wa kudumu. Vile vile, Kamati inasikitishwa na mwenendo wa serikali kutokana na miradi mbali mbali inayoianzishwa na baadae kukosa kuendelezwa pale mradi unapomaliza ufadhili.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imesikitishwa na kushtushwa baada ya kupokea taarifa za Uvamizi unaoendelea katika shamba la Mifugo Pangeni huko Mkoa wa Kaskazini unguja. Hili si suala la kuchukuliwa mzaha hata kidogo, kwani vitendo kama hivi vimekua vikiendelea katika sehemu mbali mbali zinazomilikiwa na serikali na kuleta usumbufu mkubwa pale serikali inapotaka kuyatumia maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa serikali haina hati miliki ya Ardhi katika Shamba hilo ambalo inalimiki kwa kipindi kirefu sasa, tunaiagiza serikali kuitafuta hati miliki hiyo ili kujiepusha na usumbufu unaoweza kujitokeza hapo baadae.

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi ina majukumu makubwa ya kuendeleza Uvuvi na Uhifadhi wa Viumbe na mazingira ya bahari. Wakati wa kazi za Kamati, tulikutana na watendaji wa sekta hii pamoja kutembelea Madiko na Masoko mbali ya mbali pamoja kumtembelea Mradi wa Ufugaji wa Samaki wa Maji ya Baridi – Manga Pwani.

Vile vile, Kamati ilikutana na Wavuvi wa Wilaya ya Kaskazini A na Wilaya ya Kaskazini B na kupata maelezo juu ya Changamoto na Mafanikio yao.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu imegundua kwamba wavuvi katika sehemu kadhaa hawana hati miliki za Ardhi katika madiko wanayotumia ikizingatiwa kwamba hivi sasa maeneo mengi yamekuwa yakivamiwa na kuuzwa kiholela.Hivyo, tunatowa mapendekezo yetu kwa wizara kutafuta hatimiliki hizo ili wavuvi wetu waendelee kuyamiliki madiko hayo.

Baadhi ya wavuvi wamekuwa na wasiwasi kwamba kuna baadhi ya visiwa vidogo vidogo vinavyotegemewa sana na wavuvi vinauzwa au kukodishwa kinyemela kwa wakezaji na hatimae kuwazuia wavuvi na wananchi wa sehemu hizo wasivitumie ipasavyo visiwa hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inasikitishwa sana na hatua za serikali katika mchakato mzima wa Ununuzi wa Boti kwa ajili ya uvuvi wa habari kuu. Kamati inahisi kwamba Mchakato huo unaenda pole pole mno, suala ambalo linazidi kuwaondolea matumaini wavuvi wetu. Tunaiomba serikali iharakishe

kutengeneza *"Busness Plan*" itakayoongoza katika mchakato wa ununuzi wa boti hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijakamilisha Muhtasari wa ripoti yetu, Kamati ya Mifugo, Uwezeshaji , Utalii na Habari inawashukuru sana Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zote zinazosimamiwa na Kamati hii, kwa kuweza kutoa mashirikiano makubwa ya kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa mwaka huu. Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata.

Hata hivyo, kasoro kubwa iliyogunduliwa na Kamati ni Upatikanaji wa fedha kutoka serikalini kwamba umekwamisha kwa kiasi kikubwa malengo na shabaha za Wizara zote mbili zinazosimamiwa na Kamati hii hasa katika Miradi ya Maendeleo.

Vile vile, upatikanaji wa fedha za *OC* pamoja na vitendea kazi, usafiri na malipo ya muda wa ziada wa kazi (*overtime*), navyo vimekuwa vinarejesha nyuma mwamko na ufanisi wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti**,** napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kuwa katika kipindi cha mwaka 2013/2014 Kamati yetu imetekeleza jukumu lake la kuishauri na kuisimamia serikali kwa Wizara, Taasisi na Idara tunazozisimamia kwa niaba ya Baraza lako.

Mhe.Mwenyekiti, napenda kukushukuru tena na kukupongeza wewe binafsi kwa unavyoliongoza Baraza letu katika nafasi ya Uspika. Napenda pia kuwapongeza Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kukusaidia vizuri katika kufanikisha shughuli za Baraza.

Hata hivyo, kwa heshima, Kamati inaliomba Baraza la Wawakilishi kufanya Marekebisho ya Jina la Kamati hii kwa kuondosha neno "Uwezeshaji**"** kwa kuwa masuala ya Uwezeshaji hivi sasa yanashughulikiwa na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii na pia kuongeza Neno "Uvuvi" kwa lengo la kuitukuza sekta ya Uvuvi hapa nchini.Kwa hivyo, Kamati inapendekeza jina lake hivi sasa lisomeke kama ifuatavyo:

"Kamati ya Mifugo, Uvuvi , Utalii na Habari"

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa Ushirikiano mzuri katika kufanikisha majukumu tuliyojipangia. Michango, mawazo na ushauri wao kwa kiasi kikubwa yamefanikisha majukumu ya Kamati ya Mifugo, Uwezeshaji, Utalii na Habari. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Mwenyekiti.
2. Mhe. Abdullah Mohammed Ali - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Bakari Makame - Mjumbe
4. Mhe. Mussa Ali Hassan - Mjumbe
5. Mhe. Amina Idd Mabrouk - Mjumbe
6. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali - Mjumbe
7. Mhe. Asaa Othman Hamad - Mjumbe
8. Mhe. Kazija Khamis Kona - Mjumbe

Mhe. Mwenyekiti, Napenda kumshukuru Katibu wa Baraza na Watumishi wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake .

Aidha kipekee, kwa niaba ya Kamati nawashukuru ndugu Himid Haji Choko na Ndugu Rabia Shaaban Juma ambao ni Makatibu wa Kamati yetu kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati kwa kipindi chote hadi taarifa hii inapotolewa mbele ya Baraza lako Tukufu.

Napenda pia kutoa shukurani za dhati, kwa usikilizaji mzuri wa Waheshimiwa Wajumbe wakati wote wa Uwasilishwaji wa hotuba hii na tunatoa wito kwa serikali kuyatekeleza kwa vitendo yale yote yaliyoagizwa na kushauriwa na Kamati ili kuongeza ufanisi wa Wizara hizo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa unatakiwa kuwasilisha sio kutoa hoja.

Mhe. Mlinde Mbarouk Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakubali ushauri wako kwa sababu juzi niliwasilisha kwa mara ya kwanza, nilidhani leo nitoe hoja ili Wajumbe waweze kuichangia. Basi naomba kuwasilisha.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, leo nimeamini kila wilaya zina kauli zake au kila wilaya zina tafsiri zake za maelezo. Mhe. Mwenyekiti, Wilaya ya Kaskazini "B", Mhe. Mwenyekiti wangu hakukosea, amesema kuwa anatoa hoja kutokana na lugha ya kinyumbani. Katoa hoja Wajumbe wachangie. Ameshawasilisha juzi akisema leo anawasilisha tena itakuwa kwa mara mbili. Naomba Mheshimiwa masahihisho haya Kiswahili yakubaliwe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naanza na uvuvi. Kwanza niwashukuru sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu wake, Wakurugenzi na wataalamu wao. Mhe. Mwenyekiti, mimi leo hapa nina ushauri. Nimeeleza jamani kuwa msitafute washauri wa kigeni tuwe na washauri wazalendo.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona hali sasa hivi ni ngumu sana ya uvuvi wa bahari kuu. Na kwa kuwa wananchi wetu hawana vyombo vya kufika kule, na kwa kuwa katika eneo moja la kuwaondoshea umaskini vijana wetu katika uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, natoa ushauri wangu, na kama wataufuata Serikali kwa kupitia Wizara yake, basi nikasema kuwa sasa tunakusudia kuwasaidia vijana kuwaondolea umaskini kwa njia ya uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, uvuvi uko namna nyingi. Lakini huu uvuvi ninaotaka kuuleta mimi ni wa aina ya peke yake tena ni rahisi sana. Mambo ya ki-*technician* watajua wao wenyewe. Lakini kwa mtazamo wangu ni rahisi sana katika nchi niliyokwenda kutembelea. Mhe. Mwenyekiti, kuna ufugaji wa samaki ndani ya bahari kama wapo wataalamu watasema nasema uongo au vipi. Mhe. Mwenyekiti, taaluma hiyo wanawekewa kama uzio fulani ambao ndio watakuwemo mule samaki, na mhusika mwenyewe atakuwa analishia atawaweka kwa matabaka. Huku anawafuga, huku anaanza kuvuna. Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sasa taaluma hiyo tuichukue kutoka kwa Profesa Mshimba bure tu. Hiyo haitaki fedha za kigeni.

Lakini la pili kuna maeneo ya juu ya kuwashajiisha watu wetu. Lakini mimi nashangaa tumefanya kwa mfano kama kule Bumbwini alikotoka Mheshimiwa wangu hapa mliyemkatalia lugha yake, lakini ni sahihi. Kule tayari wapo watu wa aina kama hiyo, lakini basi ndio kule tu. Mhe. Waziri tuwe *serious* katika suala hili, tuanze kufanya kampeni ya hali ya juu. Jamani Mawaziri, Serikali msione tabu kuwekeza majina kwa kuleta maendeleo katika nchi yenu. Lakini kila siku tutafanya, tutafanya, lini? Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli haya masuala mimi nasema siku zote hatukuwa *serious.* Tuliwaletea viboti wananchi wetu lakini havikuwa na *power* ya kwenda katika bahari kuu, unafikiri utajiri huo utapatikana wapi? Na tukisema tungojee boti kubwa itakwenda bahari kuu tuta-*survive* hatuna kimoja tutakitia twende tukirudi. Mambo yapo hapo chini chini haya ya kuweza kupata.

Naomba ushauri mmoja ili waweze kuufuatilia. Tena kwenye bajeti waniambie kuwa Mheshimiwa eneo fulani kaangalie tayari tumeshawekeza masuala kama hayo. Sitaki tena mjadala tumeshachoka. Sitoipitisha bajeti, na ndio maana nikasema bajeti kuu tusiipitishe mwanzo kwa sababu hawa watakuwa wanatiririka tu.

Mhe. Mwenyekiti, la pili tumezungumzia wafugaji wadogo wadogo. Tunakwenda tu tunahamasisha wananchi, wananchi wanahamasika. Lakini wakihamasika Serikali inakimbia haiwekezi tena pale. Ushauri wangu Mhe. Mwenyekiti, sasa katika kuhamasisha kwanza lazima tuwape elimu ya kutosha ndipo waweze kuwekeza. Kwa sababu fedha nyingi zimepotea. *PADEP* hapa wamekwenda kununua magombe mabovu kabisa. Jimbo la Kitope tulikuwa na ng'ombe wengi sana katika *PADEP* tumenufaika leo katizame sijui kama wapo. Fedha nyingi tu zimepotea, mbuzi tunaambiwa wa maziwa hana lolote. Pesa hivi jamani za wafadhili. Mimi naomba suala hili tuwe waangalifu sana katika kufuga.

Mhe. Mwenyekiti, ukichukulia mfano hebu njooni kule shambani kwangu muangalie jinsi gani hivyo vitu vimepatikana *quality,* mbuzi wa maziwa wapo ambao wanatoka nchi za nje na ni *quality,* bata mzinga ambao ni *quality* kutoka nje. Lakini nyinyi watu wanakwenda kununuliwa mibata mibovu tu. Mhe. Mwenyekiti, mimi sipendi namna hiyo, fedha hizi tuziheshimu. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Waziri tuwe *serious,* msione tabu kupita na sisi tukakusaidieni maarifa. Hakuna mtu mwenye akili yake peke yake ambaye anaweza kutosheleza lazima akili ziongezeke. Naomba Mheshimiwa kwa hilo namuacha mwenye uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana ripoti yao hii nakubaliana nayo hakuna tatizo marekebisho madogo madogo hapa na pale tu. Na ahadi nyingi niwapongeze wamezitekeleza sana tu, hiyo ni moja katika kuonesha heshima kubwa kwa Kamati zetu za Baraza hili. Hilo moja nakubaliana nalo lakini na ushauri wangu wautilie maanani, namwona Naibu anaandika.

Mhe. Mwenyekiti, naingia kwenye habari hapa ndio kwenye habari hasa. Namuomba sana Mhe. Waziri hapa anisikilize kwa makini. Mhe. Mwenyekiti, kwanza naingia hawa watu wetu wa humu ndani wa kamera.

Mhe. Mwenyekiti, nasikia mpaka leo hata pesa zao za mwaka jana hawajalipwa kwa shilingi elfu tano tu. Inasikitisha sana hebu angalieni mimi nakaa kwenye kiti tu sitimizi masaa kama wanavyosimama wao natoka nje kwa sababu gesi. Je, wale si watavimba miguu kama wapiga beni. Haiwezekani lazima tuwahurumie. Waandishi wetu maskini ya Mungu vitoto vya kike vijasiri, wanaume nao wajasiri wanasimama kwa masaa ambayo mpaka tunaondoka sisi japo wanavumilia lakini muda mwingi. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, hichi kibakaa basi tunashindwa kuwapa shilingi elfu tano na tulisema waongezewe hapa. Inasikitisha sana hatuwatendei haki.
Wenzetu nchi za nje hawa ndio wanawathamini sana kwa sababu wakitaka kutukorofisha dakika tatu hazitimii. Waandishi wa habari ni watu hatari sana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana tuwathamini hawa watu. Leo jua likitua utwambie umeshawalipa naomba sana mimi nakujua Mhe. Waziri mtu *active* sana kwa suala kama hilo. Katafuteni popote pesa lakini muwakamilishie pesa zao muwape.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Sekta ya Utalii hapa ndio kwenye mambo. Mhe. Mwenyekiti, sasa natoa ushauri wangu mwengine na huo ushauri ambao mnisaidie na nimeamua kwa makusudi kuwaokoa vijana wangu sasa. Huenda nikawa Rais wa Vijana mwakani iko siku tu, lakini panapo uhai nitakuwa Rais wa Vijana katika nchi hii, potelea mbali lakini vijana wataondokana na umaskini.

Mhe. Mwenyekiti, nimeamua sasa kuunda kampuni ambayo ina jina hili " OKOA AJIRA ZA VIJANA ZANZIBAR". Hiyo ndio kampuni nitakayounda sasa, sina njia, kila njia nikifanya hivi naona vijana hawafaidiki. Sasa nawafungulia kampuni vijana hiyo itakuwa ni *final case* na tuone msisaidie Serikali. Wamechoshwa vijana. Mheshimiwa kampuni hiyo uje kuiunga mkono, mimi nakujua Mhe. Waziri hii kampuni uiunge mkono si mchezo. Sasa ajira zote za mahotelini zitapitia katika kampuni hii. Mhe. Mwenyekiti, vijana hawa ni watu ambao *dangerous age*, vijana lazima tuwatetee, tuwalinde.

Mhe. Mwenyekiti, kampuni hii ipo kwenye *process* na nakuhakikishia itakuja kuundwa na wewe ndio utakuwa mzinduzi kwa kampuni hii, sasa tuone leo vijana wasipate kazi. Haiwezekani hotelini utakuta watu wengi wa nje wazalendo hawana kazi. Tungekuwa na *plan* kwa sababu kuna vitu vyengine vinakosekana kuwa na *plan.* Unaweza ukawa na vitu lakini ukawa huna *plan* navyo. Sasa tuwe na *plan* kwa makusudi. Hebu tusifichane wewe ulinambia siku moja kweli umeshindwa na kosa moja mimi nilikuwa sipo, lakini ulinikubalia ziara kweli, utalia hotelini kule Wakenya, Wazambia, Mzanzibari yumo? Hayumo. Mhe. Mwenyekiti, naomba nikomee hapo *message* imefika na kampuni iko njiani na viongozi nyote mmei-*support* kwa sababu hii mmeambiwa "OKOA AJIRA ZA VIJANA ZANZIBAR".

Mhe. Mwenyekiti, naingia kwenye michezo. Mhe. Mwenyekiti, sikuomba mimi Makamu Mwenyekiti wa Riadha kwa kutaka sifa, hapana sina sifa hizo mimi, nina sifa za utendaji, nipe sifa za utendaji, sio sifa za kuvaa koti mimi Makamo wa Rais au Makamu wa Riadha siitaki hiyo nataka utendaji.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona riadha Zanzibar imekufa nikaona mimi niifufue na nikaona niombe na nikaifufua sikubali ng'o, tuliposhindwa hatukubali kushindwa tutaendelea mbele. Mhe. Mwenyekiti, mimi nashangaa sana, halafu Mhe. Waziri nataka nikupe wazo jengine zuri tu. Mhe. Mwenyekiti wa

Baraza asichaguliwe na Rais turekebishe sheria achaguliwe na vilabu. Kwa sababu wakati wowote anaweza kutuletea manyago vilabu viweze kumuondoa. Leo hatuwezi kumuondoa kwa sababu sheria lazima atolewe na Rais. Jamani hilo ni *simple* msaidieni Rais tumpunguzie madaraka, hilo ni moja unampunguzia Rais, Rais haoni huku, kila siku Rais anasema riadha, riadha, ataiona wapi na riadha imebanikwa mbaa! Juzi tuliambiwa na sisi tushiriki ndio linaniumiza hili.

Miaka 50 ya Mapinduzi Januari riadha isiwemo, na tumeambiwa mna fedha chungu nzima mmetenga milioni 150 sijui kama kweli au *yaumu shaka* utanambia hivyo, kwa sababu sina uhakika nisije nikapigwa buti. Katika Umoja wa Mataifa riadha inawekwa *number one,* lakini mmekamata nyinyi *football* tu riadha mmeiacha. Mhe. Waziri njoo unambie sababu gani jamani.

Mheshimiwa umetupokea nakushukuru sana na ulifurahi sana kuwa sasa hivi uongozi mpya wa riadha upo na utaleta makeke katika nchi yetu ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, tupo tayari na tumeshaanza tunaweka ratiba ya kwenda maskulini kuwaambia sasa mchezo tunaurudisha tunataka kuleta viwango vya kwenda *olympic* na lazima tuvipate. Hali ya riadha Zanzibar tunataka tuifufue kwa hali na mali, piga ua. Lakini tunaomba mafungu yetu ya fedha sasa mtupe wenyewe hatutaki yapitie kwa Mwenyekiti au kwa nani, tuleteeni wenyewe mafungu yetu kwenye vilabu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi tuna mashindano ya nage na hiyo nage usiidharau kwa sababu wenzetu nao wana michezo mingi tu. Mhe. Mwenyekiti, nimekwenda nimeona michezo ile ya watu wana- *ski* katika *snow* wanakwenda, ni michezo ile, michezo kila aina. Mhe. Mwenyekiti, niwashukuru Umoja wa Vijana wa CCM, nimshukuru na Naibu Katibu wake wa Umoja wa Vijana wameonesha michezo hii kuifufua ndio ile sasa, wewe kazi yako ndogo. Ichukue itengenezee ratiba na wao wajisikie katika mashindano yao. Umeanza *footbal*l ya wanawake nakushukuru sana kombe limeonekana lile, sasa tunataka na nage, nage nayo ina mashindano makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, la kumalizia naomba sana hili suala ulitie katika ratiba ili wananchi waelewe sasa kuwa nage imepokewa kwa mujibu wa utaratibu uipangie sheria kwa Vyama vya Michezo. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu wa Mwenyekiti lazima achaguliwe na vyama vyote vya michezo Zanzibar. Mhe. Waziri katika bajeti yako nakuomba sana uje uniletee sheria tayari iko kwenye chungu ya kuweza kurekebishwa. Mimi nakuamini Mheshimiwa kwa jambo kama hilo unakuwa huna tatizo nalo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kwa heshima na taadhima zote, naiunga mkono ripoti ya Mwenyekiti kwa kuifanyia kazi, na Mwenyekiti nampenda

sana atanisikiliza hili kuitia shinikizo Serikali ili ule ushauri wa bure uwe umekubalika. Ahsante sana.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kwa kutujaalia sote kuwa katika hali ya uzima na afya, *alhamdulillah*.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kuwapongeza Mawaziri wote wawili waliowasilisha ripoti zao hapa kuhusiana na Maagizo ya Kamati. Pia shukrani zangu za dhati ziende moja kwa moja kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa uwasilishaji wake mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu moja kwa moja nitajikita katika Sekta ya Uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, kwanza tukizungumza mambo ya uvuvi tumjue mvuvi ni nani na mvuvi kabeba nini? Nchi yetu hii ni ya visiwa Unguja na Pemba, na visiwa vidogo vidogo vilivyozunguka katika bahari yetu hii. Lakini tukisema mvuvi, uvuvi ni sekta ambayo inabeba watu wengi waliojiajiri kutokana na sekta hii. Ukimtaja mvuvi mmoja ana watu kumi mgongoni wanamfuata, kwanza hilo tulijue. Kwa sababu pale ukija kuna wachuuzi, kuna walaji, kila kitu kinategemea kutokana na mambo ya mvuvi baada ya kutoka baharini.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika visiwa vyetu hivi kuna takwimu wavuvi wanayosema katika Idara hii ya Uvuvi wasiopungua 35,000, lakini mimi nasema laki moja wanazidi katika visiwa vyetu hivi vya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango ambao ni maoni ya Kamati waliyoyatoa katika Sekta ya Uvuvi, Idara ya Maendeleo na Uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba uniruhusu ninukuu. Hapa imesema katika Idara ya Uvuvi na Maendeleo ya Uvuvi. "Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ni miongoni mwa Idara za Wizara ya Mifugo na Uvuvi ikiwa na majukumu makubwa ya kuendeleza uvuvi na uhifadhi wa viumbe na mazingira ya baharini". Mimi katika sentensi hii sina mashaka nayo hata kidogo ndio majukumu yake na ndivyo ilivyo.

Lakini kuna kitu kikubwa ambacho wamekisahau hapa na kimejificha kabisa. Sheria Nam. 7 ya mwaka 2010 inatueleza kitu kimoja kinasema udhibiti. Kwa hivyo katika kuendeleza wavuvi lakini kuna kitu udhibiti. Wale wavuvi wamedhibitiwa kabisa sheria ndio inasema hivyo na inawaangalia sana. Lakini imesema katika udhibiti huu basi tumewafanya wavuvi kutofanya kazi

zao kwa ufanisi hata kidogo. Mimi niishukuru Kamati hii imekwenda na imeona changamoto ambazo wameziona.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na uchangiaji wangu naomba ninukuu tena vile vile katika sentensi hii ya pili anasema

"Aidha, wakati wa kazi za Kamati, Kamati ilitembelea madiko na masoko mbali mbali ya samaki yakiwemo Kidanzini, Kendwa, Nungwi, Marumbi, pamoja na kutembelea miradi ya ufugaji wa samaki wa maji baridi Mangapwani".

Ni vizuri mlivyowatembelea naona hapo changamoto zilivyojitokeza, lakini Kamati mimi nailaumu haikufika kwa wavuvi wa taasisi za kijamii. Kamati ingetembelea taasisi za kijamii basi mambo mengi ingeyapata. Mheshimiwa ulipata tamko kubwa zuri. Hapa ipo Jumuiya ya Wavuvi ya Wakojani ambayo mpaka sasa hivi inawasaidia hata Idara ya Uvuvi. Sasa hivi inaendeleza semina za kuelimisha namna ya sheria hii ya uvuvi, lakini maskini ya Mungu wamewasahau. Na halafu kuhusu hili hili Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii ya Maendeleo ya Uvuvi basi utapata wewe Mwenyekiti na watu wako wawili ili mshiriki kujua hilo. Mimi nawaahidi kuwaalika kabisa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nisiishie hapo katika mambo ya Uvuvi. Imezungumzwa hapa katika changamoto anasema Wizara bado haijatekeleza ahadi yake ya kuwa na boti kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu. Ndani ya Baraza hili la Wawakilishi ukifika wakati wa bajeti tunaambiwa hapa kama Serikali itajikita katika kuelekea uvuvi wa bahari kuu, lakini maskini ya Mungu imekuwa ni hadithi tu. Lakini naangalia mambo haya ni ya muda mrefu si ya muda mfupi.

Mimi ningeishauri Wizara kwa sababu haya ni mambo ya muda mrefu na wanahitaji pesa nyingi, na hata uwepo huo uvuvi wa bahari kuu basi tuna uwezo wa kununua meli hata tatu kama itakuwepo ni meli moja tu. Na meli moja ya kivuvi kama ile ya Magufuli inabeba mabaharia wasiozidi 30 mpaka 35 kwa wingi, bado hujawatendea wavuvi katika kuwakomboa katika matatizo hata siku moja. Ngoma itakuwa iko pale pale. Lakini naomba niishauri Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Idara ya Uvuvi yenyewe kuwa kuna haja ya kuelekea kuunda boti za kati na kati ili kuwasaidia wavuvi ambao zitakuwa na friji ndani kwenda masafa angalau marefu la kuhifadhi samaki siku mbili tatu na baadae watarudi kuja kutiwa katika masoko ya kuuza. Mhe. Mwenyekiti, hilo nalisihi kabisa lakini uvuvi wa bahari kuu bado miaka na miaka unatusumbua.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika changamoto tumesema hapa wavuvi katika sehemu kadhaa hawana hatimiliki za ardhi katika madiko wanayotumia ikizingatiwa kwamba hivi sasa maeneo mengi yamekuwa yakivamiwa kuuzwa kiholela. Hii ni kweli wala sio utani.

Lakini nikiendelea hapo hapo baadhi ya wawekezaji wamekuwa na tabia ya kufunga njia zinazotumiwa na wavuvi na wanavijiji wengine suala ambalo limekuwa likiwapa usumbufu mkubwa katika kazi zao. Mhe. Mwenyekiti, ni jana tu wananchi walioko Kiombamvua pwani ya Nyanjale ilidhihirisha wazi kabisa wamevunjiwa mabanda yao na mwekezaji tayari ameshaweka senyenge njia kuu wanayopitia kwenda katika shughuli zao imeshazuiwa.

Mhe. Mwenyekiti, iko siku wazalendo wa nchi hii watakuwa hata nafasi ya kwenda kujisaidia itawashinda kutokana na utaratibu unavyokwenda. Kama hatukujikita kuangalia wazalendo ni wapi na wana haki gani za kimsingi basi iko siku hawatapata tena nafasi ya kuiona ile bahari kuichungulia kwa macho.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika wananchi wa Kiombamvua wamejipanga kwa biashara ya uanikaji wa dagaa, na wananchi walio wengi pale pana wavuvi boti zisizopungua hamsini zinakwenda baharini na nyingine zinawauzia wafanyabiashara wanaofanya katika biashara ya uuzaji wa dagaa. Lakini maskini ya Mungu vijana tu katika lile banda lao lilivunjwa na kulikuwa na nguvu kubwa ya Serikali kule. Walikuwepo Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini "A", Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini "B" na *defender* mbili za Polisi zilikuwepo kule na wananchi bado wanahangaika. Baada ya kwisha kuvunjwa anaitwa yule mzungu sijui mhindi mwekezaji anaambiwa njoo uangalie, akaja pale kuangalia kazi imetendeka wananchi wanateseka. Hili si jambo zuri, uangalie Rais kachaguliwa na wananchi, na baada ya kuchaguliwa na wananchi kakupendelea pa kukuweka si kuwatesa wananchi, ni kuwatendea haki wananchi. Hiari ya hivi itafika mahali wazalendo hawana haki katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, tuliangalie sana eneo hilo na tuwe makini kabisa mwananchi apate ardhi yake halali, mwananchi kajiajiri katika mambo hayo leo unamfukuza kwa nini? Kulikuwa na vikundi vya Ubaya Ubaya hapa, kikazuka kikundi kingine cha Bom Bom katika nchi hii kutokana na kutowathamini wazalendo wa nchi hii. Mwekezaji kachukua eneo kubwa minazi ipatayo elfu tano imeangushwa pale. Mhe. Subeit Khamis Faki alikuwepo hapa juzi kazungumza kuhusiana na Serikali katika uharibifu wa mazingira, na wewe ulishiriki wakati wa kutengeneza mambo ya miundombinu kaangalie minazi kule. Nataka mtu akitoka hapa aende akaangalie inavyoathirika na mchanga uliochimbwa. Mhe. Mwenyekiti, tuangalie sana katika kutekeleza majukumu tusiwaonee wananchi.

Tuzungumze nao kwa utaratibu baadae ndio *af-wa* itapatikana, lakini nguvu kama iliyotumika jana ile si jambo la msingi kwa watu katika nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea wamezungumza ndani ya changamoto hizo uvuvi haramu naomba ninukuu. "Uvuvi haramu bado unaendelea na jambo la kusikitisha ni kwamba kumekuwa na muingiliano wa maamuzi kutoka taasisi tofauti za Serikali na hata mikono ya wanasiasa wakati idara inayohusika na masuala ya uvuvi, inavyowakamata wavuvi wanaojishughulisha na vitendo vya uvuvi haramu".

Hivi Kamati imepata changamoto hiyo, wanaujua uvuvi haramu ni upi? Naona hapa tumeelezwa uvuvi haramu lakini halali haikutajwa. Dini yetu inakataza mambo machafu na kuelekeza mambo mazuri, bado ingeelekezwa hapa kwamba haya ni haramu na mazuri ni haya. Mimi nasema uvuvi wowote ni haramu kwa hii jinsi inavyokwenda. Hivi mvuvi leo kutumia kioo cha kuangalia hali tu ndani ya bahari ni haramu? Si haramu kabisa, ndio zenyewe zinafanya kazi. Mvuvi kutumia nyavu ni haramu? Si haramu, bila nyavu utavua vipi?

Mimi nataka nimueleze hizo meli zinazovua kwenda bahari kuu, hizo nyavu zao sisi tunazijua na zote zina mabangili tuangalieni sana. Wafanyieni utafiti watu wa uvuvi, Wizara pamoja na Idara zina mabangili. Hakuna nyavu hata moja inayoweza kumvua samaki kama haijatiwa hata uzito mdogo wa kuyagawa maji, hata siku moja huwezi kuvua. Na kaitoe pale ndani inayayuka kwenda baharini kuitupa hatoingia samaki hata mmoja. Haiwezekani, lazima tuujue uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, tuchukue wazoefu wa wavuvi na sisi wengine ni Wakojani ndani ya majimbo yao utapata maelezo. Jumuiya hii ya Wavuvi wa Kojani ichukueni mutapata maelezo si tatizo, mukienda nao sambamba mutapata mengi, angalieni sasa hivi wanavyoendelea wanawafundisha wananchi ili kuweza kujua ile sheria ya uvuvi, lakini ninasema na ule udhibiti ndio unaowakandamiza wavuvi, ndio tukasema uvuvi haramu.

Mhe. Mwenyekiti, jambo hili lazima tulizingatie sana kwa sababu inasemekana hata ndani ya bajeti iliyopita hapa wavuvi kukamatwa ovyo, wavuvi walikamatwa wa Chwaka na Mahakama ikaamua Mhe. Subeit Khamis Faki, Mahakama imeshaamua kupewa vyombo vyao bado wanasuasua kutoa. Mahakama imeona kama mvuvi huyu hana makosa lakini bado wanasuasua. Sasa baada ya Mahakama tukimbilie wapi na mvuvi kaonekana hana makosa.

Sasa wanasiasa kuingia katika mambo haya ndipo wanapoingilia. Hata Mahakama imeingilia wewe unashindwa kutoa ile haki iliyopatikana kuitoa. Ndio maana sisi ni Wawakilishi wa wananchi hatutokosa kuingia hata siku moja, kwa sababu hapa tunawakilisha wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na kutoka kwenye mambo ya uvuvi, niendelee kwenye ukurasa wa 149, hapo kunazungumzwa katika mambo haya ya michezo. Nianze na kunukuu tu. Mhe. Mwenyekiti, wakati wa kazi za kamati tulitembelea Kamisheni ya Utamaduni na Michezo, ikagundulika kwamba Kamisheni inaendelea kiasi katika kuimarisha utamaduni na michezo hapa nchini.

Mimi nakubaliana nao na nampongeza Mwenyekiti wa kamati kwa kuondoa haya na Waziri. Hata mimi kwenye jimbo langu Mhe.Waziri ameshaniahidi kama kutakuwa na tamasha kubwa la kuendeleza michezo, tena ile michezo ya zamani ya asili. Nampongeza sana Mhe.Waziri.

Kwa hivyo Mhe. Waziri naomba ile ahadi uitimize tu kwa sababu jambo kubwa ni ahadi ndani ya Baraza hili. Hivyo lile tamasha la michezo ambalo umekusudia kulifanya katika Jimbo la Kojani na sio Jimbo la Kojani tu, hata Zanzibar uwemo utamaduni huo...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemalizika.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na ahsante sana ninaunga mkono hoja. (*Makofi*).

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Pia naomba niitumie nafasi hii juu ya Ripoti ya Kamati ya Mifugo, Uvuvi, Utalii na Habari kwa ripoti yao na namna Mwenyekiti wao alivyowasilisha vizuri. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu katika sekta ya mifugo kwenye ukurasa wa 151, changamoto na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati. Mhe. Mwenyekiti, changamoto ya mwanzo hapa imeeleza kama baadhi ya wafugaji wanakwepa kupeleka mifugo yao kwenye chanjo na majosho na hili linapelekea kutoa gharama kubwa kwa kuitibu mifugo yao wakati inapopata madhara.

Lakini mapendekezo yanaonesha kama wizara iifanyie marekebisho sheria ya mifugo ili iweze kuwadhibiti wafugaji wakaidi. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaiomba wizara iliharakishe hili kwa sababu hili haisababishi ongezeko la

gharama tu kwa wafugaji, lakini pia linaweza likaleta athari kubwa kwa wafugaji na hata kwa wale wasiokuwa wafugaji.

Mfano Mhe. Mwenyekiti, ugonjwa wa kichaa cha mbwa. Tusitegemee kama mbwa atakapopata ugonjwa atamtafuta mbwa mwenzake au ng'ombe, hata sisi binadamu anaweza akatuathiri. Na hii Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe mfano mmoja.

Siku moja katika kutembea tembea kwangu nilimkuta punda kafungwa katika kigogo cha mti na wale wenye punda walikuwa wakimrushia mawe, magongo na mambo mengine. Sasa mimi nikawauliza lakini yule punda alikuwa akitetemeka sana huku akitoka mate mdomoni. Nikawauliza huyu punda ana tatizo gani. Wakaniambia huyu punda tulimkuta ana jaraha wiki mbili zilizopita. Sasa hatma yake tunamuona yupo katika hali hii, tuna wasiwasi kama ni kichaa cha mbwa. Na niliwauliza mulimfuata daktari wa mifugo? Wakaniambia tumemfuata.

Ushauri aliotupa alitwambia kwa hii hali aliyokwisha kufikia punda, tusubiri afe tu. Sasa nikawauliza yale mawe waliokuwa wakimrushia, wanasema yale mawe wanamrushia kwa sababu atafune yale mawe na magongo asiitafune ile kamba akaja akaikata, kwa ajili wahofia akiikata kamba anaweza akawaathiri binaadamu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tulitazame suala kama hili. Kwa sababu mimi pale akili yangu ilinituma nikaona huu ugonjwa bila shaka hauna tiba, lakini kinga ipo. Sasa ikiwa kinga ipo na wafugaji hawawapeleki mifugo yao katika kupata hii kinga Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo la kuharakisha kuwekewa sheria na wafugaji ambao wakaidi wachukuliwe hatua, kwa sababu hapa tutakuja kupata hasara kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo naomba Kamati itupe maoni yake ni kuhusu hawa mbwa waliokuwa hawana wenyewe. Mhe. Mwenyekiti, katika kikao kilichopita Mhe. Saleh Nassor Juma aliuliza suali hili na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais alilijibu, na akasema kama hakuna mbwa asiyekuwa na mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, mbwa waliokuwa hawana wenyewe wapo. Sisi ndio tunaoishi vijijini na mbwa hawa tunawaona na chanzo chao kweli walikuwa na wenyewe, lakini pengine kutokana na wale wenyewe hawakuwatunza vizuri mbwa wale pengine mmoja au wawili waliondoka pale kwao wakahamia mwituni. Sasa wameshazaliana wameshakuwa makundi. Si mbwa tena wawili.

Sasa hili Mhe. Mwenyekiti, naiomba kamati itwambie ina maoni gani kuhusu mbwa hawa, kwa sababu pia wanaweza wakapata athari ya huu ugonjwa, hawana watu wa kuwapeleka kwenye chanjo, ni mbwa wa mwituni. Hapa serikali na wizara ikiwa haikuwa na lengo la kuwashughulikia mbwa hawa, basi ninakuhakikishia badala ya kuwa sasa hivi tuwe kwenye kinga, tutakuwa kwenye tiba wala iliyokuwa haipo na madhara makubwa yatatokea.

Mhe. Mwenyekiti, katika hapa hapa changamoto kuna ugonjwa wa ndui na mahepe. Mhe. Mwenyekiti, hapa kamati imeeleza upande ambao wameona kama wanaathiriwa zaidi na ugonjwa wa ndui, lakini napenda niseme kama ugonjwa huu hauwaathiri eneo moja tu, ugonjwa huu unawaathiri wafugaji wote, maeneo yote basi ugonjwa huu upo.

Na niliulizia swali hapa Barazani na jawabu nilipata zuri tu lakini ninamuomba Mhe. Waziri bado ajue kama ugonjwa huu ni tatizo. Kwa hivyo kamati pamoja na wizara ifanye utafiti na itwambie itawasaidia nini hapa wafugaji.

Pia Mhe. Mwenyekiti, naomba niipongeze Kamati kwa kusisitiza uagizaji wa chanjo zenye ubora na zinazokidhi viwango. Vile vile niipongeze wizara kwa utekelezaji wake. Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia wafugaji wakitumia chanjo wanazonunua katika maduka ya madawa, lakini Mhe. Mwenyekiti, ikifika msimu wa maradhi, aliyetumia chanjo, aliyekuwa hakutumia chanjo basi mifugo yake yote itamaliza. Hii ninaamini inatokana pengine chanjo hazina ubora au wafugaji hawana elimu, hawajui wazitumie vipi. Kwa hivyo hapa naomba kamati itoe ushauri mzuri kwa wizara ili waweze kuwasaidia wafugaji.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nije sekta ya habari. Mhe. Mwenyekiti, sekta hii ina matatizo makubwa na kwa kweli inahitaji mageuzi. Ukisikiliza taarifa ya habari ya redio na televisheni, habari zao zote zinatoka upande mmoja, hasa taarifa ya habari ya televisheni. Sijui ni kwa sababu gani Mhe. Mwenyekiti, televisheni ile ya *ZBC* utafikiria ni ya Unguja tu, wakati ni televisheni ya visiwa vyote viwili.

Mhe. Mwenyekiti, pia ninasikitika mpaka hii leo shughuli ikifanyika Pemba lazima kaseti yake itiwe kwenye ndege ipokelewe Unguja. Mhe. Mwenyekiti, hilo ni tatizo, ulimwengu huu sasa si wa kufanya mambo hayo. Wenzetu wakifanya tu lile jambo linatoka kwenye televisheni zao. Sisi leo tusubiri kaseti isafirishwe pengine jambo limefanyika leo, kaseti ifike kesho, usubiri kesho kutwa. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ni jambo la kushangaza. (*Makofi*). Lakini Mhe. Mwenyekiti, vile vile nimesikia kama kumeanzishwa redio jamii Tumbatu na redio ya jamii ya Micheweni tunaijua ipo na redio jamii Mtegani

Makunduchi. Kwa hivyo mikoa mitatu hii tayari imeshapata redio jamii. Je, Mhe.Mwenyekiti, naomba niulize na Mkoa wa Kusini Pemba itapatiwa lini redio jamii? Mhe. Mwenyekiti, hili ni suala muhimu. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni kuhusu king'amuzi. Mhe. Mwenyekiti, kule Pemba ukiwa na king'amuzi unaweza kuona vizuri, lakini naomba nimuulize Mhe. Waziri hapa kwa nini king'amuzi hichi cha serikali kiwe na *channels* 20 tu, wakati tunaona ving'amuzi vyengine vina *channels 40, 60, 100*. Hivyo kweli Mhe. Mwenyekiti, hii serikali kuwa king'amuzi chenye *channels* 20 haioni aibu au atueleze Mhe. Waziri kuna mwelekeo gani na kamati ina maoni gani juu ya hili?

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie uwanja wa Gombani Pemba. Una tatizo la njia ya kutumika kwa riadha. Hadi hii leo Mhe. Mwenyekiti, njia hii haijafanyiwa matengenezo, inaota majani basi hata ile lami imeshindwa kutiwa. Mhe. Mwenyekiti, naomba na katika hilo nisikie maoni ya Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nataka nije katika Shirika la *ZBC* kwenye changamoto. Nimekuta changamoto kama *ZBC* inakabiliwa wa kaseti na hufutwa baadhi ya kumbukumbu muhimu ili wazitumie tena. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli shirika hili limepoteza muelekeo. Kufuta kumbukumbu muhimu kwa ajili ya kutumika kaseti, hili ni jambo la kusitisha. Mhe. Mwenyekiti, ni juzi tu tumesheherekea sherehe za miaka 50, leo tunaambiwa Shirika la *ZBC* ambalo ni shirika la serikali mpaka lifute kumbukumbu za nyuma ndio wapate kaseti ya kurekodia mambo mapya. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, hii inasikitisha. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kuna methali inayosema *mti huliwa na tunda zake* na hii nimeshuhudia kweli kweli. Muembe ukizaa maembe, huliwa kwa kupopolewa maembe yake, na maembe yale kinachotumika ni lile tawi la muembe ndio linalokatwa ikawa gongo la kupopolea. Muembe ule ule ukitaka kuukata unatumia shoka, shoka mpaka iwe na mpini wa jiti na panga vile vile. Mhe. Mwenyekiti, leo hapa tumeshuhudia Shirika la Umeme wadaiwa sugu ni taasisi za serikali. ZAWA wadaiwa sugu ni taasisi za serikali, kumbe hata Bwawani wadaiwa sugu ni taasisi za serikali. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, vijana huwa wana msemo wao unaosema "*tushushe*!". Tunaiomba serikali itushushe tumechoka tupumzike.

Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia Ripoti hii ya Kamati ya Mifugo, Uvuvi, Utalii na Habari.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kuwapongeza sana Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wake kwa taarifa yao hii, halikadhalika niwashukuru sana Mawaziri na Naibu Mawaziri wa wizara zote mbili kwa majibu yao mazuri na utekelezaji wao mzuri wa maagizo ya kamati.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianzie na Wizara ya Uvuvi na Mifugo. Mhe. Mwenyekiti, jana wakati Waziri wa Fedha akizungumzia suala zima la kampuni mpya ya maziwa ambayo inajengwa kule Fumba. Na akawataka Wajumbe wa kamati pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwenda kukitembelea kiwanda kile ili kuweza kujionea wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuipongeza sana Kampuni hii ya Bakhressa kwa uzalendo wao kwa kuweza kujenga kiwanda kile kwa faida ya Wazanzibari na wananchi na serikali kwa jumla, kwa sababu kiwanda kile kitakapoanza biashara zake au kazi zake, basi faida nyingi zitapatikana kwa serikali pamoja na wananchi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeiomba hii wizara husika ya Mifugo na Uvuvi kuhakikisha kwamba inawawezesha wananchi kuweza kupata ng'ombe wale wa maziwa. Kwa sababu ninavyojua kwamba kampuni hii ya maziwa ya Bakhressa itakuwa inanunua maziwa kutoka kwa wananchi. Lakini ni vyema kwamba wananchi ambao wakaanza kuwezeshwa mapema ili kuweza kuwapata ng'ombe hao au mbuzi hao na kujiandaa itakapofunguliwa tu kampuni hii ya maziwa ili waweze kwenda kuuza maziwa yao na kuweza kujiendesha kimaisha yao.

Wananchi wengi wa Zanzibar ni wafugaji. Ukitazama Fumba kule kwa Mhe. Mwinyihaji Makame na yeye pia ni mfugaji, ukienda Pemba maeneo ya Shamiani, Kengeja ni wafugaji wakubwa wa ng'ombe, na ukienda Donge lakini sasa wale ng'ombe waliozoea kuwafuga ni wale ng'ombe wa zamani ambao hawana maziwa. Kwa hivyo ni vyema wizara ikaangalia kwa kina suala hili ili kuwawezesha wananchi kuweza kupata ng'ombe wale wa maziwa ili kuweza kujiendesha katika maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuunge sana mkono Profesa Makame Mshimba Mbarouk kwa suala lile ambalo alilolizungumzia kuwatetea hawa waandishi wa habari ambao tunao humu ndani. Mimi ningeomba sana wizara kusikia kilio hichi, kuhakikisha waandishi wa habari hawa waliopo ndani na waliopo nje ambao wananchi waliopo majumbani wanapata taarifa hizi, lakini hawa waandishi tupo nao hapa kwa kweli wanasikitika sana kuona wanakaa kuanzia asubuhi hadi usiku, lakini posho lao ni dogo sana. Kwa hivyo ningemuomba sana ili kuwawezesha waandishi hawa wa habari.

Mhe. Mwenyekiti, lilizungumzwa suala zima la ukumbi wa studio ya Rahaleo ambao upo katika Jimbo la Rahaleo. Kweli Mhe. Mwenyekiti, malalamiko mengi ya wananchi wa Jimbo la Rahaleo wamekuwa wakilalamika kuhusiana na *studio* ile ambayo lengo lake na madhumuni yake sivyo linavyotumika kama lilivyokusudiwa na Mhe. Rais Dr. Ali Mohamed Shein. Wakati anazindua jengo lile alieleze lengo na madhumuni ya *studio* ile, lakini inavyotumika *studio* ile ni tofauti na wananchi wa Jimbo la Rahaleo wamekuwa wakilalamika sana, kwa sababu pale ikifika usiku watu wanataka kusali pale Msikitini, makelele mengi ya magoma, kama alivyozungumza *birthday* pale na kadhalika. Kwa kweli si jambo zuri. Kwa hivyo tuendane na dhamira halisi ya lengo la studio ile ili wafaidike na yale ambayo yaliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kituo cha michezo cha Dole. Mhe. Mwenyekiti, ulimwenguni kwa ujumla hivi sasa michezo inaendeshwa kupitia vituo vya michezo. Na tumebahatika Zanzibar kupata mfadhili ambaye amejitolea kudhamini ujenzi wa kituo kile cha Dole. Lakini imeelezwa taarifa hii kutokana na mapungufu na kasoro ambazo zimekifanya kituo kile kishindwe kumalizia kwa wakati.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, Waswahili wanasema *abebwaye hujikaza*, ujikaze ni neno baya, ukijikaza vipi, mimi ninasema ukibebwa ujikaze haya. Mhe. Asha hapa anasema ukibebwa na wewe ujikaze. (*Kicheko*).

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mfadhili yule muhisani amejitolea kutusaidia. Sasa na sisi tunataka kujikaze kama alivyosema Mhe. Asha hapa mama yangu. Kwa hivyo ningeiomba sana wizara kuhakikishia kwamba wanasaidia mradi ule ni mzuri. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, mifano ipo katika nchi za Afrika kama vile Ghana, Nigeria, Cameroon zimefaidika na vituo hivi vya michezo.

Juzi tu nilikuwa ninaangalia mchezo wa mpira wa miguu kati ya timu ya Ghana na Nigeria ambapo mtangazaji anasema kwamba wachezaji wengi ambapo ni asilimia 80 wanaochezea timu ya Ghana ni wachezaji ambao wametoka katika vituo vya michezo.

Kwa hivyo kituo hiki ni muhimu na si Dole tu, ipo haja ya kuangalia kwamba Pemba kiwepo kituo cha michezo kwa sababu ndio mkombozi wa soka letu la Zanzibar. Zamani Zanzibar ni nchi ya kwanza ambayo katika ukanda huu wa Afrika katika kuandaa vijana, lakini wakati ule hata vipimo vyake vilikuwa vinatumika gongo, wakati wa Mzee Marehemu Hija Saleh.

Lakini leo tunaendelea wakati wa sayansi na teknolojia na hata wachezaji wanaocheza ulaya wanapitia kwenye vituo hivi. Kwa hivyo ipo haja

kuhakikisha kwamba tunakiendeleza kituo kile, serikali inatia nguvu zake na vile vile kuweza kufungua vituo vyengine vya michezo hivi kama Pemba, Kaskazini. Kwa sababu kituo hichi kipo Kusini, ni vizuri kuhakikisha kwamba vituo hivi vinaenezwa katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Shirika la Utangazaji. Mhe. Mwenyekiti, shirika hili Mhe. Rais alianzisha kwa dhamira na lengo zuri sana, lakini bado hakujakuwa na lile lengo la kufikia kuona kwamba kweli hasa shirika hili linaweza kujiendesha kishirika.

Ukiangalia mashirika mengine kama vile Shirika la wenzetu la *TBC*. Ukija katika Shirika letu la *ZBC*, kwa kweli ni mbali sana. Leo waandishi wa habari wanalalamika huko mitaani. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia mshahara wa mtangazaji wa *ZBC* na ukija ukiangalia mshahara wa mtangazaji wa *TBC*, unaweza kuona huruma. Kwa kweli ningemuomba sana Mhe. Waziri na serikali kwa jumla kuhakikisha kwamba linaliwezesha shirika hili ili liweze kujiendesha na wafanyakazi waweze kufaidika na dhamira nzima ya kuanzishwa shirika hili. Posho wanazolipwa wafanyakazi na waandishi wa habari kwa kweli halitoshelezi.

Kwa sababu waandishi wa habari ulimwengu mzima ndio ambao wanatupa taarifa zetu wananchi. Leo tupo hapa katika Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti, wananchi wapo katika televisheni kuangalia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao wamewachagua wao kupata taarifa mbali mbali. Kwa hivyo ni jambo muhimu sana lakini hawa waandishi wa habari hatuwawezeshi, shirika hili bado halijawezeshwa. Kwa hivyo ningemuomba sana Mhe. Waziri kuhakikisha kwamba shirika hili linatiliwa nguvu kuhakikisha kwamba linaendeshwa kibiashara na linaweza kujitegemea kama ambavyo lilivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli suala zima hili ambalo tunazungumza na ambalo limo katika taarifa hii, ninamshukuru sana Mhe. Waziri ameeleza kwamba katika maagizo ambayo amepewa na kamati kufanyia matengenezo uwanja wa Gombani kule Pemba. Ninawapongeza sana wizara kwa kuweza kuutengeneza uwanja ule, kupiga rangi na kufanya ukarabati mwengine.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ukija katika uwanja wa Amaan ambapo pesa nyingi zimetumika. Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hichi cha takriban miaka mitatu minne, uwanja ule umeshafanyiwa ukarabati mara mbili. Kipindi cha kwanza kiliweza kutumiwa takriban shilingi bilioni moja kwa sababu zilitumika pesa dola laki nane.

Baada ya hata miaka mitano haijafika, tayari tumeweza kuufanyia ukarabati uwanja ule. Kwa hivyo kwamba pesa zile za walipa kodi zimetumika kutia nyasi bandia. Ipo haja kuhakikisha kwamba utunzaji wa uwanja ule. Mimi ndio juzi nikasema kwamba ili kuviendeleza viwanja vyetu hivi, ndio nikapendekeza kwamba *ZFA* waweze kupewa viwanja hivi, kwa nini nikasema hivi kwa sababu wao wana uchungu, kwa sababu wao ndio wanaovitumia viwanja vile.

Ingawa majibu ya Mhe. Waziri alieleza kujibu pale lakini ningeomba kwamba basi angalau kuundwa kamati maalum ya kusimamia viwanja vyetu ambavyo tumetumia pesa nyingi, na lengo na madhumuni kuwajengea wananchi wetu na wanamichezo wetu na kuendeleza michezo yetu hapa Zanzibar. Yamezungumzwa mengi, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kazungumza pale malalamiko mengi ambayo kwamba serikali au wizara au Baraza la Michezo linakuwa linalenga katika masuala mazima ya *football* na kuacha michezo mengine yaani riadha.

Lakini ningemuomba Mhe. Waziri kuhakikisha kwamba kupitia wizara yake na Baraza lake la Michezo kwamba linaangalia na michezo mengine ili kuhakikisha kwamba michezo yetu ya Zanzibar, mpira wa miguu, *netball*, riadha na michezo mengine na hata huo mchezo wa nage ambao Mhe. Prof. Mshimba aliutaja kuhakikisha kwamba tunaendeleza michezo hiyo.

Kwa sababu michezo ni afya, michezo inaleta udugu, michezo inaleta umoja na mshikamano na michezo inawaunganisha wananchi wa kila aina. Hata sisi timu yako Baraza lako Tukufu Mhe. Mwenyekiti, tuna timu yetu ya Baraza yetu ya Baraza la Wawakilishi ambapo huwa tunacheza michezo mbali mbali na nchi mbali mbali. Juzi tu hapa tulikuwa na wageni kutoka Bunge la Uganda. Kwa hivyo ile ni kuonesha kwamba michezo inaleta umoja na mshikamano. Lakini tusipoangalia kuviendeleza viwanja vyetu hivi vya michezo Mhe. Mwenyekiti, tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu.

Kwa hivyo ninamuomba sana Mhe. Waziri kuhakikisha kwamba Uwanja wa Amaan unasimamiwa vyema ili kulinda na ...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umebakiza dakika 5.

Mhe. Nassor Salim Ali: Na kuleta ile dhamira halisi ya kutumia viwanja vyetu hivi vya michezo.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana lakini nitoe pongezi kubwa sana kwa wizara pamoja na Baraza la Michezo na *ZFA* kwa jumla, katika kusimamia vyema mashindano ya miaka 50 ya *Mapinduzi Cup*,

mbali na kasoro ambazo zimejitokeza kwa sababu hakuna mahali penye zuri kusikokuwa na baya, lazima kasoro zitajitokeza.

Lakini kwa kweli wananchi wamefurahika kwa sababu nchi mbali mbali zimealikwa na timu kubwa kubwa zimeshiriki kwenye mashindano yale. Ningeiomba wizara kwa sababu malalamiko Mhe. Mwenyekiti, ambayo yaliyokuwa yakilalamikiwa na *ZFA* kuhusiana na uendeshaji wa mashindano haya ya *Mapinduzi Cup.*

Mimi nikiwa ni Mjumbe wa Kamati ya Mashindano haya ya *Mapinduzi Cup* ambayo iliundwa miaka mitatu iliyopita, baada ya *ZFA* kuona mzigo ni mkubwa. Lakini kwamba *ZFA* sasa wanayataka mashindano waendeshe wenyewe, mimi naona hakuna pingamizi kuona kwamba wasiachiwe wenyewe ikiwa wao wataendesha wenyewe, wataunda kamati yao wenyewe, wapo wana michezo akina Mhe. Hamza Hassan Juma, watakwenda watasaidia kuendesha mashindano yale, sio Mhe. Nassor Salim Ali tu, wapo na wengine.

Kwa hivyo mimi ninadhani ipo haja ya kuhakikisha kwamba mashindano yale wanaachiwa wenyewe *ZFA* wayaendeshe, kwa sababu tusipate visingizio kwamba leo *CAF*, *CAF* ninakusudia *CAF* ni chama cha mpira wa miguu Afrika, *CECAFA*. Ingawa sisi bado hatujawa wanachama wa *FIFA* lakini hivyo vyama tusiwe na visingizio waachiwe wenyewe waendeshe hayo mashindano. Na nimuombe Mhe.Waziri kwa neno la mwisho kuhakikisha kwamba kulikuwa na taarifa kuwa Mhe. Mshimba kazungumza shilingi milioni mia moja na hamsini ambazo serikali ilitoa, atupe maelezo ya kina ili wananchi na viongozi wengine waelewe, kwa sababu kuna taarifa serikali imetoa milioni mia moja na hamsini katika kuendesha mashindano yale.

Sijui ukweli upo wapi, na ni vyema kwa sababu haya maneno yamekuwa makubwa. Wizara yake imekuwa katika midomo, kamati itakuwa katika midomo, ni vyema kwamba waziri atakapokuja aeleze kwa kina suala hili la milioni mia moja na hamsini.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ninakutakia kila la kheri na wewe Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii na mimi ninaunga mkono taarifa hii ya Kamati.

Ahsante sana Mhe.Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kukutana katika Baraza lako tukufu katika hali ya afya njema kwa

madhumuni ya kutengeneza mambo mbali mbali ya Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hali yangu leo si nzuri, kwa hivyo nitazungumza machache. Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya Mifungo, Utalii, Uwezeshaji na Habari na niseme tu kwamba kwa kweli niwashukuru wale wote ambao wameanza kuchangia kwa hapa na pale, kwa mintarafu ya kuisaidia kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazungumzia kuhusu habari ya Redio Jamii FM ya Mtegani. Mhe. Mwenyekiti, mtu yeyote anayefanya vizuri basi lazima umpe haki yake ya kumsifu au ya kumpongeza. Kwanza mimi nichukuwe nafasi hii niwapongeze sana Redio Jamii FM ya Mtegani ambayo ni redio pekee iliyoshughulikiwa na watoto wadogo sana katika umri wa miaka 14, ni historia.

Mhe. Mwenyekiti, watoto hawa wawili mtu na ndugu yake baba mmoja na mama mmoja ambao ni Ramadhan Bilal Jihad pamoja na Ameir Bilal Jihad. Kwa kweli ni mfano tosha kwamba vijana wetu wana vipaji ambavyo vinaweza vikasaidia kwa wakati huu wa sayansi na teknolojia. Mimi niiombe serikali kabla ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais hajatoka, kwa kupitia kwa Makamu wa Pili wa Rais, vijana hawa ni wajibu wetu kuwachukua na kuhakikisha tunawaendeleza na sio kuwaendeleza hapa, tuwapeleke mahala ambapo watasaidiwa hawa vijana, ili watakaporudi waweze kusaidia serikali yao. Kwa sababu hawa watoto sio wa leo, toka hiki kituo kianze Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, niiombe wizara husika basi angalau iwasaidie hawa vijana kwa hivi sasa mpaka serikali itakapopata uwezo wa kwenda kuwasomesha vijana hawa. Ni watoto wadogo lakini mambo waliyoyafanya ni makubwa. Baba yao hawa watoto ni mtu anayeshughulika na mambo ya uchongaji, lakini vijana hawa wamekaa wakabuni, mmoja amebuni kuhusu habari ya redio na kamati imeeleza na mmoja amebuni mpaka sasa hivi kuwa na angalau mambo ya TV.

Kwa hivyo, naiomba serikali vijana kama hawa wasiwaache tu, baba yao uwezo hana. Kwa hivyo, niiombe serikali kuu tena wakati wa bajeti hapa patakuwa pagumu, ni lazima vijana hawa twende wizara husika na serikali kuu, ili wakaangaliwe vijana hawa na wafanyiwe uchunguzi na wajulikane ni kitu gani na gani ambacho wanaweza kusaidiwa vijana wetu hawa. Kama ni kupelekwa kwenda kujiendeleza katika mambo haya. Jambo hili nilisema niliseme wazi Mhe. Spika, kwa kweli mcheza kwao hutunzwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mfanyakazi wa wizara hii hii ambae anaitwa Saumu Ali Haji, huyu Saumu ni mwanamme, maana yake jina la Saumu linakwenda kukeni na kuumeni, ni mwanamme huyu Saumu. Naiomba wizara kijana huyu kwa sababu ndie chanzo cha kuwatafuta watoto hawa na kuwaendeleza, na kufikia hadi kuwafanyia mambo yote ambayo hivi sasa redio jamii hii inafanya mambo yake kwa uaminifu na uadilifu. Kwa hivyo, naiomba wizara na huyu Saumu naye imwite imuhoji na imuangalie kwa jicho la huruma, ili na yeye apate angalau kujiendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije katika mambo haya ya mifugo na uvuvi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaenda huko nimalizie kwenye hii redio jamii. Mhe. Mwenyekiti, nilimsikia Mhe. Mwakilishi mmoja hapa akisema na wao wanataka redio jamii. Redio hii ndio ikaitwa redio jamii kwa sababu ni wananchi wenyewe wajishajihishe. Humo mote walijishajihisha wananchi wenyewe ndio wakaweka redio jamii. Kwa hivyo, awaulize wenziwe hao waliopata mpaka kukawa na redio jamii, awaulize wamefanya vipi ili na yeye ajiunge pamoja na wa Mkoani Pemba nao wapate redio jamii.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nije katika mambo ya mifugo na uvuvi. Kwanza niipongeze sana wizara hii, pamoja na ukwasi wa kupatiwa pesa za kufanyia kazi. Kwa sababu hivi tunavyokwenda, mwisho miezi mitatu hawajatiliwa hata senti, wako katika hali ngumu sana ya kifedha. Kwa hivyo, niiombe wizara husika kwamba keshokutwa ni bajeti, niiombe wizara husika angalau katika yale malengo waliyojipangia basi wapatiwe hizi fedha, ili waweze kukamilisha yale malengo ambayo wamejipangia.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba Kamati hii ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari inajipangia sehemu mbali mbali za kutembelea. Tulikwenda Nungwi katika taasisi ya kijamii. Tukawakusanya wavuvi wote wa eneo lile la Mkoa wa Kaskazini. Nasema mkoa, sio wilaya, ni Mkoa wa Kaskazini. Wakaeleza matatizo yao tukawasikiliza na wenyewe Wizara walikuwepo na mengine kwa kweli yanahusiana na mambo ya utalii.

Kwa hivyo, mimi naomba Wizara husika Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na Wizara Mifugo na Uvuvi, wanapowekeza wenzetu hawa basi hizi Wizara zishirikiane Mhe. Mwenyekiti, ili kuhakikisha wananchi wetu hawapati shida katika shughuli zao wa uvuvi. Ni kweli aliyozungumza Mhe. Omar hapa kwamba ni kweli watu wa uvuvi wanapata shida kwenye madiko yao, wakati wanapotoka au wanapokwenda kwenye shughuli zao.

Mimi nadhani kuna haja Mhe. Mwenyekiti, ya kushirikiana pamoja ili kama kuna njia inaziba kwenye hoteli ile, basi mwekezaji ahakikishe anashirikiana

na Wizara husika, ili watu hawa watafutiwe njia nyengine mbadala ya kupita.Wavuvi hawa wasisumbuke na wao wawekezaji wasisumbuliwe na wananchi. Kwa sababu na wananchi na wao wana haki. Nilisema suala hili na mimi nilizungumze.

Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli taasisi ya kijamii ya uvuvi tulitembelea, lakini madamu Mhe. Omar kazungumza hapa, basi safari inayokuja tutakwenda kwenye taasisi ya Mhe. Omar ili na wao tuwasikilize matatizo yao. Mimi nasema uvuvi haramu unajulikana na uvuvi halali unajulikana, kwa sababu ni sisi tuliopitisha sheria hapa katika Baraza lako tukufu. Kwa hivyo, kama tumepitisha sheria Mhe. Mwenyekiti, ni lazima sheria zile tuzisimamie kwa uaminifu na uadilifu.

Sio vyema sisi tunaopitisha sheria tukasema kwamba hatujui uvuvi haramu wala uvuvi halali. Kwa sababu tulipata semina mbali mbali na tukaletewa na vifaa vyote tukaoneshwa hiki haramu na hiki halali. Hiki hakifai na hiki kinafaa.

Semina hizo sio sisi tu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, hata hao wanaohusika katika vijiji vyetu wanapewa semina mbali mbali Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, ni wajibu wetu sisi, kuhakikisha kwamba tunawapa taaluma watu wetu ambao tunahisi wanayoyafanya sio mema, wafanye yale mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikimalizia na mimi nitakuwa mwizi wa fadhila. Mhe. Mwenyekiti, katika bajeti mbili zilizopita, nadhani tuliwazungumzia vijana wetu hawa wanaokaa na sisi humu ndani, wachukua picha wanaume na wanawake. Tulizungumza kwamba tufanye utaratibu, sisi tunakaa kwenye viti wao wanasimama, haidhuru ni kazi yao, lakini wao wanasimama saa zote na kusimama kwao wakiondoka hapa sisi tunamaliza, lakini wao wanaendelea na kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba sana Waziri anayehusika, au tukubaliane tuombe fedha maalum, hawa vijana wawe ni katika taasisi ya Baraza la Wawakilishi. Tulizungumza hilo kwenye bajeti. Sasa sijui Mhe. Waziri atakuja kuniambia nini, walikubaliana na hii taasisi yetu au hawakukubaliana ili na hawa vijana na wao tuwaonee huruma.

Sisi tukiondoka hapa tunakwenda kwetu miguu juu tunalala, lakini hawa vijana bado wanaendelea na kazi ili kuhakikisha mambo yao wanayaweka kwenye utaratibu na yanashughulikiwa ipasavyo, ili taarifa ziweze kutoka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilisema nizungumze hayo ili twende sambamba na mambo ambayo tunayokubaliana katika Baraza lako hili tukufu. Sasa ninamuomba Mhe. Waziri katika yale maagizo ambayo tumeyatoa anieleze yamefikia wapi kwa vijana wetu hawa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mwisho niseme kwamba naiomba sana Wizara ya Fedha, tunapitisha bajeti sisi hapa na juzi nililizungumza suala hili kwa mintarafu ya kwamba kila Wizara husika iweze kugaiwa mgao wake wa bango kitita. Lakini inaonekana bango kitita halifanyi kazi. Kwa sababu katika wizara mbili hizi tulizokwenda, lakini hasa hii Wizara ya Mifugo na Uvuvi, walituambia kwamba mpaka hivi sasa mnapokuja nyinyi miezi mitatu hatujapata chochote.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo niliyoyazungumza na mimi moja kwa moja niunge mkono ripoti hii ya kamati, kwa jinsi ilivyowasilishwa vizuri. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nasema ahsante sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, asubuhi hii ya leo na mimi kupata fursa ya kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kufanikisha kutiwa nyasi Kiwanja cha Amani na katika sherehe zile za Mapinduzi kikawa ni kivutio kizuri kwa nchi yetu, hasa katika michezo ile ya Kombe la Mapinduzi CUP. Basi wenzetu wale waliokuja kutoka nchi nyengine, waliona kumbe na Zanzibar kuna kiwanja cha michezo ambacho ni kizuri. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na pongezi zangu zote ninazompongeza Waziri. Waswahili wanasema "kila kizuri hakikosi kuwa na kasoro". Kwa hivyo, pamoja na mazuri hayo, sasa napenda nimlaumu Mhe. Waziri au nimkosowe kwa mambo mengine ambayo yanafuata.

Mhe. Mwenyekiti, utakumbuka kwamba Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi awamu kwa awamu tunakuja kufanyakazi za maendeleo ya nchi yetu, kuwafikishia wananchi maendeleo na kuikosoa serikali, kuielekeza na kuilaumu ili tupate utendaji mzuri katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda niikosowe Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa hawa wafanyakazi wetu waliomo katika Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, hawa waandishi waliomo humu ndani ya Baraza la Wawakilishi wana kazi kubwa tena nzito. Wana kazi ya kusimama kutwa kucha, tangu kipindi tunachokuwemo humu ndani wao wanasimama, wanafanyakazi hii ya habari ili kuwafikishia ujumbe wananchi juu ya yale

tunayoyafanya katika Baraza hili. Lakini cha kusikitisha mno ni kwamba sijui niseme ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kila siku tunapigia kelele masuala haya, hawatusikii au sijui kwa nini wanashindwa kutekeleza.

Hivi Mhe. Mwenyekiti, waandishi hawa wanalipwa shilingi 5,000 kwa siku. Lakini hiyo shilingi 5,000 wanayolipwa kwa siku, kwa nini hawapewi wenyewe Mhe. Mwenyekiti. Ni kipindi cha mwaka wa pili huu hawajalipwa pesa zao. Hivi shilingi 5,000 wizara inawashinda. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri awazingatie sana hawa vijana kazi yao ni ngumu sana.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ni kwamba katika kipindi kilichopita uliongezwa mshahara kwa asilimia 25, lakini kwa nini hawa wafanyakazi wetu hata hiyo nayo. Namuomba Mhe. Waziri awaone sana hawa vijana.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri kwamba tunategemea kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu hivi karibuni, kuna mchakato wa katiba na tutakwenda kwenye Bunge la Katiba. Sina uhakika lakini nasikia kwamba hawa wafanyakazi wetu wa habari waandishi wetu hawamo katika orodha ya kwenda kule kufanya kazi hii.

Naomba sana kwa faida ya serikali yetu pamoja na sisi wenyewe, basi wafanyiwe namna na wao wawepo kule Dodoma. Kwa sababu tutakuja kutaka kumbukumbu, na tutakapotaka itabidi twende tukaombe kwa wenzetu kule.

Lakini ikiwa tunawafanyakazi wetu basi kumbukumbu itakuwa ni rahisi kuzipata. Kwa hivyo, kama hilo halipo basi naomba wafikiriwe. Hata kama ni kulipwa na serikali yetu, lakini wawepo. Hilo likitokea basi wachukuliwe wale ambao wanapata kazi ngumu, tunaodumu nao, sio wachukuliwe wengine. Maana inawezekana ombi hili likakubaliwa, lakini Mkurugenzi wa Habari akachukua watu wengine nje na wale ambao wanakuja hapa wakifanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni suala ambalo lilizungumzwa nyuma kwenye bajeti zilizopita kwamba Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo itakuza utamaduni wa nchi yetu. Lakini walisema kwamba watapita vijijini, jimbo kwa jimbo, ili kuendeleza utamaduni wa nchi yetu. Sasa naona kimya hili suala, sijui lilifikia wapi na muda ndio unakwenda. Sasa namkumbusha Mhe. Waziri kwamba suala hili alilizungumza, kwa hivyo tuone utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kupongeza kile kituo chetu cha Redio Jamii kiliopo Micheweni. Kwa jinsi kinavyofanya kazi vizuri na ombi la kamati ni kwamba papandwe miti, kwa hivyo tutaendelea kuwahimiza vijana wetu ili kupandwe miti katika kipindi kile cha mvua za masika. Kwa sababu kama sio mvua za masika kwa kule kwetu miti haioti. Ikitaka kupandwa hiyo miti basi itegewe katika kipindi cha masika ndio inaweza kuoteshwa miti na ikakubali.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, nina masikitiko kidogo kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa sababu kila upande kuna matatizo na kuna vikwazo kwa wananchi wetu. Sijui hawa wananchi wetu waende wakajiweke wapi mpaka wasipate tabu.

Kila siku sisi ni mashahidi tunashuhudia kwamba mara watu wanafukuzwa na manispaa. Sasa na hawa wavuvi nao kila mara inakuwa ni vikwazo. Hivi hawa wananchi wetu wakimbilie wapi? Sisi ni mashahidi kwamba jana wavuvi wamevunjiwa mabanda yao kwa sababu tu wanataka kupewa matajiri wenye uwezo.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu uliopo ni kwamba unapomuhamisha mtu hapa basi unamuweka pengine, lakini leo bila ya kuwaelekeza kwamba tunawatoa hapa tutakwenda kuwaweka hapa mnakwenda kuwavunjia tu! Kwa kweli wavuvi wanadharauliwa mara nyingi sana. Hivi ni lini hasa serikali itaona kwamba hawa wavuvi nao ni wazalishaji na ni waendelezaji wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, wavuvi wanakuwa kama watoto mayatima hawana pakukimbilia sasa hivi. Serikali ilisema kwamba wavuvi wavuwe uvuvi wa kileo, waache uvuvi haramu, unapomuwezesha mtu anaweza kufanya ile kazi inayotakiwa, lakini kwa nini serikali inashindwa kuwawezesha wavuvi wetu ili wakavua uvuvi wa kileo. Kila siku serikali inasema tutafanya tu, lakini bado haifanyi.

Kila siku tunapiga kelele kama nchi yetu inaweza ikazalisha mali zaidi na ikaongeza kipato. Ikiwa sasa hivi tunategemea karafuu na utalii, na uvuvi unaweza ukaongeza kipato cha nchi yetu. Lakini mpaka leo hayo maandalizi ya uvuvi hatujaona dalili ya kuwa yatakuwa mazuri.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, kama ana mbio basi aongeze hizo mbio, lakini ilimradi tuone kwamba uzalishaji wa baharini iwe hiyo bahari kuu na sisi tunaitumia. Leo tunawaachia tu wageni wanakuja kuitumia. Kila siku unasikia zimekuja meli hapa kuiba, tunaibiwa sisi wenyewe tumekaa hivi hivi, hatuna la kufanya.

Mhe. Mwenyekiti, narudi tena kwa wavuvi, ni lazima wafikiriwe na wahudumiwe na waonewe huruma.Naomba wapatiwe vifaa vya kuokolea. Juzi kilikuwa kinatoka chombo safari, kikazama pale, mpaka jana wamekwenda kuokolewa na wavuvi wa Nungwi. Sasa serikali inaonaje kama ingewawekea japo wavuvi kule maboti maalum. Kwa sababu Nungwi kwa wakati wote wamekuwa ni askari wa mbele kuwaokoa watu wanapofikwa na ajali baharini. Mfano, ikiwa wanatoka Pemba kuja Unguja au kutoka Unguja kwenda Pemba.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, umebakiza dakika tatu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Bila ya kuwategemea KMKM, kwa sababu KMKM wana kazi nyingi wanazozifanya. Kwa mfano kama hiyo jana walipewa ripoti KMKM, lakini waliokwenda kuokoa ni wavuvi wa Nungwi.

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu ni nzuri sana na kama tutajipanga vizuri, basi tunaweza kupiga hatua kwa kipindi kifupi sana. Lakini tatizo letu sisi tuna azimia tu kufanya lakini hatufanyi wala hatutekelezi. Mhe. Mwenyekiti, mipango yetu tunapanga tu kwenye kitabu na kwenye mabuku kwamba tutafanya kitu fulani, lakini utekelezaji wake unakuwa ni mgumu sana.

Mhe. Mwenyekiti naona unaniangalia, kwa kuheshimu kiti chako na muda wako nisije nikauchukua. Noamba niunge mkono hii ripoti ya kamati kwa asilimia 100, lakini na mawaziri naomba watekeleze ahadi zao, ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi).*

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia Kamati hii ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Wiraza hii ni muhimu sana katika nchi yetu kwa kutuwezesha kupata habari. Wizara hii hivi sasa kwa hapa kwetu *ZBC* ni redio ambayo tunaitegemea, lakini iko chini sana kutokana na habari zake. Kwa wakati mwingi redio hii hukatisha matangazo bila ya sababu maalum.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri aisaidie kwa kila hali ili iweze kupata vifaa vya kisasa ambavyo vinatumiliwa na nchi zote duniani. Redio hii unapokwenda kuitembelea vifa vyake vingi ni chakavu, kwa kweli inatia aibu sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi kile cha sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi, wakati tulipoitembelea basi tulikuta vifaa vyake vingi vinategemea kupitia kwenye *cable* ndio iweze kurusha matangazo vizuri. Namshauri Mhe. Waziri

ahakikishe kwamba redio yetu inapata vifaa vya kisasa, ili kuweza kutoa mfano kwa redio hizi ndogo ndogo, ambazo zimeanzishwa karibuni. Isiwe hii redio kongwe ambayo tunaitegemea tangu zamani, iwe ndio inazitegemea hizi redio ndogo ndogo.

Mhe. Mwenyekiki, kuna chombo ambacho sio kikubwa kiasi hicho, ambacho kinarusha matangazo kutoka sehemu moja na nyengine ambacho kinaitwa *link.* Unaweza kufika katika kituo cha redio ukaambiwa tatizo letu hapa haturushi vizuri kutokana na *link* yetu ni mbaya ama haifanyi kazi. Kwa kweli masuala madogo madogo kama haya, namuomba Mhe. Waziri aweze kuhakikisha kwamba yanatafutiwa ufumbuzi katika redio zetu.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika masuala ya utalii. Hivi sasa utalii upo nchini na unaendelea vizuri, lakini utakuta kwamba hii Wizara yenyewe haizalishi inavyotakiwa, hasa kama tulivyotegemea nchi yetu, na hivi sasa ndio tunaweza kusema kwamba ndio uti wa mgongo wa nchi yetu. Lakini utakuta utalii hivi sasa wawekezaji hao ndio wanaopata fedha zaidi, lakini sisi nchi yetu kwa kweli haifaidiki sana na utalii. Mara nyingi wanalipa huko huko wanakotoka, sisi hapa wanatulipa pesa za kienyeji, wakati sisi tuna haja ya pesa za kigeni kwani ndizo zitakazoweza kusaidia nchi yetu. Ninamshauri Mhe. Waziri kwamba watalii wanapokuja mambo yao yote waje kulipia huku ili tupate hizi pesa za kigeni.

Mhe. Mwenyekiti utalii huu tulianzisha kwa ajili ya faida ya nchi yetu, hasa kuhakikisha kwamba nchi yetu tunawekeza na tunapata ajira kwa wananchi wetu. Lakini utakuta sasa wananchi wanafanya kazi kupeleka bidhaa katika mahoteli, lakini mahoteli mengi hivi sasa wanakatisha kuwalipa wananchi, hadi wananchi wanafika kufilisika biashara zao. Na utakuta wao wenyewe mara nyengine, badala ya mambo yale yote kufanywa na wazawa, kazi hizo wanahakikisha wanafanya wenyewe.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti nije katika bahari kuu kuhusu uvuvi wa kisasa. Kwa muda mrefu sana tunafuatilia tuweze kuhakisha tuna boti zetu za kisasa, ambazo zinawezekana zikatuzalishia fedha nyingi kwa kuvua samaki, tunaoweza kusafirisha nchi za wenzetu. Lakini utakuta hadi leo kila bajeti tunapopitisha tuko pale pale. Tunavua uvuvi huu huu wa haramu. Ningeliomuomba Mhe. Waziri, atakapokuja aniambie ni lini uvuvi huu utaanza kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, pia ingelikuwa ni vizuri kama tungelikuwa na viwanda vyetu. Mtu ahakikishe kwamba unakwenda sokoni unanunua samaki wetu wa kizanzibari ambao wanasindikwa hapa hapa. Kwa kweli tungelikuwa

tumepata faida kubwa kwa nchi yetu. Kwa hivyo ninamshauri Mhe. Waziri hili alipe kipau mbele.

Mhe. Mwenyekiti kuhusu masuala ya michezo. Kwa kweli hivi sasa nchi yetu tunaendelea na michezo lakini kila siku hapa Barani Afrika sisi ndio tunakuwa wa mwisho, kwamba sisi timu zetu haziendelei katika madaraja yanayotakiwa. Hii inatokana na ukweli kwamba timu zetu hatuzishughulikii ipasavyo.

Ushauri wangu Mhe. Mwenyekiti, afadhali tuwe na timu zetu mbili za kiserikali ambazo zinatunzwa vizuri, kuhakikisha kwamba hizo ndizo zitakuwa timu za taifa. Tunapokwenda kwenye mashindano hatukamatii tuu. Utakuta pale katika zoezi, kabla ya wiki moja watu wanatakiwa kwenda kucheza nchi za nje, ndio tunaanza kutafuta wachezaji. Mimi namuomba Mhe. Waziri, hilo alipe kipau mbele.

Zaidi ya hayo yote Mhe. Mwenyekiti mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Koani, tunaunga mkono hoja, asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipatia fursa hii. Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa hai na kuweza kuingia katika jumba hili tukiwa wazima. Aidha, nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikutumia fursa hii kukushukuru pamoja na kukupongeza wewe, sio tu kwa kunipatia fursa ya kuchangia hii hoja iliyopo mbele yetu, lakini kwa umakini na umahiri wako ulionao Mhe. Mwenyekiti katika kusimamia suala zima hili la Baraza. Kwa hivyo, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wapiga kura wa jimbo langu la Wawi, tunakwambia ahsante sana kwa kazi nzuri unayoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye hoja, nianze na hili Shirika la Utangazaji ZBC. Mhe. Mwenyekiti ZBC ni mdomo wa nchi, vile vile ni jicho la nchi nzima. Ni kiunganishi baina ya serikali na wananchi wake, vile vile baina ya jamii na jamii. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti nimeamua nianze na dibaji hiyo kwa kumtaka Waziri wetu anayesimamia chombo hiki, kuwa makini sana katika kukisimamia.

Mhe. Mwenyekiti umakini mkubwa sana unahitajika kwa sababu hiki chombo ndio *connecting link* ya nchi nzima. Kwa hivyo ukiyumba kidogo katika kusimamia hiki chombo, basi unaweza ukawakosesha raha wananchi, serikali, na jamii kwa ujumla kuishi katika nchi yao. Kwa hivyo waziri wetu anatakiwa awe makini kukisimamia. Na sio tu kukisimamia chombo hiki Mheshimiwa katika kupanga safu ya uongozi katika wizara yake, *la hasha*! Sio hilo tu,

lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, kuangalia maslahi ya wafanyakazi wa chombo hiki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa huzuni kubwa mimi na wapiga kura wangu wa Jimbo la Wawi, tunasikitishwa sana na kuona jinsi ya maslahi ya wafanyakazi wa ZBC yalivyo duni, yasivyotunzwa. Ninasikitishwa sana Mheshimiwa kwamba kuna watu wameshakitumikia chombo hiki kwa muda mrefu, lakini kwa mujibu wa taarifa nilizonazo mpaka sasa hivi hawajajaza mkataba wa ajira. Hili Mheshimiwa ni tatizo lakini isitoshe kwa taarifa tulizonazo, kuna watu wamekitumikia chombo hiki kwa kipindi kirefu lakini hawajaajiriwa.

Tunamuomba Mhe. Waziri, alifanyie utafiti wa kina suala hili, na kama suala hili amelibaini ni kweli basi ahakikishe anawajazisha mkataba watu hawa na kuwalipa mishahara yao sio kuanzia hapo alipowajazisha mkataba tu, lakini tangu mtu huyo alipoanza kulitumikia shirika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, hili Baraza letu ni miongoni mwa mabunge ya Jumuiya za Madola, humu ndani huwezi kuingia tu hivi hivi, humu ndani lazima u-*look smart* ndio uingie katika jengo. Kinyume na hivyo unapigwa kanuni unatoka nje, ukiwa umevaa shati la kienyeji barabarani lazima u-*look smart* kama nilivyo hivi sasa mimi, ndio unaweza kuingia katika jengo hili. Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha kwamba vijana wetu wapiga picha wa ZBC sio kwamba hawezeshwi ku-*look smart* wakaingia humu, lakini hata posho lao hawalipwi.

Mheshimiwa la kusikitisha zaidi ni kwamba kuna taarifa hata ile asilimia 25 ambayo serikali imeongeza hawa jamaa zetu wa ZBC hadi leo hii hawajalipwa, aibu! Waziri aje atoe maelezo ya kina hapa, kwamba kwa nini hadi leo hii wakati mawizara mengine yameshalipwa asilimia 25 hawa jamaa hawajalipwa?

Mheshimiwa hiki chombo ni makini sana na ni chombo cha serikali itakuwa ni aibu sana kumuona mwandishi wa ITV au Radio One au Zenj FM anamudu kuvaa suti anapokwenda kazini hasa anapoingia katika majengo makubwa kama haya yetu, sisi anakuwa hawezi. Mimi nadhani kuwepo special allowance kwa ajili ya hawa. Kama sisi kanuni zinavyotutaka tuingie *smart* humu, hawa na wao wawezeshwe kuingia *smart* katika jengo hili, ili kuandika habari ipasavyo. *That is (a).*

Mheshimiwa (b), nieleze mapungufu kidogo, hakuna jema lisilokuwa na kasoro. Mheshimiwa kuna kasoro zimejitokeza kidogo katika hiki chombo, kinasikitisha sana au sijui kwa sababu hamjawapa maposho au kwa sababu mishahara mnaowalipa ni kidogo hawa waandishi wetu, inasikitisha sana

Mheshimiwa kwamba linatokea tatizo, wenzetu likitokea tu *on the spot, break news ITV* unaipata pale.

Inasikitisha sana achilia mbali habari mpasuko habari za kiporo hawa wanashindwa kuzileta, sijui sababu gani. Juzi ilianguka ndege wakati inataka ku-*land* pale Uwanja wa Ndege, Pemba. Niliisikia ndege ile usiku wa saa 6.00 nikapigiwa simu na mtoto wangu anarudi shule, ananambia baba nimeiona ndege imeanguka kule nje ya uwanja. Na mimi nilikuwa ninaangalia vyombo vya habari hatukuzisikia.Ni sababu gani ya msingi, Waziri uje unijibu.

Mheshimiwa jambo jengine, sisi tumetumia fedha za walipa kodi na tumekwenda kuchuna uso kwa wafadhili kujengewa *studio* ya pale Rahaleo kwa lengo la kuboresha habari katika nchi, ndio madhumuni tu ya kujenga lile jengo, leo inasikitisha sana Mheshimiwa, wizara inayosimamiwa na mtu makini, kama kaka yangu Mhe. Said Ali Mbarouk, kuona jengo ambalo tumelijenga ili kuweka mitambo ya kisasa linachezeshwa rusha roho, *shame!*

Na lile jengo tulililoliweka kwa ajili ya ZBC Radio kuona linatumiwa na Ofisi ya Magazeti, nataka Mheshimiwa utueleze *what is going on and what happened* mpaka kikatokea kitu kile, tukafanya mabadiliko ya dhamira halisi ya majengo yale.

Nimalizie katika hilo Mheshimiwa kwa kuja kwenye radio jamii. Mheshimiwa kama kuna radio zinazofanya kazi vizuri sasa hivi ni radio jamii, na hayumo Mhe. Subeit sasa hivi katoka kidogo, lakini watu wa Micheweni kupitia radio jamii kwa kweli wamepata taaluma sana. Sio tu katika maendeleo ya pale Micheweni, lakini hata katika sekta ya afya.

Tunaambiwa hawaendi kwenye chanjo lakini kupitia radio jamii hii sasa wanakwenda chanjo, kwenye polio, alimuradi sasa radio jamii pale Micheweni inafanya kazi vizuri. Sasa mimi ninaiomba serikali ikae karibu nao sana hizi radio jamii, ili kuona hazianguki. Iwasaidie katika misingi ya kiutawala, halkadhalika katika kutoa mambo ya kitaaluma ili zizidi kuboreka zaidi.

Juzi palipoingia moto hapa radio ile ilijitahidi sana, hata ikabidi masheha na madiwani kutoka katika wilaya nyengine wakakimbilia kuwasidia kuzima moto, jamani faida ndogo hiyo? Mimi nadhani ni kubwa na kuna haja ya kuiendeleza vizuri.

Kwa upande mwengine Mheshimiwa, nataka niigusie ile radio jamii iliyopo kule Makunduchi. Kwa kweli huyu kijana nimeambiwa ni 14 *years old* ndio *discoverer* wa ile radio na sisi hiki ni kipaji bwana. Leo serikali imekaa kim

ya, mpaka inatuletea leo, ilikuwa huyo kijana aletwe pale tumuone. Leo tunapata *verbal statement*. Huyu kijana anastahiki kuendelezwa, lakini sisi wazanzibari Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa na tatizo la kudharau vipaji, hii ni aibu! Wenzetu Mheshimiwa, hata hapo Bara hawana tabia ya kudharau vipaji. Hata vipaji vya wasanii hawavidharau wanaviendeleza.

Kwa mfano yule kijana aliyekuwa Sheikh Sharif, yule keshafikishwa Saudi Arabia na anafanya madigrii mengine kwa ile fani yake aliyonayo na serikali imemsaidia. Hivi juzi wamewachukua watoto wadogo wale akina Dogo Asley, na dogo dogo mwengine wamewapeleka kufanya mambo haya ya fine art technician. Kuna haja ya yule kijana aletwe hapa tumuone, serikali imsaidie na imuendeleze na akasomeshwe mambo ya *information technology*.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende katika masuala ya sekta ya utamaduni na michezo. Imeelezwa hapa katika ukurasa wake wa 149, Mheshimiwa. Kamisheni ya Utamaduni na Michezo nadhani hii iwe makini sana katika kungalia maslahi ya wasanii wetu, yanahitaji kulindwa, kuenziwa na kutunzwa. Hawa wasanii wanatuburudisha na wanavipaji wasanii wa Zanzibar, lakini tatizo serikali inawabeza, tunasema wapemba.

Tena kunawasanii maarufu hapa lakini wanashindwa kupata soko la kuuzia sanaa zao, ndani na nje ya nchi. Lakini tuwangalie wale wenzetu wa China, wale kuna mchezo unaitwa Dodo na wakwe zake wanazungumza Kichina lakini kompyuta wamezi- *translate* kwa Kiswahili. Tunanunua zile CD huku, kwa nini sie tushindwe kufanya *translation* ile kwa kupitia wasanii wetu makini, akina Bitele, Makombora na Halikuniki. Naomba hawa wasaidiwe.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika sekta ya uvuvi. Mheshimiwa, sekta ya uvuvi ni sekta muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu. Mheshimiwa juzi nilikwenda hospitali pale nikaambiwa niache kula nyama nyekundu, sasa nile nyama nyeupe. Mhe. Mwenyekiti, naomba unisikilize vizuri maana naona makofi yamekuwa mengi. Nikaambiwa niache kula nyama nyekundu, sasa nile nyama nyeupe kwa maana ya *marine food*. Kwa sababu hizi ni *delicious and nutritious*.

Sasa Mhe. Mwenyekiti katika hili nadhani kuna kila haja ya kuwafanya wavuvi wetu kuwawezesha kuweza kutuvulia vizuri, na kuwawezesha hawa tukapata hizo nyama nyeupe na wengi tukaachana kula nyama nyekundu, kwa sabau ya maradhi yaliyoingia Mhe. Mwenyekiti.

Leo hii wavuvi wakiweko Dago, Dago linauzwa anawekwa mwekezaji. Wananyanyaswa wanakuwa hawana pa kushika, wavuvi lazima wawezeshwe. Na wathaminiwe wavuvi sio kuwathamini wawekezaji tu kwa kuzichukua

fukwe. Halafu huyu Mkurugenzi Mussa ana bidii sana lakini hawezeshwi hata kufanya doria. Lakini kinyume na hivyo tutakuwa tunamlaumu tu yule kijana, kumbe ana nia ya kuendeleza uvuvi hatumuwezeshi.

Nimalizie Mhe. Mwenyekiti, ulinambia unazitaka hizi dakika ili utoe tangazo lako, kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu, Mheshimiwa mimi na wapiga kura wangu wa Jimbo hili la Wawi, Jimbo ambalo alitoka marehemu Dr. Omar Mungu amrehemu, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kuna jambo kidogo ambalo nilikuwa nataka kulifanyia masahihisho na lilikuwa linahusu suala la Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Wakati amemaliza kutoa taarifa yake nilimwambia aje aseme neno jengine yeye alisema hoja. Nilimwambia aseme uwasilishaji kwa hivyo ukweli ni kwamba Mwenyekiti alikuwa yuko sawa. Kwa hivyo, Kanuni zinamruhusu kusema hivyo, kwa hivyo nimuombe radhi Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nimemrudisha ni suala la kanuni na alifata kanuni.

Waheshimiwa wajumbe jengine nilikuwa nataka kuwaarifu tu kwamba wachangiaji wapo 12, ambao bado hawajachangia, muda wetu nilitarajia leo labda tutamaliza hizi Wizara mbili, lakini si dhani kama tutamaliza. Lakini ningewaomba sana kwanza wale ambao nitawataja wafike mapema hapa kwa ajili ya kuchangia. Lakini vile vile wakati tutakapokuja jioni basi tujali muda, ili na wengine wengi waweze kupata muda wa kuchangia.

Ahsanteni sana ninawashukuru kwa utulivu wenu, mchangiaji wa mwanzo atakuwa Mhe. Rufai Said Rufai, akifuatiwa na Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu pamoja na wengine watafuata, lakini hao wafike mapema kwa ajili ya kuchangia.

Baada ya kusema hayo waheshimiwa ninawashukuru kwa utulivu wenu tutaonana jioni saa 11.00, ahsanteni sana.

(Saa 7.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kama nilivyotangulia kusema kwamba wachangiaji wako 11 na katika hao tulikuwa tunaombwa na Mhe. Spika, kwamba tujitahidi leo tumalize kazi hii iliyoanza tangu jana. Kwa hiyo,

inawezekana sana wengine wakashindwa kupata kuchangia. Sasa Waheshimiwa ambao watapata fursa hii naomba watumie muda mchache. Ahsanteni.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru *Allah* kutujaalia uzima na afya nzuri jioni hii tukaweza kuhudhuria kikao hichi. Pia, kuweza kutupa nguvu ya kuweza kusimama na kutoa mchango wetu katika Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kama alivyoitangaza Mwenyekiti wa Kamati hii asubuhi hii ya leo.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana kamati hii kwa ujasiri wao mkubwa wa kuweza kutembelea katika wizara hizi na kuona yale mapungufu mbali mbali na leo tukawa tunachangia mbele yako ili wizara ziweze kujirekebisha baadhi ya mambo. Na zile haki ambazo ni za wafanyakazi katika wizara hizi na wao waweze kuona wizara imewajali wafanyakazi wake ili waweze kuendesha shughuli zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu utaanza na Shirika la Utangazaji, kuna maeneo hapa ya changamoto karibu matano. Lakini katika changamoto hizi nitaanza changamoto ya mwisho kabisa, naomba niinukuu hapa inasema kwamba;

> "Baadhi ya watangazaji wa *ZBC* hawako makini na kazi zao. Pia, wamekuwa wakikosea hata kutamka majina ya watu mashuhuri au mitaa na sehemu maarufu duniani, jambo ambalo linashusha hadhi ya shirika"

Mhe. Mwenyekiti, changamoto hii imesibu, hili ni tatizo katika shirika letu hili. Mara nyingi tumesikia wakati wa taarifa za habari au maelezo hasa wanapotajwa hata viongozi wa hapa Zanzibar ikiwa ni Rais, Makamu wa Kwanza au Makamu wa Pili, inathibitika kutajwa mtu jina lake tu, hata kutokupewa ule uheshimiwa aliokuwanao. Hili kwa kweli ni tatizo, hivi tunawaondoshea hadhi viongozi wetu na kwa kweli wenzetu hawa wa Shirika la Utangazaji tunaomba sana tuwajali sana viongozi na kuwapa heshima.

Kwa sababu Waswahili walisema kwamba, "Bwana mtu huitwa kwao", na kama kule nyumbani yale mahaba ya kupendwa hayapo, basi amini kwamba popote utakapokwenda heshima ile itakuwa haipo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ningeliliomba sana shirika, hizi heshima za viongozi kuzijali sana na kuwapa hasa heshima yao kuona kwamba hawa ni viongozi wa nchi. Kwa sababu nchi mdomo huu ndio wao wanaosemea kusema mambo ya Zanzibar jinsi yalivyo na yakatoka hewani vizuri, lakini

wasemaji ikiwa ile heshima ya wale viongozi hawaitimizi sidhani kwamba kutakuwa na mwengine atakayewapa hadhi hii.

Lakini pia, Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba katika taarifa za habari au katika vipindi fulani vya televisheni au redio, ningeliwaomba sana ndugu zetu watangazaji kwamba yule mwenye kile kipindi angalau ajitangaze jina lake japo mara mbili au tatu, lakini imekuwa ni tatizo kinakuwa kipindi kiko hewani kinaendelea pengine cha nusu saa au dakika 15 au saa, ukapata kutafuta huyu mtangazaji ni nani ukashindwa kulijua jina lake.

Jina lile linaweza kuja kutangazwa na mtangazaji mwengine wa kipindi chengine, kwa muda fulani mlikuwa na ndugu yetu fulani, aliyekuwa akizungumza kipindi fulani, lakini mwenye kile kipindi hawezi akajitangaza jina lakje. Sasa hili ni tatizo Mhe. Mwenyekiti, wenzetu hebu wajifunze, kuna televisheni mbali mbali, redio mbali mbali.

Kwa mfano mtangazaji wa *BBC* hachukui dakika tano kama hajalirudia jina lake, anajitangaza, mhusika wa kipindi hiki ni fulani *bin* fulani, mliyekuwa naye hivi sasa ni fulani *bin* fulani. Lakini watangazaji wetu hapa Zanzibar tatizo hili lipo mtu anaweza kukimaliza kipindi ukakosa kujua jina lake ni nani.

Kwa hivyo, ningeliwaomba sana hili Mhe. Mwenyekiti na Mhe. Waziri ajaribu, hili halihitaji taaluma wala hakuna chuo kinachomtaka Mwandishi wa Habari au Mtangazaji ende akasomee kujitangaza katika kipindi kile jina lake, hili ni yeye mtu mwenyewe tu kujitharifu akawa ile hamu ya kujulikana anaipenda mwenyewe na watangazaji wanapojulikana wanawasaidia wananchi wetu wengi hasa wanafunzi.

Kuna mitihani wanafunzi wameshafika kuuliziwa, taarifa ya habari iliyosomwa amesoma mwandishi gani au kipindi fulani cha redio kinaendeshwa na nani, wanafunzi wakafika kufeli kwa kutokuwajua. Sababu kubwa ni wao wenyewe kutokujitangaza vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende katika sehemu ya Redio Jamii, sitaki niseme sana hapa Mhe. Mwenyekiti, lakini niunge mkono kwa wale wenzetu wanaopata kuchangia nafasi hii kwamba hasa hawa vijana wavumbuzi Ramadhan Bilal Jihad pamoja na hao wenzake. Mheshimiwa hii ni taaluma kubwa, tena hawa vijana pale chini wapo wengi Mhe. Mwenyekiti, tunao vijana wajasiriamali wanazitaabisha akili zao, mawazo yao na ule utundu wao unawapa kupata taarifa mbali mbali na kuunga unga nyaya zao na mambo mengine wakaweza kuwasilisha katika maeneo yao, kama hii redio tunayosikia hapa hivi sasa maeneo mengi tayari inasikika.

Kwa hivyo, watu kama hawa tusione tu kwamba wameandikwa katika vitabu hivi vya habari za kamati, lakini ufuatiliaji hakuna.

Wenzetu watu kama hawa, basi hufanya bidii yoyote wakawatafuta na wakawaanzisha katika maeneo yao na wakawawekea vyombo ambavyo waanze kupata ile taaluma. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, uvumbuzi hapo mwanzo huyu aliyevumbua hebu tujiulize alianza vipi? Kuna chuo alichokwenda kusoma hapana, yeye binafsi tu alianzisha kwa akili yake Mungu aliyomjaalia kwa sababu Mwenyezi Mungu keshasema, *"Allamal-insana maalam yaalam"*, Mungu ametwambia hivyo, amemfundisha mwanadamu mambo asiyoyajua. Kwa hivyo, katika uvumbuzi ni mtu tu kupanga mambo yake akapanga panga, akija akiwasha lile alilolikusudia likaanza kufanya kazi.

Kwa hivyo, hii ni elimu inatoka kwa Mungu, amemfundisha mwanadamu jambo lile mpaka likawa jambo lina thamani na watu wanalijali. Sasa watu kama hawa ni vyema wizara ikafanya kwa makusudi hasa kuwatafuta na kutoa tangazo kabisa ili wale watu waweze kulifuatilia suala kama hili ili nchi yetu ione kwamba nao wana watu ambao wanaweza kuzitaabisha akili zao na tukapata kitu ambacho kitaleta maslahi kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hoja hiyo nije hoja ya 2.3.3 inayohusu Hoteli ya Bwawani. Mhe. Mwenyekiti, Kamati imefanya kazi kubwa na imejieleza wazi kwamba hoteli hii ilikuwa ni Hoteli ya Kimataifa hapa Zanzibar miaka ya 1974 – 1993. Lakini mwaka 1994 hoteli hii ilianza kukabiliana na matatizo ya uendeshaji wa biashara yake kutokana na hali ya uchakavu. Kama Mhe. Mwenyekiti, toka mwaka 1994 hoteli hii iko katika hali ya uchakavu hadi leo mwaka 2014, Kwa hivyo, si hoteli lililobakia hapo ni gofu.

Hoteli hii ni ya serikali na kama ni ya serikali imeshindwa kusimamia mambo yake, basi ni vyema ningeliiomba sana hii hoteli iibinafsishwe, wapo watu wanaitaka hoteli ile, isikae mpaka ikawa gofu, hatima yake tutakuja kukosa mambo yote. Kwa hiyo, ningeliiomba sana serikali angalau katika changamoto ya hoteli hii ninasema kwamba madeni sugu hasa ni taasisi za serikali pamoja na maofisi wanayoyakodisha.

Kama serikali yenyewe hailipi madeni ya hoteli hii jamani si hewa, hoteli hii ni jengo limejengwa na kama ni jengo linahitaji *repair*. Sasa kama muda wote huo hakuna marekebisho yoyote na hiyo serikali ikawa hailipi madeni vipi hoteli hii itakwenda. Kwa hivyo, serikali mimi ningeliwaomba sana zile nguvu za wananchi hawawezi kuzilipa, basi hoteli ibinafsisheni, apewe mwekezaji ili hoteli ile iweze kuhuwika na iweze kufanya kazi zake vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 53 kuhusu wavuvi. Wavuvi katika sehemu kadhaa hawana hakimiliki za ardhi katika madiko yanayotumiwa, ikizingatiwa kwamba hivi sasa maeneo mengi yamekuwa yakivamiwa na kuuzwa kiholela.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii ya Kamati mimi nakubaliana nayo kwamba ni kweli madiko mengi yako hivyo, wala nisiseme mengi madiko yote yako katika hali hiyo. Serikali kama wanayachukua haya madiko ya wananchi wakawa wanayakodisha kwa sababu hayana hakimiliki itakuwa serikali inawadhulumu wananchi wake. Kwa sababu hata hiyo serikali ina ardhi na majengo mengi, haina hakimiliki, kwa nini wao hawana na wananchi huko katika madiko hawana, kwa nini serikali isiwafanyie maarifa hao wananchi kuwapa hakimiliki katika maeneo haya? Kwa nini serikali iweze kuyachukua haya madiko wanayotumia wananchi wake wakaanza kuwakodisha wawekezaji, hii itakuwa serikali haiwatendei haki wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, asubuhi hapa Mhe. Hassan Hamad Omar, ametueleza kwamba kuna eneo la Chambavua. Mheshimiwa ukienda ukaona hiyo hali katika eneo hilo ambalo amepewa mwekezaji, eneo ambalo kabla ya kufika hili diko hapo nyuma kidogo pana mava ya wazee wetu, makaburi yamechakuliwa, watu bila ya kuthamini ile hali ya mwanaadamu kuwa mwanadamu yuko hai halafu yake atakufa, maiti zile zimeburuzwa tu ovyo ovyo. Kwa kweli hii haileti sifa nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, ukianza kutokumthamini maiti, leo kaburi tunaziuza tunatafuta nini, tunayauza mava ama tunachosubiri ni kiama tu hakuna jengine. Ardhi yote tumeuza hiyo faida iko wapi, jamani *astaghafiru llah* hatari hii. Maiti zimeburuzwa buruzwa tu kama mzoga, maiti za kibinadamu Waisilamu, hatari kubwa na hatima yake hawa wananchi walioko katika eneo hili wanaambiwa sasa wahame pale wende wapi na kwao ni hapa Zanzibar wanapata uchumi kutokana na bahari ile. Pana watu karibu 1,000, wana ajira ya bahari pale wakiwemo vijana na wazee wao wananunua madagaa, wanaanika, wanafanya na shughuli nyengine. Sasa watu hawa wamejiajiri wenyewe, leo wewe umepatiwa shilingi fulani unalitoa hilo eneo wananchi hawa wende wapi, halafu tuseme Zanzibar imejaa vibaka kwa nini pasiwe na vibaka.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hali kama hii mimi ningelimuomba sana waziri anayehusika na suala hili aende na wale watu wa ardhi na watu wa mazingira waende katika hili eneo. Mambo haya mimi naweza nikaamini kwamba pamefunikwa funikwa tu taratibu hazikufuatwa.

Mhe. Mwenyekiti, eneo hili ni moja katika eneo ilipo njia ya wananchi kwenda katika shughuli zao, mwekezaji huyu keshaweka senyenge eneo hilo na kudhibiti ili wale wananchi wasiweze kupita. Kwa hivyo, hakuna sheria inayomfanya mwekezaji kuwa ni bora zaidi kuliko muasisi wa nchi hii. Mimi siko tayari kuona kwamba Wazanzibari wenyeji wa nchi hii ndio wanaopata kuteswa kuliko mgeni aliyekuja kuwekeza hapa. Hii itakuwa hatuwatendei haki wananchi na mimi siko radhi na hilo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nina mengi, lakini kutokana na muda wako ni mdogo, basi naunga mkono ripoti hii.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii na mimi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jinsi ambavyo ametujaalia uhai na uzima na leo muda huu tukiwa katika Baraza lako tukufu la Wawakilishi kwa ajili kutoa michango yetu kwenye hoja hii muhimu sana ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na Wajumbe wake, miongoni mwa kamati ambazo zimesema ukweli kwenye ripoti yake ni Ripoti hii ya Mhe. Mlinde Mabrouk Juma. Kamati nyingi hujaribu kufichaficha mambo kama ilivyo tabia yetu ya kufichaficha mambo, lakini kamati hii ni miongoni mwa Kamati ambayo iko wazi na imetoa vitu kwa ajili ya manufaa ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nianze ukurasa wa 142 pale ambapo Kamati imesema kwamba kuna udhaifu wa watangazaji wa *ZBC*. Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niwalaumu watangazaji, nataka niwapongeze kwamba wanafanya kazi katika mazingira magumu. Sisi Wawakilishi mara kadhaa tumekuwa tukishuhudia watangazaji wakilalamika kwamba hawapati fursa ya Mafunzo. Vile vile, hawapati haki zao kama watangazaji. Sasa chochote ambacho watakifanya ni kutelekezwa na serikali kwa ajili ya kuwadhalilisha. Mimi siamini kwamba watangazaji wetu wamekuwa wazito kiasi hicho, lakini ni kwamba wamekosa mafunzo na naamini kuwa hawapatiwi fursa hata ya ndani ya nchi kwenda kujifunza badala yake wakubwa wanakata nchi kuelekea nje ya nchi kutafuta miradi mbali mbali.

Kwa hivyo, usipomfunza mfanyakazi wa ndani, kazi za idara mbali mbali kuwa ni safari za nje, usidhani kwamba watangazaji hao watakuwa na uwezo wa kutangaza. Hao *BBC* wanaofanya kazi vizuri sio kama sisi Zanzibar, wanalindwa, wanathaminiwa na wanashughulikiwa, sasa mimi sidhani kama watangazaji hawa watakuwa na miujiza ya kufanya kazi ikiwa hata posho hatuwapatii, ni nani anayepewa shilingi 5,000 duniani kama mtangazaji, fedha

zenyewe baada ya kugombana ndio zipatikane. Sasa utarajie mtendaji huyo kwamba atakuwa ni mbora na atakuwa na uwezo wa kutangaza!

Kwa hiyo, mimi niwapongeze kwamba wanafanya kazi katika mazingira magumu na niwape pole kwamba wamo katika hatari sana. Kwa sababu wanafanya kazi katika mazingira magumu bila ya kujaliwa.

Leo nimesikia kwenye redio Mkurugenzi wa *ZBC* amechaguliwa kwamba ni miongoni mwa jaji kwa kupitia kazi za waandishi wa habari kwa ajili ya kutoa tunzo. Najiuliza sijui *ZBC* watampata nani huyo wa kupewa tunzo. Nadhani Mkurugenzi atajifunza kwamba tunzo hupatikana kwa kazi nzuri za waandishi na kazi nzuri haiendi kwa elimu tu ya waandishi, lakini pia ni kuenziwa na kufanyiwa kazi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo wakati wa masihara uwe umekwisha, ajitahidi sana awalipe posho wafanyakazi wa *ZBC* kama ambavyo wafanyakazi wengine wanastahiki kupata haki zao za mafao. Tabia hii ya kuwalaumu tu kwamba hawafanyi kazi, hawavai vizuri wakati hatuwaenzi na hatuwasaidii nadhani si tabia nzuri na hatuwafanyii haki.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 146 Kamati ya Mhe. Mwenyekiti, imezungumza udhaifu wa Kampuni ya *ZMUS* kwenye mradi wa ving'amuzi, kwamba walikuwa na lengo la kutoa ving'amuzi 500,000, lakini hadi ripoti hii inaandikwa wametoa ving'amuzi 5,000. Mhe. Mwenyekiti, hii ni asilimia moja kwamba serikali imetenga fedha kuwapa wenzetu hawa kwa ajili ya ufanisi, lakini hadi hii leo wamepewa ving'amuzi asilimia moja. Mhe. Waziri, nataka anambie ni dunia gani, ni nchi gani iliyofikia ufanisi kwa asilimia moja ya kazi ya maendeleo? Kwa hivyo, mimi naungana na Mwenyekiti wa Kamati kusema kwamba mradi huu umefeli na Wawakilishi wako Mhe. Mwenyekiti, walisema mwanzo kwamba *AGAPE* si kampuni, lakini kama ilivyo katika serikali kubisha wakang'ang'ania na hatimaye wakampa mkataba na tunaona matunda yake.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wa Zanzibar wanaumia mnapong'ang'ania kuwapa watu fulani kwa maslahi ya serikali mnatuumiza. Leo Mhe. Mwenyekiti, ni nusu mwaka ving'amuzi ambavyo vimepatikana ni asilimia moja tu kati ya ving'amuzi vilivyokusudiwa.

Wakati naingia Barazani hapa nimetumiwa *message* na mwananchi mmoja wa Pemba ananambia nimpongeze Mhe. Waziri, kwamba Pemba hatuoni televisheni, lakini wanashukuru kwamba wakifungua televisheni huja

msalaba. Televisheni hawaipati, lakini wakifungua tu huo msalaba unakuja. Kwa hivyo, wananchi wa Pemba wanasema wanakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, tuache mzaha fedha hizi za *AGAPE* ni zaidi ya shilingi bilioni tano, leo watu wametulia wameridhika, unaposema humu watu hawakuelewi. Mhe. Mwenyekiti, naungana mkono pamoja na kamati kwamba mradi huu umefeli na mara moja mkataba uvunjwe na waliohusika kutia hasara, wawajibishwe. Hatuwezi kuwalinda watu kwa maslahi ya watu wachache. Leo asilimia moja Mhe. Mwenyekiti, ambayo imeingizwa na *AGAPE* ndio mradi wa maendeleo wa mwaka mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba serikali waache ubishi na wasiendelee kuangamiza fedha za umma. Wawakilishi wanapozungumza humu ndani ya Baraza, basi wawe makini sana kutekeleza ukweli, Wazanzibari kamwe hawakutegemea kuona picha ya msalaba tu, walitegemea wapate matangazo ya ndani na nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nitoke hapo niende kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi na niungane mkono kabisa na ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati ukurasa wa 153.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umebakia dakika tano.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, serikali haiko pamoja na wananchi, naomba kwanza nipewe kigezo ni kigezo gani ambacho kilitumiwa na serikali kuwazuia wananchi wa Jimbo la Kiwani, Micheweni, Vitongoji na sehemu nyengine na kuwapeleka Mahakamani kwa kuharibu mazingira, lakini ikawa halali mwananchi mzalendo wa nchi za nje kutumia madoza na kuharibu mazingira eneo la Nyanjale? Ni kwa nini mwananchi wa ndani anapoharibu mazingira, basi huwa rahisi kupelekwa Mahakamani na kufungwa au faini, lakini mzalendo wa nje ya nchi eti mwekezaji inakuwa halali kuharibu mazingira mbele ya macho ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, mimi nina kila sababu ya kusema kwamba mradi ule wa Nyanjale Kiomba Mvua yapo maslahi binafsi ya watu fulani.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa mdogo nilikuwa nikisikia kwamba kuna siku watakuja majuji watakuja kula mawe, nilikuwa sifahamu nini maana yake, mimi ninaekaa kule Mwambe kwenye majabali, nilikuwa nafikiria kwamba siku moja watakula yale majabali yote, leo watu wanafika hatua ya kuchimba makaburi alimradi tajiri apate maslahi yake Mzanzibari mnyonge aondoke.

Mimi nilibahatika kupata barua ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B'. Mhe. Mwenyekiti, naomba niisome kwa heshima yako ili nimalizie mchango wangu.

> "Yahusu Kujenga bila kufuata taratibu za kisheria ndani ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B' katika eneo la Nyanjale.
>
> Kwa heshima naomba uhusike na mada ya barua hii. Baada ya ukaguzi wa wakaguzi wetu umegundua kuwa kunaendeshwa shughuli za majenzi yaani ujenzi wa banda la makaazi ya fukwe kwa mujibu wa sheria Nam. 4 ya mwaka 1995 chini ya kifungu cha 5(1)(c) "mtu au taasisi yoyote inayotaka kujenga ndani ya Mamlaka ya Halmashauri hii inawajibika kufuata taratibu zilizowekwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B'"

Kutokana na agizo la Makamu wa Pili wa Rais, narejea Mhe. Mwenyekiti, na kutokana na agizo lililotolewa na Makamu wa Pili wa Rais, unatakiwa uhamishe shughuli zote za ujenzi katika eneo hilo mpaka utaratibu utakapofuatwa.

Mhe. Mwenyekiti, barua hii walipelekewa wazalendo Wazanzibari. Ni wazi kwamba Makamu wa Pili wa Rais alitoa agizo kwamba watu wale wazuiliwe, mimi nilitegemea kwamba baada ya hatua hiyo, basi wangeelekezwa namna ya kujenga ujenzi halali, lakini hatima yake jana wanakwenda polisi *defender* zaidi ya mbili chini ya usimamizi wa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya, watu wanavunjiwa na kwa ile hamu ya kuvunja mpaka makaburi yanafukuliwa. Mhe. Mwenyekiti, mzalendo hana haki katika nchi hii?

Mhe. Mwenyekiti, wataalamu wanasema "njaa siku zote asili yake tumboni". Lakini mwanadamu anapoitoa njaa tumboni akaiweka kichwani ni wazimu. Nimeomba sana watufahamushe njaa tumboni kwenda kichwani. Njaa ikihama tumboni na kwenda kichwani inakuwa wazimu.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wa Nyanjale hawakufanyiwa haki, ni dhahiri kwamba wazalendo hawana haki kuliko wageni, ili mradi uwe na fedha yako tu. Na mimi naomba nitumie kanuni ya 120 na naomba Wawakilishi wenzangu wenye uchungu na wananchi wao, hoja yangu hii waiunge mkono.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitumie kanuni ya 120 kuliomba Baraza lako liunde kamati teule maalumu kwa ajili ya kuchunguza kwa nini mgeni akapata nguvu ya kuharibu mazingira pale Nyanjale wakati Mzawa hana haki hiyo.

Mhe. Mwenyekikti, nina wasi wasi kwamba pale pahali imetumika nguvu kubwa ya fedha. Kwa hivyo, hapa nikikubaliwa nitaunga mkono hoja hii na naomba Waheshimiwa wenzangu waniunge mkono kuhusiana na hoja hiyo. Ahsante sana.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kufika jioni hii katika hali ya usalama na afya njema sote.

Pia, Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Ripoti hii ya Kamati ya Mifugo, Utalii na Habari. Kwani ripoti ni nzuri imekamilika chini ya Mhe. Mwenyekiti wetu Mhe. Mlinde Mabrouk Juma, nampongeza sana na Wajumbe wake wote waliofanya kazi hii nzuri na tumeelewa kwa vizuri kabisa nawashukuru sana. Kabla sijaanza kuchangia niseme kwamba naunga mkono ripoti hii asilimia mia kwa mia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitagusia sehemu mbili kwa haraka haraka bila kupoteza muda wako. Nitagusia sehemu ya Habari na Utalii katika nchi yetu.
Mhe. Mwenyekiti, nianze na Sekta ya Habari, kama unavyojua sekta hii ni muhimu sana hasa katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba kwani habari nyingi tunazipata katika visiwa hivi kupitia *ZBC,* Redio na *TV*.

Pia, Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Utamaduni, kwa juhudi zake kubwa anazochukuwa katika sekta hii. Lakini hasa katika Sherehe za Mapinduzi ya miaka 50. Nimpongeze hasa katika mchezo wa mpira wa miguu katika *Mapinduzi Cup*. Kwa kweli Mhe. Waziri, kafanya kazi kubwa na tumeiona sote, kajitahidi kwa roho yake na kwa udhati kabisa kufanikisha mashindano haya na kuwa mazuri kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwanza *ZBC TV* mimi nasikitika kidogo hapa *TV* yetu hii tunaitegemea sana. Mimi mwenyewe naweza kusema kwamba siwezi kusikia raha au nikafurahia kama sijaangalia *ZBC TV*. Mbali ya kuwa na *TV* nyingi, lakini *ZBC* ina raha yake Mhe. Mwenyekiti. Lakini nasikitika sana endapo unakatika umeme, basi matangazo hayo hayapatikani tena kwa siku ile au mpaka umeme uwashwe.

Kwa hivyo, naomba sana wizara kupitia Serikali yetu ya Mapinduzi kufanya kila njia kupata jenereta la akiba endapo ukizimika umeme, maana matangazo yake huruka mia kwa mia.

Pia nasikitika sana kwamba wenzetu hawa wa *ZBC* wanafanyakazi kwenye hali ngumu hasa pale kwenye kituo. Kama ripoti ilivyoeleza hapa nilivyoona, hata uhaba ya *DVD* sasa hizi zikiwa huwa tabu kuweza kurikodia wenzetu na

kutia kwenye kumbukumbu zao. Kwa hivyo, naomba wizara au waziri awasaidie sana kupitia serikali yetu bajeti ya kununua hizi *DVD* kwani hizi sio gharama kubwa. Hivyo, nafikiri moja haifiki hata shilingi elfu tano. Nawapongeza sana wenzetu hawa kwa juhudi zao na kujitahidi matangazo haya yasikatike.

Mhe. Mwenyekiti, pia nisikitike tena wenzetu hawa wana majukumu mengi ya kununua hizi *DVD* na jenereta. Lakini nasikitika kwa ripoti hii ya kamati kwa Baraza kuwa *live* masaa yote. Lakini nashangaa yakitokea matatizo hawalipwi *ZBC* fedha za kipindi *live* kama hiki.

Kama unavyojua matangazo kama haya yanakuwa na pesa nyingi na gharama kubwa. Lakini naomba serikali na wizara iweze kufatilia suala hili waweze kulipwa wenzetu hawa kwenye masuala mbali mbali pamoja na vifaa vya matangazo.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wetu hawa wanapewa posho la shilingi elfu tano kwenye Baraza letu. Na kama unavyoona wanasimama masaa mengi sana. Na kazi kubwa ya kutumia utaalamu na akili hapa. Mimi naomba wizara kupitia Baraza letu iwafikirie angalau posho la shilingi elfu kumi waongezewe hasa kwa kutumiza miaka 50 ya Mapinduzi yetu Matukufu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, tangu Baraza la nyuma mpaka hivi leo Baraza linaendelea hawajalipwa hata posho. Kwa kweli wana hali ngumu sana ya maisha wakipitia kwenye kazi zao hizi za kurusha matangazo. Mhe. Mwenyekiti, hawa fundi mitambo na wapiga picha nao wafikiriwe sana kazi yao ni kubwa na inataka watumie akili.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu nitoe kwa wasanii wetu ambao wako Zanzibar wanapata tabu sana, hasa kurikodi nyimbo zao. Mimi nitoe mfano mdogo nilikwenda Dar-es-Salam kipindi fulani kuna *Studio Special* kwa ajili ya wasanii na Mhe. Rais wa Tanzania ndio katoa hizo pesa na hiyo *studio* ambayo inaitwa *THT* .

Kwa hivyo, naomba huu mfano wa Dar-es-Salam, kazi hii naomba iende kwa wenzetu hawa wakajifunze *studio* hii iko vipi. Kwa hiyo, nampongeza sana muongazaji huyu kuwa makini sana na yuko makini kuwafundisha wasanii wetu wa Tanzania.

Kwa hivyo, naomba tuige mfano huu wa wenzetu ili na sisi tukaweza kurikodi nyimbo zetu bila ya wasi wasi. Kwani kama tunavyojua wasanii vipaji wanavyo na wanatakiwa kidogo katika msukumo wa serikali yetu. Kama tunavyojua kwamba siku hizi mziki ni ajira.

Mhe. Mwenyekiti, sekta yetu ya Utalii kama tunavyojua kuwa ni roho ya nchi yetu. Uchumi mkubwa sasa tunao kwenye sekta ya utalii. Lakini niseme kidogo tu katika wageni wetu wanaokuja kutembelea visiwa hivi vya Zanzibar, saa nyengine inakuwa usiku na wanaibiwa sana na watu ambao wasiojulikana. Mhe. Mwenyekiti, ulinzi unakuwa mdogo sana na hawa watalii wanapenda kutembea saa za usiku.

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana hawa askari jamii wa Mji Mkongwe. Kwa kweli askari hawa wanafanya kazi nzuri na wanajitahidi sana kuuweka mjini Mkongwe katika hali ya usalama. Mhe. Mwenyekiti, hawa wawekezaji nao pia wanahitaji kuekewa ulinzi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono pamoja na wananchi wangu asilimia mia juu ya mia kwa ripoti hii. Ahasante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nachukuwa nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia jioni hii kuwepo hapa kutelekeza majukumu yetu ya kitafa.

Pili, nachukuwa nafasi ya kukushukuru wewe kunipa nafasi hii ili na mimi kuchangia mawili matatu katika kazi yetu hii.

Pia, nachukuwa nafasi ya kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa ajili ya kutuwasilishia ripoti hii nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, mimi mchango wangu utakuwa si mkubwa sana nitaanzia na Shirika la Utangazaji *ZBC*. Hapa nitakwenda kwenye changamoto. Mhe. Mwenyekiti, kuna changamoto nyingi zimezungumzwa hapa. Kwa kweli neno changamoto ni matatizo. Miongoni mwa changamoto ambazo zinaikabili *ZBC* ni nyingi.

Kwanza *ZBC* haina uhakika wa matangazo yake hasa pale inapotokea ukatikaji wa umeme na kukosekana kwa jenerata.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo kama tunavyosema kwamba Vyombo vya Habari ni mdomo wa serikali na ndivyo vinavyotoa habari tofauti zinazotokea katika nchi. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri, hili alizingatie sana hasa suala la upatikanaji jenereta alipe kipaumbele.

Pili, kukosekana kwa taarifa za *TV* kisiwani Pemba. Hili ni tatizo na tatizo hili linazungumzwa muda mrefu nafikiri toka lianze Baraza hili mwaka 2010 mpaka leo tatizo hili halijatatuka. Labda nimuulize Mhe. Waziri, tatizo hasa

ni nini awaeleze wananchi wa Zanzibar kwa nini matangazo haya hakuna Kisiwani Pemba.

Mhe. Hija Hassan Hija, amesema hapa amerushiwa *Message* hapa na wananchi wa Pemba wamesema kwamba wanashukuru kwamba wanapofungua *ZBC* waona msalaba. Tunakuomba Mhe. Waziri, suala hili kwa kweli uende mbio zako zote ziingie kwenye tumbo. Lakini tuhakikishe kwamba watu wa kisiwa cha Pemba wataona mambo mbali mbali yanatokea katika nchi hii na nchi nyengine kupitia *ZBC*.

Mhe. Mwenyekiti, mengine yameshaelezwa kimustasari, lakini na mimi nitaieleza hivyo hivyo, Baadhi ya watangazaji *ZBC* hawapo makini na kazi zao, pia wamekuwa wakikosea hasa kutamka majina ya watu mashuhuri au mitaa na sehemu maarfu duniani. Jambo ambalo linaharibu hadhi ya shirika. Mhe. Waziri, hili ni tatizo na mimi nataka niseme kwamba hivi kuna vyombo vingi vya habari vya watu binafsi.

Sasa tunatakiwa tujitahidi sana na wafanyakazi wetu ili waendane na soko la uandishi wa bahari na utangazaji liliko hivi sasa. Kwa kweli nasikitika sana kwa kuwa miongoni mwa kazi muhimu na nzuri na utamaduni ni kazi ya utangazaji, kazi ya uandishi. Kwa hivyo, vijana wetu tunapaswa watu wa shirika tuwe makini kuwaelekeza ili wafanye kazi zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti inasikitisha sana kuona kwamba watangazaji miongoni mwao wanakuwa na matatizo ya namna hii. Lakini mimi nashauri waandishi wa habari na watangazaji wote wawaige kama Fatma Said, huyu anasifiwa hapa na Waheshimiwa. Kwa hivyo, nawaomba watangazaji wote waithamini vyema kazi yao na wafanye kazi kwa madaha na kwa maringo ya kuipelekea mbele taasisi hii ya habari ili wasiwe miongoni mwa wenye kudharauliwa.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 145 Kamati imegundua kwamba katika vyombo vya habari vya watu binafsi kumekuwa na ufanisi wa kazi na vimejipanga vizuri. Hivyo, kamati ina wasi wasi kwamba kutokana na mwenendo ulipo sasa vyombo vya serikali vinaweza kukimbiwa na wasikilizaji na watizamaji.

Mhe. Mwenyekiti, ina maana hapa tuige baina ya vyombo vya serikali na vyombo binafsi. Namuomba Mhe. Waziri, ajitahidi ipasavyo akiboreshe chombo chetu cha Shirika la Utangazaji ili liende na wakatii lisiwekwe nyuma. Kuwekwa nyuma kwa shirika letu, kwa kweli ni tatizo na mtihani mkubwa na hatuipeleki mbele serikali yetu ya Zanzibar, bali tunairudisha nyuma. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, aliangale vizuri suala hili ili tuende na wakati.

Niende katika changamoto za Tume ya Utangazaji hii ya mwisho ni ukosefu wa jengo la ofisi lenye hadhi ya Tume. Serikali tunaishauri mara nyingi na tunaishauri mambo mengi na mawaziri husema hapa kwamba serikali yetu ni sikivu. Huu usikivu uko wapi kila ripoti inayoletwa hapa ina mambo makubwa ambayo ni ya kasoro tena zinakuwa nyingi zaidi kuliko ufanisi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, ukosefu wa jengo la ofisi yenye hadhi ya Tume lichukuliwe hatua ili hii ofisi iwe na hadhi ya Tume ya Utangazaji, watangazaji ni watu muhimu, maarufu, wanaotoa taaluma. Kwa hivyo, ofisi yao ionekane nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Kamisheni ya Utalii ukurasa wa 147 kuna kipengele nukta ya kwanza hapa. Kinasema upatikanaji wa takwimu sahihi za watalii wanaongia nchini, ambapo huathiri mipango ya uendelezaji na utangazaji wa watalii.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo, kwa kweli zipatikae takwimu sahihi ili ijulikane kabisa Watalii wanaoingia ni wangapi, mapato yanayopatikana kwa mujibu wa utalii ni namna gani. Kwa sababu bila kujuulikana takwimu sahihi, kwa kweli itakuwa hatuwatendei haki watu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 150 Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale. Hapa nitaelezea mambo machache tu. Kuna maeneo mengi ya historia katika maeneo yetu mbali mbali, sijui wizara inayaangalia vipi maeneo haya. Kuna misikiti ya asili ya zamani kama vile Mkumbuu, Mkamadume na Chambani, katika jimbo langu kuna msikiti unaitwa Mjini Chambani, sijui mnayaangalia vipi magofu haya na haya ni maeneo ya historia.

Vile vile, kuna maeneo ya Jambangome ambapo mji wa Jambangome ni miongoni mwa mji mkongwe sana katika maeneo ya Pemba na kule kuna magofu mengi ya kihistoria sijui mnayaangalia vipi masuala haya na mnawaeleza vipi wananchi na historia ya maeneo haya ambayo ni ya muda mrefu sana.

Pale Chambani kuna watu wamefariki wakiwa na umri wa miaka zaidi ya mia moja. Lakini ukimuuliza historia ya lile jengo lilipo pale mjini Chambani, kwa kweli anashindwa kukueleza kiusahihi. Je, wizara inayaangalia vipi majengo yale na historia yake.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Sekta ya Uvuvi nitazungumza mambo matatu. Miongoni mwao nitakayozungumza ni ufugaji wa samaki. Mhe. Mwenyekiti, kuna maeneo mengi wananchi wetu wamejiajiri kwa ufugaji wa samaki.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umebakiza dakika tano.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Ufugaji wa samaki umeenea katika maeneo mengi sana. Lakini inasikitisha sana kwamba watu hawa wafugaji wa samaki, wizara haiwatembelei haiwapi taaluma haiwawezeshi katika ufugaji wa samaki.

Katika jimbo langu la Chambani kuna wafugaji wa samaki maeneo mengi tu. Lakini kila mwaka wanakula hasara kutokana na miundo mbinu ambayo wanaiweka pale ya kujenga yale matuta kutokana na umasikini. Kwa hivyo, naiomba wizara iwatambue wafugaji wa samaki na iwaendeleze kimaisha ili waweze kujiwekea mitaji ambayo itawaongoza katika maisha nyao.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu dakika zangu zimebakia chache niende katika Diko la Nyanjale Kiombamvua. Mhe. Mwenyekiti, wasemaji wengi wamelizungumzia suala hili. Kwa kweli hili ni tatizo na ni masikitiko ya hali ya juu kabisa. Wananchi wa Nyanjale ni Wanzanzibari wamekaa pale kwa ajili ya kujitafutia maisha na serikali kila siku inatamka kwamba watu wajiajiri, Watu wa Nyanjale wamekaa pamoja kuvua pamoja na kina mama kununua dagaa na kuwaanika na kuuza.

Lakini leo wametokea wajanja, mimi sisemi wawekezaji kwa sababu wawekezaji hawawezi tu kuingia pale ila itakuwa wameruhusiwa na serikali. Mimi naiomba serikali kama ambavyo ilifanya mapinduzi kwa ajili ya kuirejesha ardhi ya Wazanzibari kwa Wazanzibari, tusiwaondoe Wazanzibari katika maeneo yao wanayopatia riziki zao.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo. Tatizo hili litaondoka lini? Tuangalieni katika fukwe zote za Zanzibar zimejengwa na watalii na Wazanzibari wenyewe wameondoka katika maeneo yale. Waheshimiwa hawa Wazanzibari tunawatafutia ajira au tunawatafutia nini zaidi ya udhalilishaji wa namna hii. Inasikitisha sana hivi leo inasemekana kwamba miongoni mwa usafishaji wa eneo la Nyanjale hata watu waliozikwa miaka kadhaa viwiliwili vyao vinafukuliwa. Mhe. Mwenyekiti, *innaa lillaahi wainnaa ilayhi raajiun.*

Nataka nimalizie maneno yangu kwa kusema kwamba kwa kweli ikiwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mwakilishi, Mbunge, Rais, kuna neno alikumbuke Mwenyezi Mungu anasema "Kisha mtaulizwa siku ya kiyama juu ya neema mlizoneemeshwa na Mungu".

Cheo ni miongoni mwa neema, tuvitumieni vyeo vyetu kwa kuwatendea haki na wema wananchi wetu Wazanzibari wajisikie kwamba wanakaa Zanzibar yao iliyo huru, wasikae katika Zanzibar yao ambayo kila wakati wanakuwa wanameza mate machungu kwa madhila ambayo wanafanyiwa na miongoni mwa viongozi.

Mhe. Mwenyekiti, naheshimu muda wako, kwa hayo machache nasema ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nishukuru kwa kunipatia nafasi hii, lakini kabla ya kuanza mchango wangu naomba uniruhusu niipongeze Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano baada ya kupata taarifa jana usiku kwamba kuna boti inazama. Na mimi nilipopata ripoti hiyo nikachukua hatua ya kumpigia Mwenyekiti wa Kamati haraka anisaidie kuwatafuta wengine. Baada ya kupigiwa Naibu, tukampigia na Waziri wa Miundombinu, nataka niwapongeze kwa dhati walichukua hatua hiyo mara moja na tukafanikiwa kuwaokoa wenzetu wale wote walipatikana kamili na hakuna aliyekufa isipokuwa wamepoteza mizigo, na mizigo ni kitu cha kupatikana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo nataka nianze na mimi niipongeze sana ripoti hii na nimpongeze sana Mwenyekiti kwa umahiri wake alivyokuwa akiwasilisha pamoja na Wajumbe wake wote waliofanya kazi hiyo, lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze na mifugo na hasa pale ilipoelezea uvamizi wa mashamba.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze na shamba la Kipange ambalo nalikumbuka shamba hili lilikuwa linazalisha ndama wazuri lakini kwa muda mrefu nimekuwa sioni harakati katika shamba hili, na hili lilikuwa ni shamba la Serikali. Niombe Mhe. Waziri atakapokuja basi aweze kunieleza hili nalo limevamiwa na nani? Kwa sababu zamani mimi nakumbuka utaratibu Serikali ikianzisha mradi wake mahala na ukifeli basi ilikuwa ile sehemu huwapatia wananchi wake wakaweza kuitumia hadi pale itakapoweza kujipanga tena kurejesha mradi ule, wanarudia kuwaomba tena wananchi wao wanalitumia lile eneo. Kwa hiyo mimi nilitaka kujua ili tuone basi kama kuna mtu labda amepewa au mimi nilitaka nipate habari zake nizijue na kwa nini labda kama aliyepewa basi wasikatiwe na wale wananchi wa pale na wao wakaweza kufaidika nalo.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende katika shamba la Pangeni. Shamba hili mimi tangu utoto wangu nalifahamu ni shamba la mifugo lilikuwa na mifugo mingi na lilikuwa limezungushwa senyenge, lakini leo nasikia shamba hili nalo limevamiwa. Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha na niiombe sana Serikali kwa

nini mnayaachia kiholela maeneo yake. Kwa sababu hili shamba lilikuwa limezungushwa senyenge *wallahi* wavamizi walikuwa ni watoto waliokuwa wakiingia kuokota embe basi. Lakini kama ilikuwa sehemu zimebomoka zikashindwa kurejeshwa kwa hiyo tutamlaumu nani? Kwa hiyo Serikali mimi naomba ijipange na kwa sasa ardhi ilivyokuwa imekuwa tatizo inapokuwa na maeneo iyadhibiti.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilitaka niseme kuhusu eneo la Nyanjale ambalo wenzangu hapa wanalitaja sana, lakini nataka nilitaje kwa ninavyofahamu mimi.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli eneo hili kuna wanaoanika dagaa na ni wengi, na pia nichukue fursa hii kuwapongeza kwa sababu siku zote tunawahamasisha wananchi wetu kwamba wajiendeleze katika miradi mbali mbali ili wajikwamue na umaskini. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze na sisi viongozi. Sisi viongozi maana ya kuletwa hapa kwa sababu wenzetu wametuamini sana. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, si vyema sisi tunapolisikia jambo tu labda tukalichukua tukikupa kwa sababu kazi yetu sisi kwanza kuwalinda hawa wananchi wetu wasipambane na matatizo. Kwa hiyo sisi tunapolisikia jambo tusiripuke tu tukalitia sherehe tu, tukaingia jazba hapana, wajibu sisi turudi chini kulifuata hili jambo liliko tukalijua ukweli wake ukoje.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachokumbuka katika eneo hili kulikuwa na Kamati iliundwa na wakakubaliana na mwekezaji wakampa masharti, na masharti mwekezaji alikubaliana nayo hakuwapinga. Walimtaka awajengee soko mwekezaji kalijenga, walitaka watengenezewe uwanja wao mwekezaji katengeneza, pia walitaka miundombinu ya maji ili waweze kuvutiwa maji kule yaliko yaje pale wanapotaka kufanyia wao shughuli yao, mwekezaji amefanya hayo yote.

Tatizo linalojitokeza ni wao kwamba ile sehemu ambayo walikuwa wanaitumia na ndio yote kukubaliana na haya kwa sababu mwekezaji ile sehemu amewakataza kama hapa kuna uwanja wa gofu ule haitakubalika tena pale kuanika dagaa. Mhe. Mwenyekiti, hayo yote yamefanywa na pia mwekezaji kakubali atawapa boti, mwekezaji kakubali kuwanunulia gari na tayari ipo, kwamba pia wasipate usumbufu kutoa lile dagaa kule ndani kulileta barabarani au kupeleka wenyewe wanakohitaji.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema sisi viongozi hatuna tofauti na waandishi wa habari. Mwandishi wa habari akiitumia kalamu yake vibaya akiandika vibaya anaweza akasababisha matatizo makubwa yapatikane. Pia

akikitumia chombo chake cha habari akirusha matangazo vibaya inaweza ikasababisha matatizo. Lakini na sisi kwa sababu tunaaminiwa na wengi, kwa hiyo mtakapolitoa tu hapa jambo maana yake wakisikia wananchi wetu huko wanaweza wakalipokea ndivyo sivyo. Kwa hiyo sisi tunatakiwa tufanye utafiti kwanza wa kina tulijue jambo hili baadae ndio tukija tukilisema hapa, maana yake tuna umadhubuti mzuri tu wa kuwa tunalijua jambo hili. Kwa hiyo tunakuja hapa sasa kwa kuwatetea wananchi wetu.

Lakini tukichukua jazba tu hatutakwenda Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu sisi viongozi hatutakiwi tuwachochee wananchi wetu, tunatakiwa sisi ulipo mgogoro tukautulize. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, sisi tumeunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa hapa, lengo ilikuwa tayari ni kuondosha ile migogoro na hasama na magomvi haya ya kila wakati. Kwa hiyo leo kama sisi viongozi tunashabikia linapotokea jambo kama hili fanyeni tu, msiondoke kaeni hapo hapo itakuwa hatutendi haki, sisi tunatakiwa kwenye migogoro twende.

Sasa mimi niwaombe sana wenzetu hawa ambao wajasiriamali wenye kuanika dagaa. Viongozi wapo kuna Mwakilishi na Mbunge katika Jimbo lao, tena niseme wao wana nafasi ya pekee. Kwa sababu katika Jimbo la Kitope Mbunge wao ndio Makamu wetu wa Pili wa Rais. Kwa hiyo wana nafasi nzuri, lakini kama kuna Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa pia hawaridhiki na maamuzi yake uongozi bado upo mbele. Wapo Mawaziri wanaohusika na hii sekta yenyewe kwa nini wasifike wakatoa lalamiko lao wakaja wakasikilizwa.

Lakini pia uongozi haujesha yupo Mhe. Rais hawezi akakubali kuona watu wake wanagombana hawa ndio wapiga kura wake. Kwa hiyo angekubali hili akalituliza kwa hali yoyote ili wananchi wale warudie katika hali yao nzuri. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba lazima sisi viongozi tukilisikia jambo kwanza tusiripuke kwa sababu jazba, malumbano hayatasaidia wala hayatawasaidia watu wetu. Kitakachowasaidia watu wetu ni kuwasaidia wanapokuwa na kadhia yao sisi tukaweza kuisimamia hatimae wao wakaweza kufanikiwa. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka kusema hilo kwa hapo niende katika Idara ya Habari.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Habari naomba na mimi nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri hasa kwa kuwekea nyasi ule Uwanja wa Amani. Lakini pia mimi nataka nimuombe Mhe. Waziri nchi yetu inakua na tunaendelea na sisi siku hadi siku. Kwa hiyo ni vyema na sisi tukaanza hivi sasa hasa tunavyojua tatizo la ardhi linazidi kutupungukia. Tukaweza kutafuta kiwanja kwa sababu kiwanja cha Amani kwa sasa kinaonekana kinakuwa kidogo hakitutoshelezi. Kwa hiyo ni vyema Serikali hivi sasa ikaingia mbioni

kuweza kutafuta uwanja mwengine ili tukajenga uwanja wa kisasa na utakaokuwa mkubwa utakaotutosheleza.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika idara zetu hizi Shirika la Utangazaji. Mimi napenda nichukue nafasi hii kwanza kuwapongeza waandishi wetu wote hawa wa *ZBC* Radio na *TVZ.* Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu lakini tushukuru wazalendo. Kwa hiyo mimi naomba Mwenyezi Mungu awazidishie uzalendo wao waweze kufanya kazi kizalendo, lakini wenzangu wengi wamesema hapa pale inapokuwa neema ipo na sisi tuwatumie hawa hawa ndio wakati wa shida tunakuwa nao. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, hilo mimi nilitaka nilisisitize.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka pia niungane na maoni ya Mwenyekiti alipokuwa akitoa hotuba yake pale asubuhi aliposema hawa Maofisa wa Mifugo watutembelee. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli watakapotutembelea maofisa hawa kwanza wao wenyewe watapata kugundua mambo mengi, lakini watapata na sisi kutupa elimu ambazo zitatufanya ile mifugo yetu maradhi yanapojitokeza haraka haraka tuweze na sisi kuyatambua. Yale ambayo yatakuwa hayawahitaji wao sisi tutaweza kuyadiriki na kuwatibu wanyama wetu. Kwa hiyo ile kututembelea sisi tungeweza kupata elimu mbali mbali lakini pia na wao wangepata kujua changamoto ambazo zingewasaidia wao katika kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi naiunga mkono ripoti hii na naipongeza sana na naitakia kila la kheri. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa sababu kwa kweli niliomba mapema sana, na inaonesha ulinisahau lakini nakushukuru kwa kunikumbuka. Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nilikuwa na mambo matatu madogo sana.

La kwanza Mhe. Mwenyekiti, mshahara ni haki ya kila mfanyakazi. Na kwa kuwa tulipitisha hapa bajeti ya kwamba wafanyakazi wetu wote wa Serikali waongezwe mshahara kuanzia kima cha juu mpaka kima cha chini. Sitokubaliana kuja kupitisha bajeti ya Wizara hii ikiwa hawa wenzetu hawajalipwa nyongeza yao ya mshahara, lakini vile vile na *arrears* zao. Kwa sababu wenzao wote walilipwa nadhani kama sikosei ilikuwa kuanzia mwezi wa Oktoba. Kwa hiyo nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri wetu mpendwa tunampenda sana, hodari sana kwa kazi, lakini kwenye hizi haki za watu naomba sana ajaribu kuzisimamia. Na Mhe. Waziri wa Fedha hayupo hapa lakini kwa kweli hili suala lazima kuwepo mashirikiano baina ya Wizara ya Fedha na Wizara hii ya Habari. Mhe. Kaimu Waziri wa Fedha yupo

nashukuru kumbe kanisikia, na naamini pengine na yeye anaweza akatoa ufafanuzi baadae.

Mhe. Mwenyekiti, limezungumzwa sana suala la waandishi wa habari kwenda na sisi Dodoma. Mimi nitashangaa sana kwamba huu ndio mdomo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hivi juzi tumeadhimisha maadhimisho ya miaka 50 ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa leo Wabunge wao, maana yake sisi tukisha kufika kule sote tunaitwa Wabunge, wakasema maneno yao, wao waje wachukue kupitia katika redio za wenzao itakuwa ni aibu kubwa sana, tena sana.

Sasa hili Mhe. Mwenyekiti, vile vile ni la Kaimu Waziri wa Fedha. Kwa sababu hili liko nje ya Bajeti ya Wizara naomba sana Serikali tuondoke na *pool* yetu, waandishi wa habari wa Redio na Televisheni tunakwenda zetu Dodoma tena muanze kuwakodia nyumba mapema maana karibu zitajaa. Wakae pale waje wachukue kumbukumbu.

Mhe. Mwenyekiti, hili suala linalokwenda kufanywa Dodoma sio suala dogo, ni suala kubwa. Tunakwenda kutengeneza misingi ya nchi kwa miaka 50 na 100 inayokuja lazima tuwe na kumbukumbu zetu. Kwa hiyo hili nilikuwa naomba sana Mhe. Kaimu Waziri wa Fedha yupo lazima atutengenezee utaratibu waondoke na *pack.*

Kwanza Serikali inadaiwa pesa nyingi sana na hii Wizara ya Habari hasa Baraza la Wawakilishi. Kwa sababu hawa wanapokuja hapa sisi matangazo ya humu ndani ya Baraza la Wawakilishi ni haki ya Baraza la Wawakilishi, lakini Baraza haliwalipi. Na kwa sababu katika Bajeti ya Baraza haimo, kwa hiyo bajeti hii bado inatakiwa ibebwe na Kaimu Waziri wa Fedha. Kwa hiyo Mhe. Kaimu Waziri wa Fedha hapa kuna mambo matatu yote unatakiwa uyabebe ili wenzetu hawa tuweze kuwalipa vizuri. Tutamlaumu bure Mhe. Waziri kwa sababu yeye anafanya kazi, lakini hii kazi anayofanya ni kazi ya Baraza la Wawakilishi.

Wenzetu Bunge la Kenya Mhe. Mwenyekiti, hakuna chombo chochote cha habari kinachoruhusiwa kutoa matangazo ya Bunge la Kenya mpaka upate kibali. Sasa leo hawa hizi habari ni mali yetu, sisi tumo Barazani tumeshamfukuza mwandishi wa habari asiingie wala asiripoti taarifa zetu kipindi hicho tulipokuwepo Kikwajuni kule. Alituletea manyago huku watu wanazungumza vyengine karipoti vyengine, tukampiga hapa tukamwambia usije na hakuja mpaka leo. Kwa hiyo hizi habari ni haki ya Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo Mhe. Kaimu Waziri wa Fedha andaa mkoba mzuri safari hii umkabidhi Mhe. Waziri wa Habari aondoke na *pack* yake anakwenda nayo Bungeni kule Dodoma.

Sasa la mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka nizungumze suala ambalo limezungumzwa na Wawakilishi wengi. Mhe. Panya Ali Abdalla kazungumza vizuri sana sasa hivi kwamba tunapoambiwa jambo tufanye utafiti. Mhe.Mwenyekiti, Kamati yangu baada ya kupata malalamiko ya wananchi wa Nyanjale, mimi nilitoka na Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa tukaenda mpaka Nyanjale.

Baada ya kufika kule Mhe. Mwenyekiti, kwanza kitu ambacho nilichoamua kwa sababu tulipata mambo mawili, kwanza kulitokezea uharibifu mkubwa wa mazingira wa ukataji wa miti, lakini la pili kuna wananchi ambao walikuwa wanatumia eneo la bandari pale, lakini vile vile wanaanika madagaa ikabidi lazima twende tukaangalie hali halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kitu ambacho nataka nikwambie kwamba kwa upande wa mazingira kweli kuna minazi imekatwa, lakini ile minazi tayari mingi yao kama utaratibu wa kawaida ilikuwa imeshazeeka. Lakini lile eneo vile vile ni eneo ambalo tayari mwekezaji alikwisha kupewa na anataka kuweka mradi mkubwa sana. Katika utalii wetu wa Zanzibar siku zote tunalalamika tunasema watalii wengi wanakuja fedha ndogo. Lakini je, watalii wa aina gani tunaopokea. Wale wanajenga uwanja wa gofu, watalii wa gofu ni watalii wakubwa sana, wanatumia fedha nyingi, ni matajiri wakubwa sana. Ukiwa na uwanja wa gofu utalii unaongezeka maradufu na watalii wanaokuja ni wale wenye pesa zao.

Mhe. Mwenyekiti, leo mradi ule mwekezaji yule sisi tumekaa tukamuuliza akatuonesha mikataba ambayo walikaa na Kamati ya Wanakijiji wa Nyanjale kwa makubaliano tena wakatia saini. Kwamba kwanza ile bandari wataendelea kuitumia hawajakatazwa, ili boti zao zinaporudi kwenye uvuvi wanakuja wanaziweka pale. Pale kitu kilichoondolewa ule uanikaji wa dagaa kwenye ile fukwe, na yule mwekezaji amekubali kuwahamisha katika eneo lile akawahamishia kwa juu. Kama alivyosema Mhe. Panya Ali Abdalla amewajengea vyoo, amewawekea maji, amewajengea ule uwanja wa kuanikia dagaa, amewapa mpaka na gari ya kubebea lile dagaa watakapoondoka pale chini kwenda juu. Wawekezaji kama hawa ndio tunaowataka ambao wanakaa na wananchi wanakubaliana tena kwa maandishi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, leo unajua katika maeneo kama yale lazima kila mtu atakuwa na lake, huyu atasema hivi, lakini shilingi ina pande mbili. Kwa hiyo jambo lolote unaliangalia mizania yake, jambo gani litaleta faida zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, yule mwekezaji sio kama kaziba njia, amewatolea njia nyengine ambayo watafikia mpaka kule juu. Lakini zile shughuli zinazofanyika kule baharini Mhe. Mwenyekiti, sio kama zile shughuli

zinafanyika kule kutwa nzima, lile ni suala la kuanika dagaa tu, kuanika dagaa tayari wameshapewa eneo jengine na gari wamepewa. Lakini kuna jengine ambalo liko nje ya makubaliano tukawaambia wale wawekezaji, pale kuna kazi nyengine ndogo ndogo zitakazotokezea ambazo zilizokuwa hasa si za kitaalamu. Bado waendelee kutoa *incentives* kwa wale wananchi wa Nyanjale waweze kutoa ajira pale mradi ule utapoanza na wamekubali hilo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana na nawaomba sana watu wa Nyanjale hata mimi juzi niliwasikia kwenye Mawio lakini kwa kweli yule mwekezaji amefanya kazi kubwa, na kwa kuwa amekaa na wananchi na saini zao wametia. Lakini sasa kama hivyo ninavyosema katika mambo haya kuna wengine watakuwa wanapendelea, wengine hawapendelei, sasa kuna watu wameshawishiwa nasikia ile Kamati pia wameamua kuivunja. Lakini Kamati utaivunja vipi wakati ile Kamati ndio iliyoanza mazungumzo na tayari wameshakubaliana. Ina maana kama Kamati imevunjwa na yale makubaliano na ile gari pia wanaikataa, na lile eneo pia wanalikataa.

Mimi nitashangaa sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kule baharini sio kama wale watu wanakwenda kushinda kutwa nzima, pale ni sehemu ya kuanika dagaa, tena hii sehemu ya juu ndio wamerahisishiwa hata kwa wale wateja wao wanaokwenda kununua dagaa, au vile vile kwa wale wateja wengine ambao wanakuja kununua dagaa kupeleka sehemu nyengine. Mimi naomba sana wananchi wetu tuwasaidie zaidi kuliko labda kuwapotosha.

Mhe. Mwenyekiti, kweli wapo wawekezaji ambao kwa kweli wanakuwa wanawanyanyasa, wanawafungia njia wananchi wasipite na hawakai nao kwa mashauri ya aina yoyote, na wananchi wanakuwa hawafaidiki kwa jambo lolote. Mimi nadhani hawa lazima tuendelee kuwashughulikia. Lakini hawa wanaokubali kukaa na wananchi wakazungumza nao mimi nafikiri tuwaunge mkono kwa sababu huu utalii ndio sehemu ambayo inayotupatia fedha. Leo uchumi wetu asilimia kubwa unategemea zaidi utalii.

Mhe. Mwenyekiti, ingawa ulisema kwamba utampa Mhe. Naibu Waziri wa Habari atoe maelezo machache, lakini kuna mambo mazito Mhe. Kaimu Waziri wa Fedha ni vizuri basi na yeye ungelimpa nafasi kidogo angalau akawekaweka sawa. Kwa sababu kuna mambo mazito ambayo tunahitaji taarifa zetu ziweze kupokelewa, ziweze kuchukuliwa ziwekwe katika rekodi pale Redio Zanzibar na Televisheni Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii, naona Mheshimiwa anaurusha rusha mpira lakini naomba bado atupe maelezo. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kama hili la posho la hawa Mhe. Waziri utambana bure, hii kazi

anaifanyia Baraza, kwa hivyo hii keki bado Mhe. Kaimu Waziri wa Fedha, fedha azitoe awape hawa ili waweze kulipwa.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono ripoti ya Mwenyekiti, lakini vile vile na Mhe. Waziri naomba haya mambo mengine watusaidie ufafanuzi. Nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kutoa ufafanuzi mdogo kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wawakilishi wamechangia mambo mbali mbali yanayohusiana na Wizara yetu. Nataka nitoe maelezo kidogo yanayohusiana na Wizara kwanza nianze kwenye *ZBC TV*.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niwahakikishie Wajumbe kwanza Mhe. Hija Hassan Hija amesema king'amuzi chetu hakionekani Pemba na Mheshimiwa wa Jimbo la Chambani. Nataka niwahakikishie kwamba mimi nikiwa Naibu Waziri wa Habari tangu tarehe 25 niko Pemba nimetembelea Kusini Pemba na Kaskazini Pemba. Micheweni king'amuzi chetu kinaonesha vizuri na redio pia inatoa vizuri. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wawakilishi tujue kwamba Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo inafanya kazi vizuri.

Sababu ya kusema hivyo nawahakikishia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na namhakikishia Mhe. Hija Hassan Hija kuwa nilikuwepo Kusini Pemba na nilikuwepo kwenye jimbo lake na nililala na king'amuzi kile kikawa kinaonesha vizuri. Na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanapochangia anaonekana mmoja mmoja na sauti zake. Nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kama kuna mtu aliyemwambia hivyo mimi nakataa kabisa, kwa sababu hakika ninayo na mimi nilikuwepo Pemba nimerudi jana.

Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni kuhusu miti iliyopandwa Redio Jamii. Mhe. Subeit Khamis Faki kwa kweli mimi nikiwa ni Mwakilishi wa Viti Maalum Mkoa wa Kaskazini Pemba na nikiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Vijana nimetembelea Redio Jamii miti iko wewe ingawaje unasema kama miti imekufa kwa jua, miti iko na inatiliwa maji.

Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni amezungumzia kuhusu ngoma za asili. Mhe. Mwenyekiti, kama unavyojua sasa hivi kwenye maeneo yetu mengi tumeingiliwa na mambo ya dini. Ukiwa wewe Mwakilishi wa Jimbo lile la Micheweni na mimi nikiwa ni Mwakilishi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba naishi kwenye Jimbo la Micheweni, nakuomba Mhe. Mwakilishi

tushirikiane baina ya mimi na wewe ili tuendeleze ngoma zetu za asili na mila na desturi.

Mhe. Mwenyekiti, niende kuhusu Redio Jamii ambazo zipo kwenye mikoa yetu ya Unguja na Pemba. Mhe. Salma Mohammed Ali ameeleza kuwa Redio Jamii na Pemba inatakiwa iwepo. Nataka nimhakikishie Mhe. Salma kwamba sasa hivi taratibu zote za Redio Jamii Mkoani zimefikia pahali pazuri. Na Mhe. Salma ukiwa ni Mwakilishi wa Mkoa wa Kusini, Wilaya ya Chake Chake nakuomba sana kwa sababu nataka nikwambie Redio Jamii ni jamii wenyewe. Sasa nakuomba ushirikiane na jamii ili kuiendeleza Redio Jamii.

Mhe. Hassan Hamad Omar wa Jimbo la Kojani ametupa pongezi nyingi za kuhusu Tamasha la Kizanzibari. Nataka nimwambie Mhe. Hassan kwamba mwaka jana kulikuwa na tamasha Mangapwani na mgeni rasmi alikuwa ni Mhe. Mzee Ali Hassan Mwinyi. Nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba yule ni mlezi kwenye tamasha lile na ni muasilia wa utamaduni wa Kizanzibari Mangapwani. Nakuomba Mhe. Mwakilishi ingawaje umetupa pongezi za shere, lakini nakwambia kwamba wewe ukiwa ni Mwakilishi wa Kojani, unajua mila na desturi za Kojani uweze kusimama kidete kwa kushirikiana na Wizara kufanya utafiti mwanzo ndipo twende tukafanye tamasha Kojani.

Mhe. Mwakilishi nakuomba sana ushirikiane na Wizara ya Habari, na kwa kweli nakuahidi kwamba tutashirikiana pamoja na wewe. Lakini tunakuomba wewe una kipaumbele zaidi kwa sababu kama unavyojua Kojani kuna mila na desturi za Kizanzibari ambazo sisi wenyewe hatuwezi kuzifikia, ufikie wewe mwenyewe mwanzo ndipo na sisi tuweze kufika.

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote wamezungumzia kuhusu matatizo ya waandishi wetu wa habari ambao wanaingia kwenye Baraza hili tukufu. Nataka niwaambie kwamba kipindi kilichopita tulifuatilia na tukawalipa. Lakini nataka niwaambie shirika sasa hivi ni changa, muwe na ustahamilivu Waheshimiwa. Na nawaomba wafanyakazi wetu wa Wizara ya Habari muwe wastahamilivu kwa sababu jambo hili mngelileta kwangu nikiwa Naibu Waziri wenu msingelifikisha kwa Waheshimiwa ili kuweza kulizungumza hapa, kwanza mngekuja kwangu mimi mkanambia Mheshimiwa umechukua hatua gani, lakini nataka niwahakikishie hatua nimeshazichukua na mtalipwa pesa zenu. Nawaomba sana muwe pamoja na Wizara, wafanyakazi wetu wa Wizara yetu ya Habari muwe pamoja na sisi kwa mashirikiano mazuri. Pale panapotokea jambo lolote lile huwezi ukalipeleka juu mwanzo, lilete chini halafu ndio litakwenda juu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ufafanuzi huu.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Naibu Waziri kwa maelezo yako mazuri sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora: (Kaimu Waziri wa Fedha): Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kupata wasaa huu kuzungumza machache sana kwa niaba ya Waziri wa Fedha hasa kuhusu hoja iliyoulizwa na Wajumbe juu ya madeni ambayo wafanyakazi wa Shirika la *ZBC* wanaidai. Kwanza naomba nifahamishe tu kwamba *ZBC* ni shirika na wao wanapaswa kuendesha mambo yao kibiashara. Sasa hili Mhe. Waziri labda atalieleza kwa ufasaha matatizo na mafanikio yaliyopo, lakini kama Wizara ya Fedha na kuhusu hasa chombo chetu cha Baraza, hapa ninafikiri kama serikali tuingie kati tuone kwamba kama kuna deni shirika linaidai serikali hasa upande wa Baraza tuone hili basi tunakaa chini kwa pamoja tunalimaliza vipi.

Sasa mimi ninamuomba sana Mhe. Waziri tukimaliza tu pengine leo hivi, basi hata Jumatatu tukae kwa pamoja tuweze kuona tunaweza tukalifanikisha vipi hasa madeni ya hawa vijana wetu wanaodai.

Lakini jengine hili la Dodoma ni wazo zuri. Ni kweli kama Wawakilishi wote tunakwenda kule na kazi nzuri wanayoifanya hapa inapaswa na kule nayo ionekane. Kwa hivyo ni jambo tukaa nalo tuweze kuona tunalifanikisha vipi.

Sasa hili naomba pia nilichukue kama Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, tukae pamoja tuone tunalifanikisha vipi hilo suala. Ni suala muhimu na kweli lazima Waheshimiwa Wawakilishi waonekane kule nao wanachangia mstakabali wa nchi yetu katika Katiba hii mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa ninaomba nichukue ahadi hizo mbili, tutakaa pamoja na Waziri wa Fedha tuone tunafanikisha vipi masuala haya mawili. Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru. Mhe.Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba sasa nitoe majumuisho kutokana na michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kuchangia hotuba ya Kamati ya Mifugo, Utalii na Habari kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Allah kwa kutukutanisha kwa mara nyengine tukiwa katika hali ya uzima wa afya, lakini pili napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi pamoja na Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango yenu.

Michango yote iliyotolewa ilikuwa na nia njema, nia ya kusaidia mimi binafsi lakini pamoja na watendaji wa wizara yangu katika kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi na kufikia malengo tuliyojiwekea.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu sasa nitoe shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Mifugo, Utalii na Habari ya Baraza la Wawakilishi chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Mlinde Mabrouk Juma kwa ushauri nasaha na maelekezo waliyotoa katika kuielekeza wizara yangu ili kufikia malengo ya kuwahudumia wafugaji, wavuvi na wakulima wa mwani. Wizara yangu itafuata maelekezo ya kamati kwa kadri Mwenyezi Mungu atakapotupa uwezo huo.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba hii imechangiwa na jumla ya Wajumbe 14 pamoja na 3 kwa maandishi kuhusiana na wizara yangu. Naomba uniruhusu niwataje kwanza wale wote waliochangia hotuba hii, waliochangia moja kwa moja ambao ni kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Hassan Hamad Omar
3. Mhe. Salma Mohammed Ali
4. Mhe. Nassor Seif Salum
5. Mhe. Asha Bakari Makame
6. Mhe. Subeit Khamis Faki
7. Mhe. Mussa Ali Hassan
8. Mhe. Saleh Nassor Juma
9. Mhe. Rufai Said Rufai
10. Mhe. Hija Hassan Hija
11. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
12. Mhe. Mohamed Mbwana Hamad
13. Mhe. Panya Ali Abdalla
14. Mhe. Hamza Hassan Juma

UTARATIBU

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, wakati anataja jina amesema kwamba Mhe. Nassor Seif Salum na mimi jina la Seif katika ukoo wangu hamna, kwa hivyo naomba aweke sawa jina langu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri naomba ufanye marekebisho.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba samahani, ni kweli ninafikiri watendaji walikosea jina. Kwa ufupi Mhe. Nassor Salim Ali (Al -Jazira).

Na Mjumbe wa mwisho ambaye ni wa 15 aliyechangia kwa maandishi ni:-
Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii tena kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba michango, maelekezo, maoni, ushauri na mapendekezo waliyotupa tumeyapokea na tutayafanyia kazi ipasavyo, kwani yatatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ili kukidhi matakwa ya wadau wote wa sekta hii ya mifugo na uvuvi hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nichukue fursa hii ili kutoa ufafanuzi wa baadhi wa hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe pamoja na kuwasilisha majibu kwa hoja zilizotolewa kama ifuatavyo.

Mjumbe wa kwanza alikuwa Mhe. Mlinde Mabrouk Juma ambaye ni Mwenyekiti wa kamati hii kwamba, hoja yake ilikuwepo kwa maradhi ya ndui kwa kuku waliochanjwa dhidi ya maradhi ya mahepe. Jawabu ni kwamba wizara yangu inatambua kwa tatizo hilo na inaendelea kufanya uchunguzi juu ya suala hilo.

Hivyo wizara yangu itazidi kuendelea kutoa taaluma juu ya matumizi bora ya chanjo zote za mahepe na ndui ili ufugaji uzidi kuwa wa tija. Hoja yake ya pili uvamizi wa shamba la Pangeni na kutowepo kwa hatimiliki ya shamba hilo.

Mhe. Mwenyekiti, shamba la Pangeni linamilikiwa na serikali tokea mwaka 1951 na tuna hakika hati yake ipo na tumejaribu kuifuatilia *archives* lakini haijapatikana. Shamba la Pangeni limekwisha kupimwa tena kwa kufuata ramani asilia kwa matayarisho ya kuomba hatimiliki. Watu wanaovamia maeneo yote nao hawana hati ya aina yoyote lakini inaonekana uongozi wa Wilaya ya Kaskazini ya B na Mkoa kwa jumla inawatetea wavamizi.

Wizara imefanya vikao na viongozi hao na lengo letu hivi sasa ni kuitumia Kamati yetu ya Baraza la Wawakilishi tukae kwa pamoja na viongozi hao kulipatia ufumbuzi wa kudumu suala hili.

Hoja yake ya tatu visiwa vidogo vidogo vya wavuvi, wanasema vinauzwa wao hawapati tija yoyote, hawapati kuweka dago. Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu haina taarifa juu ya kisiwa chochote kilichouzwa visiwa vidogo vidogo viliomo ndani ya maeneo ya hifadhi, vimo ndani ya utaratibu kamili wa sheria za maeneo ya hifadhi na wizara haijapata taarifa yoyote kuhusu wavuvi kuzuiliwa kwenda dago.

Aidha, wavuvi hupatiwa hata msaada na wawekezaji pale ambapo wanapotokezewa na dharura yoyote. Hoja yake nyengine wataalamu wa mifugo kutowatembelea wafugaji badala yake wafugaji huwafuata wataalamu vituoni. Mhe. Mwenyekiti, wizara inajitahidi sana kutoa huduma za elimu juu ya ufugaji na utibabu.

Suala la wafugaji kuwafuata wataalamu vituoni ni ishara ya wao kujua umuhimu wa utaalamu baada ya kuwaelimisha. Sababu kubwa inayofanya ziara ya wataalamu wetu wafugaji kuwa wachache ni ukosefu wa wataalamu wa kutosha na vitendea kazi vikiwemo vyombo vya usafiri pamoja na mafuta. Wizara inajitahidi kutafuta vyanzo vyengine vya fedha ili kuweza kuwafikia wafugaji na kutoa huduma za mifugo.

Wizara ihakikishe utayarishaji wa *business plan* ili uvuvi wa bahari kuu uwe endelevu. Mhe. Mwenyekiti, suala la utayarishaji wa *business plan* unahitaji ushauri wa kitaalamu hasa katika masuala ya biashara. Hivyo wizara imeanza kuchukua hatua ya kuwasiliana na wataalamu ili kupata ushauri. Watendaji wa serikali watatembelea nchi mbali mbali zinavyotengeneza vyombo kama hivyo vya uvuvi wakati ili kupata uzoefu wa nchi hizo katika kuendeleza uvuvi huo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk naye alikuja na hoja zake, tuendeleze taaluma za ufugaji wa samaki baharini kwa kutumia uzio. Mhe. Mwenyekiti, taaluma ya ufugaji samaki baharini kwa kutumia vizimba tayari imeshatolewa kwa wajasiriamali wa mazao ya baharini. Wizara yangu itaendelea kutoa tu taaluma hiyo kwa wajasiriamali hao. Kwa sasa wananchi wamejitokeza na kuhamasika na ufugaji wa majongoo na kaa katika vizimba. Mfano Wambaa na Mtambwe Kaskazini Pemba na kwa upande wa Unguja ni Nyamanzi, Bweleo na Fukuchani.

Hivyo wizara yangu itaendelea kutoa taaluma ya ufugaji samaki baharini ili kuongeza lishe na maslahi ya kiuchumi. Hoja yake nyengine wafugaji wadogo wadogo wawezeshwe kitaaluma kabla ya kupatiwa mifugo. Wizara itaendelea kutoa huduma za elimu kwa wafugaji kupitia mashamba, darasa ya mifugo, vikundi vya mfugaji mmoja mmoja.

Halikadhalika Mhe. Hassan Hamad Omar naye alikuwa na hoja zake. Wavuvi wanakamatwa ovyo pamoja na wavuvi wa Chwaka kutupiwa vifaa vyao baada ya kuachiwa Mahakama. Mhe. Mwenyekiti, suala la wavuvi wa Chwaka waliokamatwa na kuachiwa na Mahakama, vifaa vyao vyote vilipelekwa kwa Msajili ili wapatiwe wenyewe.

Aidha suala la wavuvi kukamatwa ovyo halipo, kwani wanapokamatwa hupelekwa kwenye vyombo vya dola na kufuata utaratibu kamili wa sheria ambayo imepitishwa na wavuvi wenyewe, serikali na hatimaye hapa Baraza la Wawakilishi.

Hoja yake nyengine wavuvi bado hawana hatimiliki za madiko na baadhi ya wawekezaji wanafunga njia kwa wavuvi kuelekea kwenye madiko yao. Mfano Kiombamvua. Wizara ina hatimiliki ya baadhi ya madiko na inaendelea na kutafuta hatimiliki kwa madiko yaliyobakia.

Hoja yake nyengine uvuvi haramu upi na halali ni upi. Wizara yangu hivi sasa imeandaa muongozo wa kuwafikia viongozi na wananchi juu ya uvuvi haramu na matatizo yake na upi uvuvi halali na faida zake. Muongozo huo tayari umepitishwa na serikali na hivi sasa upo katika matayarisho ya uchapishaji na ninaamini kwamba utakapotolewa utaondosha utata wote ambao unaonekana kwa viongozi na wananchi. Hapa Mhe. Mwenyekiti, ningetoa ufafanuzi kidogo kwa Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kojani Mhe. Hamad ambaye amesema kwamba uvuvi haramu na wa halali ni upi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ninafikiri kuna masuala mengine si ya kutoa hoja kwa sababu hili suala ni la sheria, na sheria ambayo imepitishwa hapa hapa na Wajumbe wakaipitisha. Sasa anaponyanyuka Mjumbe kusema kwamba uvuvi haramu upi na halali upi, kwa kweli ninashangaa sana. Hata kama wewe labda ilipopitishwa sheria ilikuwa hupo lakini wajibu wako ni kuiheshimu ile sheria, kwa sababu imepitishwa katika chombo hichi.

Halafu hakuna sheria ambayo haiwezi kubadilika isipokuwa Msahafu tu (Quran) ndio hauwezi kubadilika lakini sheria zote tumeziunda sisi binadamu ni sheria ambazo zipo na zinaweza zikabadilika wakati wowote. Kwa hivyo Mjumbe yeyote akihisi kwamba labda kuna kipengele chochote cha sheria ambacho labda hajakielewa au kinamtatiza, milango iwazi aje ofisini atueleze ni kifungu gani ambacho kina matatizo, tunaweza tukakaa tukajadili na tukihisi kwamba kuna haja ya kubadilisha, tutabadilisha.

Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe kama kuna tatizo lolote, tusizue mambo ambayo tumepitisha hapa hapa, kama kuna kitu ambacho hakijafahamika basi acha Mjumbe aje tufahamishane na kama kuna haja ya kubadilisha tutabadilisha. Ahsante.

Nikiendelea kuhusu uvuvi huo huo wa haramu na upi wa halali. Kama nilivyoeleza ni kwamba sheria imeeleza kila kitu, upi haramu na upi ni halali.
Mhe. Salma Mohammed Ali naye alikuwa na hoja zake. Sheria ya kudhibiti maliasili ya mifugo ifanyiwe marekebisho ili kudhibiti wafugaji wakaidi na

kuchanja mifugo yao wachukuliwe hatua. Mhe. Mwenyekiti, sheria hii inaendelea na mchakato wa kuifanyia marekebisho. Hoja yake ya pili ni hatua gani zimechukuliwa kudhibiti mbwa wasiokuwa na wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, wizara inaendelea kutoa taaluma kwa wafugaji wa mbwa, wafuge idadi wanayoimudu kuihudumia kwa chakula na malazi. Vile vile inatoa huduma za matibabu, chanjo na kufunga uzazi kwa mbwa. Taaluma itazidi kutolewa maskulini ili kuhamasisha jamii juu ya kujikinga na magonjwa ya mifugo hasa kichaa cha mbwa.

Hoja nyengine kuna tatizo gani cha chanjo kwani ikitokea ugonjwa hupata wanaochanja na wasiochanja. Mhe. Mwenyekiti, wizara itazidi kutoa taaluma juu ya umuhimu wa kutumia dawa za chanjo na umuhimu wa kuzitumia.

Mjumbe mwengine ni Mhe. Nassor Salim Ali, hoja yake ni kuhusu wafugaji wawezeshwe ili kupatiwa ng'ombe wa maziwa kukidhi mahitaji ya kiwanda kipya cha maziwa kilichoanzishwa. Ni Kiwanda cha Bakhressa ninatumai. Mhe. Mwenyekiti, wizara imeweka utaratibu wa kuwatembelea wafugaji na vikundi vyao kwa madhumuni ya kuwaeleza umuhimu wa fursa hii ya kuitumia ya kukitumia kiwanda hichi cha kisasa cha maziwa.

Vile vile wizara baada ya kuona fursa hii ya soko la maziwa inashirikiana na Shirika la *Help Project International*, kuona ni jinsi gani wataweza kuwasaidia wafugaji wadogo wadogo waliopo na vile vile kuibua wafugaji wapya ili kukidhi mahitaji ya kiwanda kilichoanzishwa.

Mhe. Asha Bakari Makame naye alikuja na hoja yake, kabla ya kuanzisha miradi ya uwekezaji ni bora kuihusisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kuondoa usumbufu kwa wavuvi. Mhe. Mwenyekiti, ushauri huu ni mzuri.

Vile vile Mhe. Subeit Khamis Faki na Mhe. Mussa Ali Hassan nao walikuja na hoja kwa nini wavuvi hawawezeshwi ili kuvua uvuvi wa kileo na wa kisasa. Mhe. Mwenyekiti, suala hili litapatiwa ufumbuzi baada ya kukamilika *business plan* ya uvuvi wa bahari kuu. Kama nilivyoeleza awali kwamba ni suala la kitaalamu. Kwa hivyo tumo katika *process* hiyo ya kutengeneza *feasibility study* ili kuona nini cha kufanya.

Mhe. Panya Ali Abdalla naye alikuwa na hoja yake kuhusu shamba la Kipange limevamiwa. Mhe. Mwenyekiti, shamba la Kipange halikuvamiwa. Mwaka 2003 alipewa mwekezaji mzalendo kampuni ya mifugo ya *care*. Naye mfugaji huyu ameliendeleza vizuri sana. Wakati lilipokuwa chini ya serikali shamba hili lilikuwa na ng'ombe 7 na wafanyakazi 14.

Hivi sasa pana ngo'mbe 32 wa maziwa na limeajiri wafanyakazi 4 wa kudumu na 6 wa *daily paid*, yaani ya kutwa. Shamba hili linazalisha maziwa mengi na kuzalisha ndama 11 kwa wastani kwa mwaka. Mwekezaji kajenga mabanda, kachimba kisima na anafuga mbuzi wa kisasa wa maziwa. Shamba limeendelezwa vizuri mno.

Mhe. Mohamed Mbwana naye alikuwa na hoja zake, wafugaji wa samaki wawezeshwe na wapewe elimu. Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inawawezesha wafugaji wa samaki kwa kuwapa elimu ya ufugaji bora na kuwasaidia vifaa kama vile *pump* za kuvutia maji katika mabwawa ya samaki. Jumla ya watu 59 kutoka Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo ya ufugaji wa samaki nchini China akiwemo mfugaji wa samaki kutoka Chambani.

Aidha, wafugaji wa samaki na viongozi mbali mbali ambapo elimu na taaluma ya ufugaji bora wa samaki itatolewa.

Mhe. Mwenyekiti, huo ulikuwa ni ufafanuzi kwa hoja ambazo zimetolewa kwa Waheshimiwa Wajumbe. Naomba kuwasilisha. Ahsante. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kunipa nafasi hii ya kueleza machache kuhusiana na hoja nyingi za Waheshimiwa Wajumbe kuhusiana na ripoti ya Kamati yetu.

Lakini kwanza niruhusu kumshukuru sana na kumpongeza Mhe. Mlinde Mabrouk Juma; Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Habari na Uvuvi, kama alivyosema mwenyewe kwa namna ambavyo anashirikiana na wenzake katika kamati na kuisaidia sana wizara yangu.

Kama nilivyosema asubuhi ziara zao za mara kwa mara na wakati mwengine wanakuja tu kwa sababu wamesikia jambo wizarani, kwa kweli tunapata kushauriana na kwa kweli wanaisaidia sana wizara, ninawashukuru sana na ninawaombe waendelee na mwenendo huo, kwa sababu kwa kupitia njia hiyo ambayo ni ya Kikatiba, Kisheria na Kikanuni, ndio ambavyo wanaweza kunisaidia mimi kama msimamizi mkuu wa wizara katika kufanya mambo na kufanya ufanisi kwenye wizara yetu ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati yetu imechangiwa na Wajumbe wanaofika 20 ambao ni:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Hassan Hamad Omar

3. Mhe. Salma Mohammed Ali
4. Mhe. Nassor Salim Ali
5. Mhe. Asha Bakari Makame
6. Mhe. Subeit Khamis Faki
7. Mhe. Mussa Ali Hassan
8. Mhe. Saleh Nassor Juma
9. Mhe. Rufai Said Rufai
10. Mhe. Hija Hassan Hija
11. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
12. Mhe. Mohamed Mbwana Hamad
13. Mhe. Panya Ali Abdalla

Wengine waliochangia kwa maandishi ni:-

14. Mhe. Farida Amour Mohammed
15. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman
16. Mhe. Mgeni Hassan Juma
17. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
18. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
19. Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi
20. Mhe. Hamza Hassan Juma

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninawashukuru Wajumbe wote waliochangia. Kwa kweli michango yao yote ilikuwa ni michango mizuri sana yenye kujenga. Ninaamini mimi na watendaji wangu michango ambayo wametoa Waheshimiwa Wajumbe itatusaidia sana katika kusimamia mambo pale wizarani na kuhakikisha kwamba kasoro ambazo zimetajwa ziliomo ndani ya wizara yangu, basi zinapata nafasi ya kuondolewa.

Mambo makubwa ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe ni jengo la redio ya zamani, *ZBC* kwa jumla, kulipwa posho waandishi wa habari na nyongeza ya mishahara, redio ya jamii lakini zaidi Mtegani. Wamezungumzia pia suala la *Z-MUX* pia na *AGAPE*, viwanja vya Amani na Gombani, studio ya redio kutumika kama afisi ya magazeti na mwisho suala la utalii na ulinzi. Haya ndio mambo makubwa ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe lakini kuna na mengine madogo madogo ambayo pia nitayatolea ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ambaye kama nilivyosema mbali ya kuwa ni Mwakilishi wa Jimbo la Kitope lakini ni Makamu wa Rais wa Zanzibar anayeshughulikia na riadha taifa. Ninamshukuru sana kwa mchango wake, lakini amezungumza suala ambalo

limezungumzwa na watu wengi, suala la waandishi wa habari na zaidi wanaofanya kazi hapa Barazani kwamba hawajalipwa.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba waandishi ambao wanaofanya kazi hapa Barazani, hawa wanalipwa mshahara na wizara yangu kupitia Shirika la *ZBC* ndio waajiri wao. Kwa hivyo wanalipwa mshahara na Shirika la *ZBC*. Hivyo kazi yao wanayoifanya tunawalipa mshahara.

Hivi sasa wanaingia kwa *shift* hapa. Kuna wengine wanaingia asubuhi wanafanya kazi masaa matatu manne baadae wanaondoka. Kwa hivyo wanapata mshahara kwa kazi yao ile ya usiku na wengine wanakuja jioni na masaa matatu manne, halafu wanaondoka. Kwa hivyo wanapata mshahara pia kwa kazi yao hiyo.

Kwa hivyo hawa ni wafanyakazi wa serikali ambao wanalipwa mshahara. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu wanafanya kazi katika Baraza la Wawakilishi tumefanya mazoea ya kuwalipa posho, ni jambo zuri. Wakati ninapitisha bajeti ya mwaka 2012/2013, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walilizungumza hili kwa hamasa kubwa. Na moja jambo nilitakiwa niongeze posho la wafanyakazi hawa kutoka shilingi elfu tano kuendelea zaidi.

Jibu nililojibu ni kwamba lile ni shirika Mhe. Mwenyekiti, na kwa hivyo lazima bodi ya shirika iidhinishe hizi nyongeza. Sasa nilizindua bodi mwezi wa Oktoba. Wakati ninazindua niliwapa jukumu hili bodi kwamba tuna agizo la Baraza la Wawakilishi tuongeze posho la vijana wanaokwenda Barazani.

Mhe. Mwenyekiti wa Bodi ambaye yeye mwenyewe aliwahi kuwa muandishi na mtangazaji. Ameahidi kwamba kikao cha mwanzo cha bodi kitakachokaa mwezi wa Februari, jambo la mwanzo ni kushughulikia maslahi na *scheme of service* ya wafanyakazi wa shirika lake. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi nisingeweza hata kidogo kuwalipa vijana hawa posho shilingi elfu tano katika kikao kilichopita huku nina agizo la Baraza lako tukufu ambao ninaliheshimu sana kwamba waongezwe posho lao. Kwa hivyo ninaomba sana Mhe. Mwenyekiti, ninajua wanadai kikao kimoja kilichopita na hichi. Lakini ninamuamini sana Mwenyekiti wa bodi ya shirika na wajumbe ambao nimewateua kwamba hili watalisimamia. Kwa hivyo ninajua kwamba wanadai posho la vikao viwili, ninaamini sana kwa huruma ya mwenyekiti, mama mtu mzima ambaye yeye mwenyewe aliwahi kuwa mtangazaji, hili atalisimamia vizuri na ninaamini kwamba *arrears* watakayopata basi ni *arrear* ambayo itakuwa imetononeka. Hilo la kwanza.

Lakini sababu ya pili Mhe. Mwenyekiti, Shirika la *ZBC* ni shirika tulililolipitisha hapa Baraza la Wawakilishi na linatakiwa lijitegemee, lifanye kazi kwa malipo. Mhe. Mwenyekiti, hakuna Bunge lolote katika *Commonwealth* ambalo haligharamii shughuli zake za matangazo. Fanyeni utatifi, nendeni Kenya, Uganda, Tanzania na nje, Mabunge yote yanaweka katika bajeti zao fedha za kutangazia shughuli zao.

Baraza la Wawakilishi Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hija Hassan Hija ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti ya Baraza hili, ni vizuri sana unapofanya bajeti ya Baraza masuala ya namna gani mutalipia gharama za matangazo haya ni muhimu sana. Vyenginevyo mambo mawili; huduma hizi zitakatishwa kwa sababu ya ukwasi wa shirika ambao hautoweza kumudu gharama zake, tutakuwa hatuna *option*. Lakini wananchi kwa sababu wamezoea kumuona Mwakilishi wao wa Kiwani akiwa anaangalia televisheni, anaangalia Mwakilishi analeta vitu vyake. Sasa hatupendelei kabisa kukatisha matangazo haya, ni muhimu mno. Wananchi wanaona namna michango inavyoendelea baina ya serikali na wajumbe wa Baraza lako Mhe. Mwenyekiti. Suala la kulipia ni muhimu.

Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, ili shirika la *ZBC* liwe na uwezo wa kuhudumia wafanyakazi wote, lakini pia kupata uwezo wa kununua vifaa maalum na muhimu kwa shughuli za kazi. Ni lazima Baraza la Wawakilishi sasa lizingatie maoni ya shirika kwamba ni wakati sasa umefika kuona kwamba Baraza la Wawakilishi kama ambavyo Bunge linalipa *TBC*, basi na Baraza la Wawakilishi lilipe *ZBC* katika kuona kwamba huduma hii muhimu sana inafikia wananchi wetu katika maeneo yote ya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Kaimu Waziri wa Fedha, hili jambo ni muhimu kwa vijana wetu hawa kupata huduma, mimi huwa nazungumza na Mhe. Naibu Waziri na nimempa jukumu la kusimamia. Suala hili Mhe. Mwenyekiti, tutalisimamia iwezekanavyo, lakini ni muhimu sana ofisi yake tuone ni namna gani tutashirikiana. Sio vibaya kwetu sisi kama shirika hatuna tatizo, pia kama mtawachukua katika orodha ambao wanalipwa posho kama watu wengine.

Jambo hili hatuoni kama ni baya na linawezekana na ni mazungumzo tu baina ya shirika na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, ili kuona ni namna gani wafanyakazi hawa ambao ni waandishi wanaokuja hapa namna gani watapata malipo yao. Mhe. Mwenyekiti, hilo halina wasi wasi. Suala hili nadhani nitakuwa nimeshajibu hoja za Wajumbe mbali mbali, ambao walizungumza kuhusu malipo ya waandishi wanaokuja hapa Barazani.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makame Mshimba alizungumzia kuhusu ajira katika hoteli za kitalii. Mimi nakubaliana nae, tumeanzisha chuo cha utalii makusudi kwa hilo na tuko pamoja. Kama kampuni yako itasajiliwa rasmi basi tutashirikiana, ili kuona ni kwa namna gani vijana wa Kizanzibari wanapata ajira katika mahoteli, sina tatizo na hilo Mhe. Mwenyekiti.

Kuhusu kurekebisha sheria ili Mwenyekiti wa Baraza la Michezo asichaguliwe na Rais, achaguliwe na wenyeviti. Wacha tulifanyie kazi na baadae tutashirikiana pia na kamati ili tuangalie namna ambavyo tunaweza kulitekeleza hili, na pia wadau wa michezo kulishughulikia hili.

Suala la riadhaa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, yeye ni Makamu wa Rais wa Zanzibar anayeshughulikia riadha. Kwa hivyo, ana nafasi nzuri sana ya kuona namna gani yeye na wizara pamoja na Baraza la Michezo tutashirikiana pamoja katika kuona kwamba riadha Zanzibar imepata nafasi nzuri.

Mhe. Hassan Hamad Omar, Mwakilishi wa Jimbo la Kojani pongezi zake tumezichukua na tumezipokea na tamasha la Kojani tuendelee kushirikiana ili kuona ni kwa namna gani tunaweza kulifanya kabla ya bajeti, tukijaaliwa. Tukienda kwenye Bunge la Katiba tutawaachia watendaji hapa walishughulikie hili, na tukirudi *Inshaallah* tutaangalia namna gani tamasha la wananchi wa Jimbo la Kojani, ambao wana utamaduni mkubwa miongoni mwa tamaduni za Zanzibar, utaweza kuibuliwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salma Mohammed Ali alizungumzia kuhusu televisheni ya Zanzibar. Naomba kwa kupitia hapa nizungumzie *ZBC* ambayo imezungumzwa karibu na Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia. Mhe. Mwenyekiti, *ZBC* ni shirika ambalo lina umri wa mwaka mmoja, tulipitisha sheria hapa mwaka jana, hivi sasa ni shirika changa.

Ni kweli ilikuwa idara, lakini ilikuwa na matatizo mengi. Kwa hivyo, mtoto wa mwaka mmoja hata kusimama vizuri Mhe. Bi Panya aliniambia hajaweza inakuwa ni mtihani kidogo. Kwa hivyo, tusitegemee umri wa mwaka mmoja wa Shirika la *ZBC* kwamba tuweze kupata ufanisi sawa na *TBC* ambayo ina umri mkubwa, *KBC* ya Kenya, *UBC* ya Uganda au *BBC* ya Uingereza nalo ni tangu enzi ya ukoloni.

Hili shirika letu ndio kwanza tunalijenga, kikao hiki kinachokuja cha bodi ndio cha kwanza rasmi ambacho kina mikakati mingi ya kuona ni kwa namna gani tutali-*reform* Shirika la Utangazaji. Kwa hivyo, ni kweli Shirika la Utangazaji la Zanzibar *ZBC* limerithi ule uidara mkubwa, lakini bado halijaondoka liko katika *transition*, yaani liko katika zama za mpito kutoka idara kwenda katika shirika.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, bodi ambayo nimeichagua ina watu mahiri na makini sana na wenye uzoefu mkubwa sana. Kwa hivyo, naamini kwamba tutasaidiana na wizara katika kulifanyia mabadiliko makubwa shirika hili. Yote ambayo yamezungumzwa ni ya ukweli, hivyo tutashirikiana na bodi pamoja na maoni yenu tutayachukua, ili kuona ni namna gani *ZBC* itabadilika.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hivi sasa taarifa yake ya habari sana ina habari za Unguja na kama alivyosema Mhe. Salma Mohammed Ali, ni kwamba kaseti ya shughuli Pemba ni lazima ije kwa ndege, hili ni tatizo ambalo tumeliona.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuondokana na tatizo hili ndio sasa tukasema serikali inawekeza karibu dola milioni moja, kujenga *studio* ya kisasa Unguja pale Karume House na kujenga *studio* ya kisasa Mkoroshoni, ili baada ya ujenzi wa *studio* hizi kuwe na uwezekano wa vifaa vya kisasa ambapo shughuli ikishafanyika Pemba, basi inaweza kuletwa bila ya kutumia tena ndege au meli.

Kwa hivyo, vifaa hivi tayari vimeshanunuliwa kwa awamu ya kwanza, watendaji wangu wananiambia mpaka juzi viko Dar es Salaam. *Studio* hizo kwa Unguja na Pemba zinarekebishwa hivi sasa, ili viweze kufungwa vifaa hivi. Naamini baada ya muda mfupi kumalizika kufungwa vifaa hivi vya *studio* mpya, basi tatizo hili litakuwa limeondoka.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Redio Jamii ya Mkoani. Mhe. Naibu Waziri amelijibu, lakini la msingi ni kwamba tunategemea mpaka wakati wa bajeti tutaliarifu Baraza lako Mhe. Mwenyekiti, wapi tumefikia katika kuanzisha Redio Jamii Mkoani. Tunafanya mazungumzo na *Pemba Press Club* ya Mkoa wa Kusini Pemba, kuona ni namna gani tutashirikiana na ni wapi pazuri katika maombi ambayo yamekuja redio hii itaanzishwa. Kwa hivyo Mhe. Mjumbe usiwe na wasi wasi, hili limo katika hatua za mwisho za kushughulikiwa.

Ni kweli *ZMUX* Mhe. Mwenyekiti, imezungumzwa na hapa nataka nirekebishe kidogo. Taarifa ya mwenyekiti ambae alisema kwamba *AGAPE* ni mwekezaji. Hapana, *AGAPE* sio mwekezaji. Kampuni ya *AGAPE* ni mjenzi, amepewa mikataba miwili. Mkataba mmoja ni ujenzi wa miundombinu ambayo ni mali ya serikali sio mali ya *AGAPE*. La pili, amepewa mkataba wa muda wa miaka miwili ya muda wa uendeshaji. Kwa hivyo, ningependa kuiweka sawa hii ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati. Nadhani makatibu wamenukuu vibaya na kwa hivyo walimuandikia vibaya mwenyekiti.

Nilichotaka kusema Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba hapa tunachofanya ni kuwa Kampuni ya *AGAPE* amepewa mkataba wa ujenzi na kwa kiasi kikubwa kazi hii ameimaliza. Ndio maana akasema Mhe. Naibu Waziri, mtu akiwa Micheweni na akiwa na king'amuzi basi anapata huduma.

Sasa Waheshimiwa Wawakilishi ni vizuri mnapotoa taarifa basi msichukuwe ya kusikia. Hiki chombo ni kikubwa sana, hakihitaji habari za kusikia, kinahitaji uhakika wa unachokizungumza. Kwa hivyo, ni vizuri mwakilishi aseme mwenyewe kwamba mimi nina king'amuzi nyumbani kwangu, lakini sipati au mimi nina televisheni nyumbani kwangu sipati huduma, hilo ndio jambo la msingi.

Lakini usiseme nimepata *message* jamaa anapata msalaba. Aaa! Jamani hiki chombo ni kikubwa. Usichukue taarifa za ajabu ukazileta katika chombo hiki Mhe. Mwenyekiti, sio jambo zuri hata kidogo, kuna *hansard* humu. Sasa unapozungumza mambo ya kusikia ya *record* ya mtu yuko Kiwani keshakula mashelisheli, halafu anakuletea habari hizi hapa inakuwa ni mtihani sana Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, ninasema kwamba tuhakika kuwa miundombinu tayari ipo Kusini Pemba, Kaskazini Pemba, Kusini Unguja, Kaskazini Unguja na Mkoa wa Mjini Magharibi, hivi sasa tunachofanya waandisi wa wizara yetu, wana-*verify* kitu gani kimewekwa na kitu gani hakijawekwa. Lakini kwa ujumla matangazo ukiwa na king'amuzi basi yanapatikana vizuri sana.

Pia *ZBC* hasa kwa Pemba, inapatikana vizuri kuliko hata hapa Unguja. Wale ambao bado wanatumia mfumo wa *analogy,* kwa Pemba wanaipata vizuri zaidi kuliko ambavyo wanaipata hapa Unguja. Kwa nini?

Kwa sababu wataalamu wa ZBC Pemba, wamekichukua king'amuzi halafu wamekiingiza katika *transmitter* ya *analogy*. Kwa hivyo, ZBC wanarusha matangazo kutoka katika king'amuzi ambacho kwa kweli unakipata vizuri sana. Zile chengachenga zote zimekosekana na hata watu wa Gando ambako ni mbali sana basi wanaipata ZBC vizuri sana. Kwa hivyo, suala hili nilitaka niliweke wazi, kwa sababu kama nilivyosema Mhe. Mwakilishili kuzungumza mambo hapa anahitaji awe na uhakika vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu *channel* ni 20. Ni kweli *channel* tulizonazo katika king'amuzi chetu ni 20 kwa hivi sasa na kwa sababu bado tunatumia *analogy* na *digital*. Tutakapofanikiwa kuzima *analogy* hata kesho, basi kutakuwa na uwezo wa kupata *channel* 40. Tatizo letu ni kwamba bado kuna wananchi wetu ambao hawajanunua ving'amuzi na kwa hivyo hatuwezi kuzima hivi sasa.

Lakini tunafanya mashauriano ili tuongeze ving'amuzi zaidi ili ukifika wakati wa bajeti, tutawatangazia wananchi kwamba lini tutazima mitambo ya *analogy*. Hatuwezi kwenda na mitambo ya *analogy* na *digital* kwa muda mrefu kwa sababu ni gharama sana na hivi sasa tumekubaliana kwamba zama hizi ziwe ni zama za *digital*. Kwa hivyo, ni kweli Mhe. Mwenyekiti, *channel* zetu ni 20, lakini tunahakikisha kwamba baada ya muda tukiweza kuzima mitambo ya *analogy* basi zitakuwa *channel* 40 na tukiweza kutumia *transmitter* 2 za *analogy* ziliopo Masingini na Kichungwani tutakuwa na *channel* 60. Kwa hivyo, hilo ndio jambo ambalo tunaweza kufanya, angalau king'amuzi chetu kibebe *channel* 60.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la malipo. Nataka niseme kwamba wakati wa bajeti tuliwatangazia wananchi kwamba tukishaweza kufanikisha kukamilisha miundombinu yote ya Unguja na Pemba, basi tutatoa punguzo la bei kwa muda. Kwa hivyo, nataka niseme kwamba kuanzia tarehe 8 Januari mpaka tarehe 8 Februari, king'amuzi kinauzwa kwa bei ya shilingi 50,000 katika vituo vyetu vya Rahaleo na Mkoroshoni Pemba.

Kwa hivyo, ningewaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, muwanunulie wananchi wenu ving'amuzi wale ambao hawana uwezo na ikifika tarehe 10 Februari, basi ile seli itamaliza na itarudi pale pale kwenye shilingi 73,000. Kwa hivyo, nasema kwamba ile ahadi ambayo tuliitoa hapa katika Baraza la Wawakilishi wakati wa kikao cha bajeti, tulitoa ahadi kwa muda wa wiki moja tu. Lakini sisi tumekwenda nayo kwa muda wa mwezi mzima, ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu ambao hawana uwezo waweze kununua ving'amuzi hivi kwa shilingi 50,000.

Kwa hivyo, nawaomba sana wananchi hasa Pemba ambako tumeuza ving'amuzi kidogo sana, tumeuza ving'amuzi 300 tu na kuna ving'amuzi karibu 700 viko pale vinahitaji wateja. Kwa hivyo, nawaomba sana wananchi popote wanaposikia tangazo hili basi waende wakanunuwe ving'amuzi, ili waweze kupata matangazo yetu bila ya tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la *running track* ya Uwanja wa Gombani, suala hili alilizungumza Mhe. Salma Mohammed Ali. Ni kweli hivi sasa ina matatizo kidogo, na kama juzi nilipokuwa nikimjibu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwamba tunalizingatia na muelekeo wa Wizara yetu ni kwamba badala ya kutia lami, basi tunafikiria pia kutia *tartan* kama tulivyotia hapa Unguja, ili wanariadha wapate nafasi nzuri ya kujifundishia mchezo wa riadha.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Nassor Salim Ali alizungumzia suala la waandishi wa habari na posho, nimeshalizungumza. Kuhusu suala la *studio* ya Rahaleo limezungumzwa na wajumbe wengi hili, kwamba inatumika kwa ngoma.

Kwanza nataka niweke sawa hapa, *studio* ambayo hapa inazungumziwa ni *studio* ya redio ambayo ilijengwa enzi za mkoloni, sio hili jengo jipya la Wachina. Maana baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe hapa walizungumzia kama jengo limejengwa na wafadhili kwa pesa nyingi, leo mmebadilisha matumizi yake. Hapana. Jengo lile lilijengwa toka enzi ya ukoloni na lilikuwa likitumika kwa shughuli mbali mbali, zikiwemo za kurikodia muziki enzi hizo.

Kwa hivyo, serikali ilichofanya ni kuwa baada ya kujenga jengo jipya la redio la Rahaleo, jengo lile lilikabidhiwa Shirika la Magazeti ndio ambao walikuwa nalo jengo lile. Kwa sababu tuna mpango wa kuanzisha kama alivyosema Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, ambaye ni Mwakilishi wa Jimbo la Bububu, kwamba kuna umuhimu wa kujenga eneo ambalo vijana wetu watapata nafasi ya ku-*record* sanaa zao.

Sasa ndipo jengo lile la *studio* ya zamani, ndio wizara na serikali kwa jumla imelitenga jengo lile kwa shughuli hizo. Isipokuwa sasa kuna ukumbi mule ambao tulianza kuutumia kwa shughuli hizo za kukodisha. Lakini wakati wa bajeti ambapo wawakilishi mbali mbali akiwemo Mhe. Nassor Salim Ali waliishauri wizara kwamba ni bora ukumbi huo usitumike kwa shughuli hizo za burudani. Wizara imesitisha shughuli hizo tokea wakati huo.

Sasa ikiwa Mhe. Mwakilishi ana habari hiyo kama unatumika hivi sasa na sidhani, kwa sababu maagizo yangu ni kwamba ukumbi ule usitumike tena. Kwa sababu Waheshimiwa Wajumbe wameishauri serikali na wizara hii inasimamiwa na Baraza la Wawakilishi na kwa hivyo, tumechukua maamuzi hayo ya kwamba hautumiki tena kwa shughuli hizo, isipokuwa labda kwa shughuli za semina utatumika.

Mhe. Mwenyekiti, lengo ni kwamba *studio* zile ambazo vimo vile vifaa, basi ni kuzigeuza kuwa ni *studio* nzuri za kurikodia muziki. Katika bajeti ya mwaka huu, tumetenga fedha maalum kwa ajili ya kushughulikia hiyo *studio*. Kwa hivyo, hilo ni jambo ambalo tunalishughulikia.

Jengine ni kuhusu kituo cha Dole. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba pale *TOC* ndio inayomiliki ile *academic* na sisi kama wizara tunashirikiana na *TOC*, ili kuona kama wana matatizo tuweze kuwasaidia. Lakini kimsingi wanaomiliki ni *Tanzania Olympic* na kwa hivyo tunashirikiana nao kuangalia ni kwa namna gani tutasaidiana.

Vile vile alizungumzia suala la *ZBC* ambalo nimeshalitolea maelezo. Suala la Viwanja vya Amani vitunzwe. Tunauchukua ushauri wako mheshimiwa, na tutashirikiana na wewe hasa ukiwa mwanamichezo, basi tutalishughulikia sana suala hili.

Pia kuhusu pongezi za miaka 50 kwa kushughulikia masuala ya mchezo wa mpira wa miguu. Suala hili linatuhusu mimi na wewe kwa sababu wewe ni mjumbe wa kamati. Vile vile aliuliza kwamba tumepata fedha kiasi gani. Tumepata shilingi milioni 150, alitaka kujua hilo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli ilizungumzwa kuwa wizara imepewa milioni 150 kwa ajili ya kushughulikia Kombe la Mapinduzi. Lakini zilizopatikana ni milioni 26 tu, na katika hizo milioni 16, milioni 8 zimetumika kwa ajili ya kuzigharamia usafiri wa timu zilizokuwa zikicheza mashindano haya katika Kiwanja cha Gombani Pemba. Na shilingi milioni 18 zilizobakia zilinunuliwa medali, makombe na tiketi mbali mbali zilizokuwa zinatumika katika shughuli hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu *ZFA* kushughulikia na kusimamia Kombe la Mapinduzi. Wizara haina tatizo na hilo, kama imejipanga sisi pia hatuna tatizo, tutashirikiana nao katika hilo. Lakini hili la miaka 50 ilikuwa ni agizo maalum kwamba ni lazima wizara itie mkono wake, lakini kwa sababu tumemaliza sisi hatuna tatizo na hili.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Asha Bakari Makame ni mjumbe wa kamati, alizungumzia vitu viwili muhimu. Kimoja ni kuhusu waandishi wa habari ambalo nimeshalitolea maelezo na jengine ni kuhusu redio Mtegani, ambalo suala hili limezungumzwa na wajumbe wengi sana. Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa kwa kupitia Mhe. Asha Bakari Makame nitowe maelezo kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba hizi redio za jamii ni muhimu na zinasaidia sana kuwaelimisha wananchi hasa katika maeneo yao. Redio Jamii ya Micheweni ni mfano mzuri sana, kama alivyosema Mhe. Mwakilishi wa Wawi, kwamba kwa kweli imesaidia mambo mengi sana na kama tulivyoripoti kwamba tumezindua Redio Mtegani na Redio Tumbatu. Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa kuna maneno mengi kwamba Redio Mtegani yule kijana haendelezwi ametupwa, wizara na serikali haimshughulikii.

Mhe. Mwenyekiti, ni sisi wizara tulianza kushirikiana naye, baada ya kufanya kiredio chake kikawa kinarusha rusha. Katika kuonesha kwamba tunashirikiana naye, tulimuombea msaada kutoka *UNESCO*, kapata vifaa vya karibu milioni 110. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ukisema serikali na wizara yule kijana haimshughulikii, sasa sijui anataka watu tumshughulikie vipi.

Mhe. Mwenyekiti, tulipoona tu ujuzi wake na anafanyakazi vizuri ni katika eneo lake ambalo wizara iliwaalika *UNESCO*, akapata vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 110. Kuanzia hapo kuna programu maalum ya mafunzo ambayo inaendeshwa na yeye ni sehemu ya mafunzo hayo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hilo tumelifanya na ikiwa mawazo ya Waheshimiwa Wajumbe kwamba apatiwe nafasi maalum ya kusoma ni jambo zuri. Lakini mwacheni kwanza amalize basi masomo ya sekondari angalau, ili aweze kusomesheka. Sisi tuna vyuo ambavyo vinaweza kumsomesha. Lakini unamchukua kijana wa miaka 10 au 14 unamsomesha nini? Kwanza unampa *practical training* ambayo tayari ameumbwa na kipaji, halafu akishamaliza *form IV* ana uwezo mzuri, tutampeleka katika vyuo kwa sababu ameonesha ana kipaji kizuri, ili aweze kuendelea vizuri.

Mhe. Subeit Khamis Faki, tunakushukuru suala la waandishi wa habari nimeshalizungumza. Kuhusu nyongeza ya mishahara kwa waandishi, limezungumzwa suala hili na Waheshimiwa Wajumbe. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba *ZBC* ni shirika na linapata ruzuku. Ninavyojua mimi mpaka hivi sasa taasisi zote ambazo zinapata ruzuku, basi hawajapata nyongeza hii ya mshahara. Kwa hivyo, mimi sina ujanja kwamba tu kwa sababu ni *ZBC*. Kuna wafanyakazi wenzao wa gazeti nao vile vile wanapata ruzuku, na hawajapata nyongeza ya mshahara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo tunashauriana na Wizara ya Fedha, ni utaratibu gani tufanye, kwa sababu haikuwemo katika bajeti yao ya ruzuku. Tukijaaliwa serikali hii haimdhulumu mtu. Tukishakubaliana ni wapi tupate kifungu, basi watalipwa ruzuku ya mishahara yao na malimbikizo ya kile ambacho wanakidai.

Mhe. Mussa Ali Hassan tunamshukuru, mawazo yake kuhusu *ZBC* tumeyachukua, tunayafanyia kazi na tumeshayatolea maelezo. Suala la vifaa, tutajaribu kufanya hivyo. Hivi karibuni tumenunua *microwave* ya shilingi milioni 70, tumewakadhi *ZBC*, ni mpya hiyo ambayo inatoa matangazo hivi leo na ni kwa sababu hiyo. Lakini tulikuwa tunapitishia kwa *Zanzibar cable* ni aibu kama ulivyosema. Haiwezekani Shirika la Serikali kupitisha matangazo yake kwa televisheni binafsi, lakini tulikuwa hatuna budi. Lakini tulipoona hivyo tumenunua *microwave* yetu na ndio hivi leo haya matangazo yanarushwa kwa kutumia *microwave* hiyo. Kwa hivyo, tumejitahidi kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni *ZBC* tuliwakabidhi shilingi milioni 260 kwa ajili ya kununua vifaa katika shughuli yao. Serikali inajitahidi kuliwezesha shirika hili kufanya kazi zake, lakini tumo na ndio kwanza tunaanza kama nilivyosema, ndio kwanza tunaliunda kwa hivyo mageuzi yake yanahitaji

muda Waheshimiwa Wajumbe, hivyo tuvumilieni kwa hili. Lakini tumedhamiria kwamba baada ya muda Shirika la *ZBC* lipate hadhi ambayo linastahiki.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Kamisheni ya Utalii. Tunamshukuru sana Mhe. Mussa Ali Hassan kwa mchango wake katika hili. Kamisheni ya Utalii ipo, na wizara yale ambayo yamezungumzwa yote tutayafanyia kazi. Tutaona namna gani ambavyo tutayafanyia kazi.

Kuhusu michezo Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hatujaweza kufanya vizuri na suala kubwa ni kwamba vyama vingi vimekuwa na migogoro ya siku nyingi, na walikuwa hawajafanya chaguzi siku nyingi. Kwa hivyo, agizo tumelitoa kwamba kila chama kifanye chaguzi zake. Vyama vya michezo vifikavyo 8 tayari, tunaamini kwamba baadae hivi vitakuwa vimejipanga vizuri. Ndio maana Mhe. Makame Mshimba akaingia, baada ya chama cha riadha kufanya vizuri. Kwa hivyo, tunaamini kwamba chama cha riadha kwa viongozi wa aina ile, basi itapata ufanisi baada ya muda mfupi sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma wa Jimbo la Wawi tunamshukuru sana. Kuhusu *ZBC* maslahi ya wafanyakazi, tumeshalizungumza hilo. Kuhusu mkataba wa ajira. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna wafanyakazi ambao hawana mkataba. Kwa sababu katika utaratibu wa vyombo vya habari kuna watu wanaitwa *freelance*. Hawa sio wafanyakazi wa kudumu wa chombo.

Kwa hivyo, mimi siwezi kuwapa mkataba *freelance* ni watu ambao wanafanyakazi kivyao vyao, wakileta habari tutainunua. Wanakwenda kutafuta habari nyengine tunawalipa. Kwa hivyo, hawa sio wafanyakazi wa kupewa mikataba na vyombo vyote vya habari duniani vina utaratibu wa *freelance*. Hivyo, hakuna utaratibu wa kuwapa mikataba ya kudumu ya ajira. Kuhusu posho lao, nimeshalizungumza. Asilimia 25, tumeshalizungumza hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu habari mpasuko ni kweli. Suala hili nimelizungumza, lakini kama ambavyo nimezungumza kwamba tukifanikiwa kujenga zile *studio* zetu mbili kwa Unguja na Pemba kama ambavyo tumekusudia, basi mambo haya yataweza kufanikiwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ndege, haikuanguka iliserereka, Mhe. Abubakar Khamis Bakary alikuwemo na *Alhamdulillah* yuko salama na tunaye hapa katika Baraza. Mhe. Mwenyekiti, vijana wetu wa *ZBC* walikwenda na kamera zao kuchukua, lakini kwa bahati mbaya iliserererekea katika eneo lenye kumilikiwa na jeshi. Kwa hivyo, kama tunavyojua kuna *limit* ya kupiga picha katika maeneo ya jeshi. Kwa hivyo hawakuruhusiwa kuchukua picha. Lakini

magharibi vijana walikuwepo pale wakitaka kuchukua na mimi kwa bahati nzuri nilikuwepo Pemba, wakaniambia Mhe. Waziri hatukuweza kuchukua video wala picha yoyote, kwa sababu eneo lile linamilikiwa na jeshi na kuna mipaka yake.

Mhe.Mwenyekiti, kuhusu studio ya Rahaleo ya zamani nimeshaizungumza. Suala la Redio Jamii Micheweni tumeshalizungumza hilo na pia Redio Mtegani limeshajibiwa. Kuhusu maslahi ya wasanii wetu. Suala hili tunalifanyia kazi vizuri. Serikali nzima tunashirikiana kwa hili. Hivi karibuni Waziri wa Katiba na Sheria, alitoa karibu shilingi 25 milioni kama mrahaba kwa wasanii ambao wamefanyakazi zao vizuri. Kwa hivyo, tuone kwamba serikali inachukua kila jitihada ya kuona kwamba wasanii wetu wanatunzwa vizuri.

Mhe. Rufai Said Rufai wa Tumbe, alizungumzia suala la umakini wa watangazaji. Mhe. Mwenyekiti, tumelichukua hili tutawasimamia vizuri. Kuhusu kukatwa majina ya viongozi, suala hili lilikuwepo lakini hivi sasa limesita. Kuhusu Redio Jamii ufuatiliaji hakuna. Hapana, ufuatiliaji upo, na tunafanyakazi vizuri na sababu hiyo ndio nikasema kama Redio Mtegani wale vijana tumewapa fedha hizo nyingi.

Vile vile kuhusu Hoteli ya Bwawani kwamba kuanzia mwaka 1994 mpaka leo 2014 imechakaa. Kweli ni hoteli kongwe sana, na serikali kama alivyosema Mhe. Rufai Said Rufai tunakubaliana na wazo lake la kuibinafsisha. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe kama unaye mtu basi mlete na alete *proposal* yake *ZIPA*. Tunakubaliana na wazo lako na hivyo kwa sababu serikali haifanyi biashara, kwa hivyo hatutaki sisi serikali tuonekane tunafanya biashara.

Kwa hivyo, hili waachiwe sekta binafsi na ndio sera tunayokubaliana nayo. Kama unaye mwekezaji mzuri au wewe mwenyewe mfuko unakuruhusu, peleka *proposal ZIPA*, na *ZIPA* itazingatia kama unaweza kuchukua hoteli, basi utamsaidia ili tuone kwamba inakwenda vizuri.

Mhe. Hija Hassan Hija wa Jimbo la Kiwani, alizungumza kuhusu *ZBC*, udhaifu wa watangazaji, na fursa za masomo. Tutajitahidi kidogo, kwa kipindi hiki tumejaribu sana kuwapeleka vijana wa *ZBC* China. Kwa karibu miaka hii miwili naweza kusema kama vijana 30 wamekwenda China kusoma. Kwa hivyo, tunajitahidi kidogo, nadhani tunahitaji kupongezwa badala ya kushutumiwa katika hili. Katika miaka ya nyuma walikuwa hawaendi. Hata baadhi ya hawa wanaochukua kamera hapa, kuna wengine wameshakwenda China kujisomea zaidi, hivyo suala hili tunalifanya.

Kuhusu haki zao na posho lao. Nilizungumza kwamba bodi inashughulikia suala hili na litafanyiwa kazi Mhe. Mwenyekiti. Kuhusu *ZMUX* ina msalaba. Aaah! Hii ni habari ya vionjo ambayo kwa kweli isingepaswa kuja katika Baraza. Sio kweli kwamba ukifungua *ZMUX* unaona msalaba. Kila mmoja anacho king'amuzi hapa, mimi ninacho na wengine wanacho. Tumezungumza suala hili, haipaswi kuzungumza hivo na hili lilianza zamani sana Mhe. Mwenyekiti.

Siku moja mnadhimu wangu alikuwepo katika Msikiti mmoja anaswali Ijumaa kama leo. Shutuma hizo alizotupiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo siku hiyo, maapizo makubwa kwamba vipi Waziri wa Habari analeta mambbo haya. Tunachozungumza AGAPE yupo hapa Zanzibar tangu mwaka 2007/2008 akishughulikia suala hili. Kwa hivyo alikuja enzi ya awamu ya sita akafanya *feasibility study* kubwa, kutoka Kusini Unguja hadi Kaskazini Pemba. Hakuna Kampuni yoyote ambayo imekuja imefanya *feasibility study* yake na ripoti kubwa katika hili.

Sasa hatuwezi kufanya kazi hii kuja mtu hivi wa juu juu, akasema anataka shughuli serikali tukampa ambaye hajafanya *feasibility study*, yoyote hili si jambo dogo ni suala kubwa na gumu sana ambalo linahitaji utaalamu mkubwa sana. Kwa hivyo tulikuwa hatuna namna isipokuwa tumpe mtu ambaye ana uwezo, keshafanya *feasibility study* kubwa.

Ni kweli tulikubaliana alete ving'amuzi laki tatu sio tano, kama alivyosema Mhe. Hija. Hivi sasa ameleta vin'gamuzi elfu tano, lakini elfu tano vilivyopo vimeuzwa elfu tatu, elfu mbili bado na tukachukua jitihada tukapunguza bei kidogo, kwa sababu Baraza lilitoa agizo hilo na sisi tukaona upo umuhimu kwa manufaa ya wananchi wetu.

Kwa hivyo Mhe. Hija vikipungua mpaka vikifika elfu nne, vikiwa viko mikononi tutamlazimisha viletwe vyengine. Lakini hizi pesa nyingi, huwezi kumwambia anayeendesha hii lete vin'gamuzi laki moja vibakie *store*. hizi ni pesa zinatakiwa zi-*rotate.* Kwa hivyo ni muhimu kwanza vin'gamuzi hivi vichache vilivyopo viingie kwa watumiaji baadae tumlazimishe, vin'gamuzi vimemaliza lete vyengine.

Hivi elfu tano alileta kwa ndege kutoka China. Kwa hivyo vitumike, angalau viuzwe elfu nne, au elfu nne mia tano, tutamlazimisha alete vyengine na kama nilivyosema tunaangalia kwamba tukiuza vin'gamuzi elfu kumi hadi elfu ishirini, tutazima mitambo ya *analogy,* ili tuwalazimishe wananchi sasa kama tulivyokubaliana na jirani zetu kwamba ukifika mwaka huu ianze *digital*. Kwa hivyo, wananchi wote anayetaka asiyetaka, ama akose televisheni au aingie

katika zama za *digital*, tunaangalia hilo na tutalitolea ripoti nzuri wakati wa kikao cha bajeti Mheshimiwa.

Mheshimiwa Hussein Ibrahim Makungu tunamshukuru sana kwa mchango wake na pongezi alizotupa. Watendaji wamezipokea na wamefanyia kazi na suala la kurikodi wasanii kama nilivyozungumza, jengo tumelianza tayari, bado vifaa ambavyo tunavifanyia kazi. Amelizungumza suala muhimu sana la ulinzi na usalama kwa sekta ya utalii.

Mhe. Mwenyekiti, hili jambo ni muhimu sana na wananchi wote lazima tushirikiane. Kwa sababu, hili serikali inajitahidi, kamisheni ya utalii lakini wananchi nao mmoja mmoja lazima tushirikiane kwamba huu ndio uchumi wa nchi yetu lazima kwa njia moja au nyengine kila mmoja atoe mchango wake.

Kuhusu Z *mooks* na *local channel,* Mhe. Mwenyekiti tulikubaliana kwamba ving'amuzi vioneshe *local channel* bure. Sisi Zanzibar *local channel* zetu ni ZBC. Sisi hatuwezi kuchukua Star TV ya Bara na ITV tukasema zote zile kwa Zanzibar ni *local channel* hapana, zile zimekuwa *registered* kule, zinalipa kule. Na kwa makubaliano na TBC sasa hivi *channel* mbili tumekubaliana kwamba hizi zitaonekana bure, kama umelipa mwisho wa mwezi, hukulipia hizi zitaonekana bure. Kwa hivyo yoyote yule ambaye ana kin'gamuzi basi kama zile ishirini hazipatikani, hajalipa elfu nane.

Hoteli ya Bwawani, pongezi zako Mhe. Hussein tumezichukua na tuendelee kushirikiiana kuona kwamba katika kipindi hiki cha mpito kabla hatujapata muekezaji, basi tuendelee kushauriana namna gani hoteli itakwenda vizuri sana. Tunashukuru sana kwa namna ambayo unashirikiana na Wizara katika kuona kuwa hoteli ile inapata ufanisi mzuri sana.

Mhe. Mohammed Mbwana kuhusu ZBC nishajibu, kuhusu vyombo vya habari binafsi vimejipanga vizuri. Mheshimiwa hili kwetu sisi ni fakhari kuona hivyo kwamba sera zetu hazivibani vyombo vya habari, vinavipa nafasi ya kujitanua na kukua. Kwa hivyo kila vyombo vya habari vikikua kwetu sisi ni fakhari kwamba sera ambayo tumeitunga na tunaisimamia inawezesha sekta binafsi kufanya kazi vizuri. sisi hilo hatuoni tatizo wala hatuoni wivu, ila tukiona tuko nyuma kidogo serikali ina mbinu zake za kuona kwamba inawapiku sekta binafsi.

Tume ya Utangazaji ina jengo finyu kidogo. Mheshimiwa ushauri wa Mheshimiwa tumeuchukua sana. Upatikanaji wa takwimu sahihi, hili tunalifanyia kazi na kama tulivyosema awali kwamba tuna Kamisheni ya

Utalii na Wizara ya Fedha wenyewe binafsi wanalishughulikia hili, kuona kwamba tunakuwa na takwimu sahihi ya watalii ambao wanakuja nchini.

Maeneo ya kihistoria ambayo yako Chambani. Mhe. Mwakilishi tunaomba tushirikiane hasa hili la mjini Chambani. Haya mengine ya Jambang'ome tunaelewa, tunakwenda nayo lakini hili la mjini Chambani hata mimi ni mgeni kidogo. Kwa hivyo naomba tushirikiane, mimi na wewe na Idara hii, kuona namna gani na hili tutaliibua kwa maslahi ya nchi yetu kihistoria na vizazi vinavyokuja.

Mhe. Panya tunakushukuru sana na tunashukuru sio kwa hivi sasa tu lakini kwa namna ambavyo ukiliona jambo linalohusu Wizara na hasa ZBC hunyamazi, husubiri kikao. Naomba uendelee na utaratibu huo, ili tuendelee kushirikiana na Wizara na si vizuri kuona jambo ukasuribi siku ya kikao cha bajeti. Ni vizuri ukiliona kama anavyofanya Mhe. Panya basi ushauriane na uongozi wa Wizara, ili lile jambo lipate ufafanuzi pale pale.

Mhe. Hamza Hassan Juma ninakushukuru sana, mchango ulikuwa mzuri sana. Umenisaidia sana hata kujibu kwangu hoja, kwa kweli kumekuwa kufupi sana baada ya mchango wako hasa kuhusu nyongeza ya mishahara ya wafanyakazi wa ZBC, tunalifanyia kazi hilo. Waandishi wa habari kwenda Dodoma totalifanyia kazi Mheshimiwa, na hili litategemea mfuko kama ulivyosema bajeti yangu ni finyu. Shirika ndio kwanza linakwenda tata, lakini kwa kuwa Waziri wa Fedha hapa yupo basi tutakaa na serikali kuona namna gani kwa vijana hawa angalau hawa waliomo humu ndani.

Kama alivyosema Mwakilishi mmoja kwamba tusije tukawaona watu wengine ambao wako nje, ndio wamechukua mabegi wanakwenda Dodoma, ni vizuri hawa hawa. Kwa hivyo hali ya fedha ikiruhusu basi vijana watakwenda Dodoma, lakini kama haikuwezekana basi ndio haiwezekani. Kwa sababu hawa ni vijana, kwenda kuwachukua kule wakaanza kuomba omba itakuwa mtihani mkubwa kwao na kwa familia zao. Lakini hali ikiruhusu Mheshimiwa, hilo halina wasiwasi. Kuhusu suala la uwanja wa Gofu umelieleza vizuri, naomba suala hili likitokea tuweze kushauriana vizuri sana.

Mhe. Farida tunakushukuru sana, kuhusu jengo la ZBC la zamani kubadilisha matumizi. Tumefanya hivyo makusudi lakini sio kwa rusha roho, lakini ni kwa ajili ya kujenga vipaji vya wasanii wetu. Tutaweka mashine mbali mbali za mitambo kwa ajili ya kufanyia kazi hiyo.

ZBC watangazaji wawe makini. Wapo wenyewe, Naibu Mkurugenzi Mkuu yupo, na mimi mwenyewe kama msimamizi nitaendelea kulisimamia hilo.

Hoteli ya Bwawani ni kweli Taasisi nyingi zinadaiwa za serikali, Mheshimiwa nawaomba wale wote Taasisi za Serikali wanaodaiwa basi tuhakikishe kwamba wanalipa madeni yao.

Mhe. Shadya kuhusu kutoonekana baadhi ya sehemu katika kituo cha Pemba kwa televisheni. Hilo tumelifanyia kazi kwa kiwango kikubwa na ninaomba tusaidiane kufanya utafiti zaidi. Taarifa nilizonazo za watendaji wangu kwamba hali ni nzuri, na kama alivyosema Naibu Waziri kuna maendeleo mazuri sana. Na ving'amuzi kutoonekana labda uwe hujalipa. Siku moja waziri mmoja alinambia aa Mheshimiwa baada ya mwezi mmoja sikuona tena matangazo, nikamwamba hujalipa, akanambia kumbe vinalipiwa, aa vinalipiwa. Kama hujalipa elfu nane mwisho wa mwenzi utakatiwa matangazo.

Kuhusu kuondoshwa mfanyakazi Juma Mmanga. Mhe. Shadya hili nililitolea maelezo wakati wa bajeti na bado nimewaagiza Bodi walifanyie kazi na ninaamini wakati wa kikao cha Bodi watalifanyia kazi. Na kuhusu watangazaji wanaosoma magazeti kwamba hawana mvuto, tutalifanyia kazi na tukiona kwamba Mhe. Juma Mmanga mwenyewe aingie pale akisoma tutalifanyia kazi hilo. Lakini mtizamo wa Wizara ni kwamba kwa sababu amefanya kazi nzuri sana, basi iwezekane Juma Mmanga kumpandisha hadhi au cheo awe Mkuu wa Wizara ya Habari pale Dar es Salaam. Lakini cheo hicho, hakitamzuia pia kushugulikia mambo ya ZBC au mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri nataka nikupe muda umalize kwa sababu leo waheshimiwa wajumbe tumekusudia hii ngwe tuimalize. Ningeomba tumuombe Waziri katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais atengue Kanuni ya muda ili tuweze kuongeza muda kidogo, tumwachie Mhe. Waziri amalize na baadae aje Mwenyekiti kumaliza.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshi kumalizia shughuli zilizo mbele yetu. Hivyo Mhe. Mwenyekiti naomba Baraza lako tukufu tuweke kanuni ya muda kando ili tuweze kumaliza shughuli zilizo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru na kwa sababu ya muda ulionipa nianze kuzungumzia mchango wako, si kwa sababu ya rushwa ya kuniongeza muda lakini kwa sababu ulichangia.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wako kwamba Kamisheni ya Utalii ipewe hadhi ili iweze kufanya kazi zake vizuri, serikali imeanza kufanya kazi hiyo. Lakini kwa sababu ya agizo lako na ushauri Mhe. Mwenyekiti, tutauchukua na tutauendeleza kwa *speed* kubwa zaidi. Kuhusu ZBC wawe wabunifu wasirudie rudie vipindi taarab na ngoma zimekuwa nyingi, kuwe na vipindi vya kuelimisha zaidi kama alivyofanya Mzee Karume. Mhe. Mwenyekiti tunakushukuru kwa agizo lako hilo na ushauri wako tutalifanyia kazi na tutaona baada ya muda mfupi ZBC imebadilika.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi amezungumza suala la michezo maskulini lirudishwe kwa sababu ina manufaa makubwa. Ni kweli Mheshimiwa, na tayari tumeliangalia hili na tumeunda Kamati ya pamoja ya Wizara mbili; Wizara ya Habari Utamaduni Utalii na Michezo na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mimi na Mhe. Shamuhuna ndio tunaosimamia kamati hii, imeshafanya vikao vyake vingi sana na tayari tuna ripoti ya kuitekeleza. Kwa hivyo Mheshimiwa tunakushukuru na suala lako tayari tumelifanyia kazi.

Kuhusu kuvifanyia kazi ving'amuzi kwani imekuwa ni tatizo kama hujalipa hupati *channel*. Ni kweli Mheshimiwa kama hujalipa utapata *channel* 2 tu, kwa hivyo tunachokuomba Mheshimiwa kama king'amuzi unacho, ili bamkwe akione vizuri basi kamlipie shilingi elfu nane ataweza kukiona vizuri bila ya matatizo.

Mheshimiwa wa mwisho ni Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa wa Kikwajuni, tunakushukuru Mheshimiwa, pongezi zako tumezichukua na kuhusu ushauri wako kwamba tutakapoanza matengenezo ya kiwanja cha *Mao tze Tung* wewe tukushirikishe, basi Mheshimiwa tutahakikisha kwamba tunashirikiana na wewe bega kwa bega, kuona kwamba kiwanja kile kimetengenezwa kwa ushauri ambao mwenye Jimbo utaona utie *inputs* zako Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa kunisaidia kujibu na kutoa ufafanuzi wa michango ya waheshimiwa wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti mwisho kabisa kama nilivyoanza nimshukuru sana Mwenyekiti Mhe. Mlinde, kwa kweli anafanya kazi zake vizuri sana, ananisaidia sana, anaitakidi hasa kwamba Wizara ya Habari ana jukumu la kulifanya na kwa hivyo hasubiri kikao cha kamati. Yeye bahati nzuri yupo

Unguja, hata kamati haipo basi huwa tunashauriana mambo yakionekana yanakwenda vibaya. Kwa hivyo ninamshukuru sana naomba aendelee mwendo huo huo, kwa sababu mimi na yeye tuna jukumu zito la kuisimamia Wizara hii na kwa hivyo bila ya yeye mimi nitakosa usaidizi katika usimamizi wangu.

Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti nilikuwa nataka nimuombe tu Mhe. Waziri kuna suala moja atusaidie na hili zaidi kwa kumtakia yeye mema kwa sababu ingawa taarab haipigwi pale Rahaleo sasa hivi, lakini taarab inapigwa jengo la Wizara ambapo pale tunawasumbua sana walinzi wetu. Na kwa sababu unajua inapokuja kutokezea maharibiko baadae, watu ambao watakaoanza kutiwa ndani kwanza watakuwa ni Polisi. Sasa nilikuwa naomba tu kidogo, hizi shughuli za burdani tuzitafutie maeneo yaliyokuwa maalum, isiwe katika majengo ya Wizara Kikwajuni.

Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni Utalii na Vijana: Ni kweli kwamba huwa tuna tatizo kidogo la ukosefu wa kumbi, wawekezaji hawajajielekeza sana katika eneo hilo. Kumbi zetu ambazo tunazo maarufu ni Bwawani. Bwawani ikiwa imejaa na huwa inajaa hasa siku kama hizi za maharusi, wananchi wetu mbali mbali wananza kuhaha wapi wajibanze kufanya shughuli zao.

Kwa hivyo wamekuwa na utaratibu wa kuja katika Wizara yao ya Habari na Utamaduni. Wanaona Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, ofisi yake pale uwanjani, kila mmoja anapafahamu kwa sababu ndio Baraza letu la Wawakilishi la zamani kwenye uwanja ule uliokuwa wa netball, wanakuja kuomba pale kufanya shughuli zao. Ama kama wana harusi wanalisha chakula pale, wengine wanafanya akdi pale pale na wengine wanaomba kupiga burdani. Sasa kwa kweli kuna mambo mengine taswira yake haipendezi kidogo.

Kwa hivyo Mhe. Mwakilishi ninakushukuru kunitanabahisha, zuri na tutalifanyia kazi.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kuna suala moja ambalo nilikuwa nataka muongozo wa Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti wakati Mhe. Waziri anajibu suala la fedha la milioni mia moja na hamsini ambzo amesema kwamba fedha zilizopatikana.

Na katika milioni mia na hamsini ambazo serikali ilikuwa itoe kwa ajili ya kuendesha mashindano yote wakati wa sherehe za miaka 50. Lakini fedha

zilizopatikana ni milioni kumi na sita kama asilimis 10.6. Vile vile Mhe. Mwenyekiti, fedha ambazo mashindano ya Mapinduzi Cup zimepatikana kupitia *gate collection* pamoja na zile za wahisani ni takriba milioni mia mbili. Pesa hizi ndizo ambazo ziliendesha michezo yote takriban michezo ishirini, sasa kukosekana kwa zile fedha za serikali imeifanya kamati iwe na madeni makubwa ambayo Mhe. Waziri anayafahamu.

Kwa hivyo suali langu ni kwamba, zile fedha ambazo serikali ilikuwa imeahidi kuendesha mashindano mengine katika shehere hizi zitapatikana lini, ili kuweza kulipa yale madeni ambayo Kamati imeyabeba hivi sasa.

Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni Utalii na Vijana: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru na ni kweli kama alivyosema Mhe. Nassor kwamba pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Kamati ile inayoshughulikia Kombe la Mapinduzi, imefanya kazi moja kubwa sana, inahitaji pongezi kubwa. Kama nilivyosema kwamba tulialika timu kubwa kutoka nje, kwa mara ya kwanza ilikuwa ni heshima kubwa sana.

Mwaka jana ilikuwepo ya Kenya tu lakini mara hii, ilikuwepo Kenya, Uganda nne, kwa hivyo kulikuwa kuna gharama kubwa na fedha hizi tulikuwa tunazitegemea kwamba zitusukume. Sasa ni deni ambalo tunalo na Ofisi ya Katibu Mkuu imeanza kuwasiliana na Wizara ya Fedha kuzipata hizi fedha, ili ziweze kuondoa madeni ambayo inayadai.

Kwa hivyo, hali ya Wizara ya Fedha ikiwa nzuri Kaimu Waziri yupo, basi tutahakikisha kwamba hakuna deni kwa mtu yoyote anaedai. Fedha yote itakayopatikana mwanzo italipia madeni ambayo yanadaiwa Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Mwenyekiti napenda nichukuwe fursa hii kukushukuru wewe na waheshimiwa wajumbe wote kwa kunipa fursa hii, kuja kuzungumzia yale machache ambayo kwa upande wa kamati yanahitaji maelezo kidogo. Lakini takriban michango yote ambayo imetolewa, imepata jawabu na ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote takriban 4 wametolea jawabu ambazo zilikuwa zinastahili kabisa. Kwa hivyo mimi kama Mwenyekiti wa Kamati hii, sitoweza kujibu yale ambayo yameshajibiwa. Nitajibu yale mawili tu ambayo yanaihusu kamati.

Lakini kwanza Mhe. Mwenyekiti napenda niwataje waliochangia. Jumla ya wachangiaji walikuwa 22, wachangiaji 18 walichangia kwa mdomo na wachangiaji 4 walichangia kwa maandishi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
Mhe. Hassan Hamad Omar
Mhe. Salma Mohammed Ali
Mhe. Nassor Salim Ali
Mhe. Asha Bakari Makame
Mhe. Subeit Khamis
Mhe. Mussa Ali Hassan
Mhe. Saleh Nassor Juma
Mhe. Rufai Said Rufai
Mhe. Hija Hassan Hija
Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
Mhe. Mohammed Mbwana
Mhe. Panya Ali Abdalla na
Mhe. Hamza Hassan Juma

Pia kwa upande wa Waheshimiwa Mawaziri alianza Mhe. Naibu Waziri wa Habari Utamaduni Utalii na Vijana na Mhe. Kaimu Waziri wa Fedha ambae pia ni Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Mhe. Mwinyihaji Makame. Pia Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdillahi Jihad na Mhe. Said Ali Mbarouk.

Waliochangia kwa maandishi ni:-

Mhe. Mgeni Hassan Juma
Mhe. Ussi Jecha Simai
Mhe. Fatma Said Mbarouk na
Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa

Mhe. Mwenyekiti, maagizo ambayo yalitolewa na kamati kwa kweli tunashukuru, Wizara zote tunazipongeza maagizo yale waliyafanyia kazi, ila tu kwa upande wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuna hili moja, Kamati kidogo inahitaji Wizara wakae na waweze kumsaidia, hasa kuhusiana na chanjo zenye ubora.

Wizara ilijitahidi katika hili, lakini kinachoonekana kwamba chanjo hizi kwa hivi sasa hazina ubora kwani baada ya matumizi zinaonekana zinaleta athari nyingi. Kwa hivyo kwa upande wa Wizara Mifugo na Uvuvi, tuwaombe tu walizingatie hili.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa Wizara ya habari kuna agizo namba 3 ambalo linahusiana na mmong'onyoko wa fukwe katika Chuo cha Utalii Maruhubi. Hili ni tatizo la muda mrefu, barua zimeandikwa tokea mwezi wa tisa,

tunaomba taasisi zinazohusika zikutane, tunataka ifuatiliwe na tuone utekelezaji wake. Na pia tupewe maelezo ya kutosha wakati wa bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, agizo namba 6 ambalo linahusiana na ZBC hasa linalohusiana na masuala ya umeme. Tumeelezwa kwamba tayari ZBC imeshakaa na Shirika la Umeme kuzungumzia suala hili. Pia tumeelezwa kwamba kumebuniwa mikakati ya kulipa deni hilo isipokuwa mikakati hiyo haikutajwa. Tunaomba suala hili liharakishwe na kikao kijacho tuelezwe limefikia katika hatu gani.

Na agizo namba 8 kuhusu haya mambo ya mionzi kulikuwa kuna taarifa za wafanyakazi kwamba wanapata athari kutokana na mionzi hasa wale wa mambo ya IT, kwa hivyo hatukuelezwa ni lini utaratibu huu utaanza, siku nyengine tuelezwe vizuri suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na michango ya wajumbe kama nilivyokwishaeleza kwamba mingi imefafanuliwa na sihitaji mimi kuitolea maelezo zaidi. Ila kwa yale ambayo yanahusu kamati na kwa kweli wajumbe wawili walitaka maoni ya kamati kuhusiana na michango yao.

Kwanza alikuwa ni Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Hassan aliilaumu kamati kwa kutoonana na Jumuiya ya Wavuvi wa Kojani. Mhe. Hamad tunachotaka afahamu kwamba maeneo ya kufanya kazi ni mengi na si rahisi kuyamaliza kwa mara moja. Lakini tunamshukuru sana kwa kutukumbusha, juu ya umuhimu wa jumuiya hii kwa kazi za kamati yetu kwa muda ambao tutaupanga baadae. Pia tunatoa wito kwa waheshimiwa wengine watusaidie maeneo kama haya ya kazi. Tunamuahidi kwamba tutakutana nao katika mzunguko ujao wa kazi zetu za kamati.

Pia Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salma Mohamed Ali aliitaka kamati kutoa maoni kuhusu mbwa wanaozurura ovyo. Maoni ya kamati katika hili ni kwamba mbwa hao wakamatwe na wafanyiwe utaratibu kama ule wanaofanyiwa ng'ombe wanaozurura ovyo.

Mhe. Mwenyekiti, narudia tena wajumbe, ninawashukuru waheshimiwa wote mawaziri kwa michngo yao mbali mbali ambayo imeweza kuisaidia kamati yetu.

Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha.

UTARATIBU

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti natumia kanuni ya 120 haki ya kuundwa kwa kamati teule. Nilipokuwa nachangia hoja yangu nilionesha wasiwasi kwamba serikali imetoa agizo rasmi kwamba wananchi si ruhusa kuharibu mazingira na nikasema kwamba wananchi wa Muambe na sehemu nyengine wamewahi kupelekwa Mahakamani kwa kuharibu mazingira hata kwa kuchimba tofali moja. Ni jeuri gani aliyoipata mwekezaji wa Nyanjale ya kuharibu mazingira kwa kung'oa minazi zaidi ya 300, huku taarifa zilizopo kwamba hata makaburi ya maiti za wananchi yakafukuliwa.

Nikajenga hoja kuwa Kanuni ya 120 kwamba inaelekea kuna jeuri ya mwekezaji huyu. Kwa hivyo, Baraza liridhie kuundiwa Kamati Teule ili kuangalia nguvu gani aliyoipata mwekezaji huyu kwa ajili ya kufanya uharibifu wa mazingira, wakati wananchi wengine wazalendo wanazuiliwa. Na kwa mujibu wa kanuni hiyo ya 120(2) hoja ikitolewa ya kamati teule huwa haijadiliwi hutegemea maamuzi ya Baraza. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja hiyo unamuelekezea nani? Unataka jibu kutoka kwa nani?

Mhe. Hija Hassan Hija: Hoja hiyo naielekezea kwa Baraza. Kwa hivyo, wewe uwahoji Baraza sasa, waangalie busara ya kuamua hoja yangu, kama haina maana waone kwamba hakuna maana, mimi ninavyoona kuna maana kwamba kwa nini mzalendo anazuiliwa kuharibu mazingira, lakini mwekezaji anafanya jeuri ile huku maiti za wananchi zikifukuliwa. Naomba Baraza liridhie kuundwa kamati teule na kama kuna hoja uwahoji kwa mujibu wa hoja hii.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Hija Hassan Hija, kwa kuonesha uthibiti wake na kuhakikisha kwamba mazingira ya nchi yetu yanalindwa. Ndio msimamo wa serikali kuona kwamba mazingira ya nchi yetu hayachafuliwi. Kwa sababu hili jambo amelileta hapa leo tunaanza kulisikia, si vyema kwa kila jambo tukaanza na utaratibu wa kuliundia kamati teule, kuna mambo ni ya kuyashughulikia moja kwa moja.

Kwa sababu Mhe. Hija Hassan Hija, ameliwasilisha jambo hili serikali inalipokea sasa ni wajibu wetu kulifuatilia tukajua yanayosemwa, pale ambapo tutashindwa kufanya shughuli kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa, basi Baraza linaweza kuamua vyenginevyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa kwa kuwa jambo hili tumelipokea hapa, si vyema kwa kila jambo hasa tukiangalia kwamba hivi sasa tukimaliza Baraza hili tunaelekea kwenye Bunge la Katiba, huo muda peke yake utakuwa tatizo. Kwa hivyo, mimi ningeomba Baraza hili liridhie kuikubalia serikali kwenda kufanya uchunguzi wa jambo hilo, tupate ithibati na ikionekana kuna mambo yametendwa kinyume na taratibu za kisheria, basi hatua za kisheria zitachukuliwa na serikali itafuatilia jambo hili kwa kina, ili kujua undani wa jambo lenyewe. Naomba Mheshimiwa Mwakilishi na Waheshimiwa Wajumbe wavute subira tulishughulikie jambo hili. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa Mhe. Waziri na sina tatizo nae, lakini ninavyoamini mimi ni kwamba maamuzi ya mwekezaji yule yamekuja baada ya kupata nguvu za serikali. Chombo hiki kazi yake kubwa ni kusimamia serikali . Kwa hivyo, serikali tayari imeshampa *authority* mwekezaji kufanya yale anayofanya, Wawakilishi kwa niaba ya wananchi ndio wachunguzi kwa yale anayoyafanya yana uhalali gani kwa mujibu wa sheria ya mazingira, kwa mujibu wa sheria ya uwekezaji, ili wananchi wapate taarifa sahihi.

Sasa kuiachia serikali kwenda kuchunguza jambo ambalo wao wameliridhia na mpaka mtu unampa *lease,* anafanya yale maana yake ameridhiwa, nadhani hakuna busara hiyo.

Kamati teule inaweza ikasubiri hata baada ya Bunge la Katiba, hata baada ya katiba mpya, lakini Baraza liridhie maamuzi sahihi kwa ajili ya kuangalia haki itendeke kwa mujibu wa sheria. Hatuwezi kuwaona wananchi wanapata vikwazo ndani ya nchi yao, lakini mwekezaji ana nguvu zaidi kuliko mwananchi yule, jambo ambalo sio malengo ya Mapinduzi. Kwa hivyo, naomba kwamba Baraza liridhie kuundwa kamati teule hata kama baada ya Bunge la Katiba, lakini wananchi wapate ukweli kwa nini mwekezaji yule ana jeuri ya kufanya yale aliyoyafanya na mwananchi wa ndani ya Zanzibar hii awe hana nguvu hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na pia nimshukuru tena Mhe. Hija Hassan Hija, kwa maelezo yake. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa kwamba hatuwezi kuridhia uchafuzi wa mazingira, hatuwezi kuridhia kufukuliwa kwa makaburi, kama alipewa kibali cha uwekezaji, kina utaratibu wake na masharti yake na inafaa yafuatwe, kama masharti yamekiukwa tutafuatilia tuone namna yalivyokiukwa na hatua zichukuliwe. Namuomba Mheshimiwa kama hatukutekeleza wajibu huo ndio basi afikirie kulishauri Baraza kwenye suala zima la kuunda kamati teule.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa naona tutakuwa tunaichelewesha hii hoja bure,wakati serikali inaweza kufanya wajibu wake vizuri katika kulitatua tatizo hili la msingi, hapa ni kulitatua tatizo. Twende tufuatilie, tuone kilichopo kama kuna kufukuliwa kwa makaburi tutaona, kama kuna kuchafuliwa kwa mazingira tutaona, na namuamini Mhe. Hija Hassan Hija, itakuwa kweli kafanya kazi yake vizuri. Kwa hivyo, atuachilie tulifanye hili jambo na tupate ufumbuzi uliostahiki.

Ninamhakikishia kwamba hatua zitachukuliwa kwa mtu yeyote yule anayeharibu mazingira katika nchi yetu pamoja na kutokufuata utamaduni wetu, huwezi kwenda kufukua makaburi ambayo tayari wapo watu wamezikwa pale. Hilo ni kosa. Kwa hivyo, tutafuatilia tujue undani wake. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti naomba sana Baraza lako hili liturudhie tuendelee na shughuli hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hija Hassan Hija, mimi nafahamu *concern* yako sana, naifahamu kwa sababu hilo suala hata na sisi Kamati yetu tulishughulikia na najua kwa nini leo unasisitiza suala hilo. Lakini nakuomba kwa hapa Mhe. Waziri, tayari ameshaelezea na tunajua serikali italifanyia kazi. Hivyo, leo tuache, tuna muda wa kutosha wa kuitizama serikali itakavyofanya kazi na pindi tutakapokuwa hatujaridhika, basi pale tuunde kamati teule. Nafikiria tukubali hivyo leo ili kwamba tuna muda mrefu na tuna *session* nyingi ambazo tutazifanya tutakuwa na muda wa kutosha wa kuibana serikali.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakuelewa sana na kwa kweli mimi Hija Hassan na wewe ni Mgeni Hassan, hatuna upinzani huo. Lakini Mhe. Mwenyekiti, anayejenga maeneo yale sio Mgeni wala sio Hija, ni mtu na uwezo wake, anaweza kuifanya kazi ile hata ndani ya wiki moja akamaliza, kesho na keshokutwa mimi na serikali hatutaamini kwamba pale palikuwa pana uharibifu wa mazingira, kwa sababu ana fedha na atatengeneza mazingira ambayo mtu aliyekuwa hajayaona hatoamini kwamba hapa pamefanywa uharibu wa mazingira.

Mimi ninachosema kwamba serikali naiamini, lakini ninavyoamini kwamba yule asingefanya yale na kwa mujibu wa barua ambayo nimeisoma hapa kuwa serikali imeagiza, Halmashauri ya Kaskazini ‘B’ imeagiza na barua ipo na wao wame-*quote* kwamba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndio waliotoa agizo. Sasa ninachosema mimi kwamba serikali tayari imeridhia. Serikali imeridhia jambo ambalo wameamini kwamba ni sahihi, Wawakilishi ndio wanataka kujua kwamba je, mauzo ya serikali ni sahihi? Kuwaachia wao waendelee kujisahihisha watajisahihisha kwamba ni sahihi.

Kwa hivyo, mimi Mhe, Mwenyekiti, nakuachia wewe sasa, uamue kwamba ukiona haina haja hoja yangu sawa, lakini mimi naona ni hoja ya msingi kuwa serikali imeji-*commit* kuwa iko radhi jamaa kuyafanya yale, lakini mimi kwa niaba ya wananchi wa Kiwani na hata wa Nyanjale wengine wanalalamika hawakufanyiwa haki. Sasa naomba kwa mujibu wa busara zako ukiona maelezo yangu aloona Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo mashelisheli Kiwani, yaani ukiona hayana maana sawa, lakini mimi nasema ni hoja ya msingi kwa maslahi ya watu wa Zanzibar, kwa nini mwenyeji awe hana haki, mgeni atambe. Mhe. Mwenyekiti, naomba busara zako.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba tena nimwambie ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija. Kwanza Mheshimiwa, hii kusema mzalendo hana haki, si neno zuri, kwa sababu haya tunayoyafanya yote ni kwa ajili ya maslahi ya wazalendo, hata kukaribisha uwekezaji ni kwa ajili ya kuleta maendeleo ya nchi yetu isaidie wananchi wa nchi hii. Si vyema kabisa kwa serikali kupambanishwa na wananchi wake, kwa sababu nia yetu ni kuhakikisha kwamba tunawahudumia wazalendo na wananchi wa nchi hii ndio tukawa tunayafanya yote haya.

Mimi nataka nirudie tena kusema, hakuna katika nchi hii atakayevumilia kuona makaburi ya wananchi yanachimbuliwa akayafumbia macho au kuona uharibifu wa mazingira unafanywa akafumbia macho, tutakwenda *physically* tuone kama kuna kosa turekebishe na hatua zichukuliwe. Lakini kama kuna suala tu ambalo halijafanyiwa tathmini ya kutosha tukajua ukweli wenyewe hapo tutatoa maamuzi kinyume na hali halisi ilivyo.

Ningeomba Mhe. Hija Hassan Hija na Waheshimiwa wengine tuvute subira, twende katika eneo tuone ukweli ulivyo, lipi la kurekebishwa lirekebishwe na lipi la kuchukuliwa hatua lichukuliwe hatua, Lakini pia tukumbuke kwamba, nao uwekezaji una nafasi yake na lazima tuupe nafasi yake, kama kuna makosa yoyote yametendeka, basi tutarekebisha na kama kuna hatua zichukuliwe, tutachukua.

Naomba sana Mheshimiwa tusifikie mahala ambapo tutawaogopesha wawekezaji wetu, tutavutana kwa sababu ya jambo dogo hili ambalo linaweza kurekebishika, mimi naamini kabisa kama kuna kosa limefanywa, basi hatua zitachukuliwa. Nawaomba sana Waheshimiwa tuvumiliane tuweze kutekeleza wajibu huu vizuri na ninamhakikishia Mhe. Hija Hassan Hija, atafurahia uamuzi wa serikali utakaochukuliwa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, sina nia ya kuvutana na Mhe. Waziri, ananijua sana mimi, ni ndugu yake, nina usikivu sana. Kwa sababu nahofia kwamba ushahidi utapotea na sitaki niwe na ushahidi ule wa

Kinyamwezi, namuomba aridhie sasa, mimi binafsi na serikali kupitia kwake na Wajumbe fulani wa Baraza hili kesho twende Nyanjale tukapate ushahidi wa kina juu ya makaburi yaliyofukuliwa na mazingira yaliyoharibiwa ili tuwe na ushahidi kamili kwamba hadi kesho mazingira yameharibiwa, ndio tuwaachie serikali wachukue hatua, ili baadae huko mbele nisijenikaambiwa kwamba Mhe. Hija Hassan Hija alisema uongo.

Kwa hivyo, twende kesho asubuhi tukaangalie hali ilivyo baadae tuiachie serikali ichukue hatua. Naomba hili tukubaliane kwamba kesho twende na yeye na baadhi ya wajumbe tukaone hali halisi ilivyo ili tuanzie pale, sasa tuwaachie serikali wachukue hatua kwa ajili ya hatima ya baadae. Mwenyekiti naomba hilo lifanyiwe utaratibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mimi binafsi kesho nina shughuli nyengine ambayo nimeshaitolea ahadi na itabidi niitekeleze, haitokuwa rahisi kwangu binafsi kwenda pale. Lakini kama Waheshimiwa Wajumbe watakuwa tayari itabidi tutayarishe utaratibu wa wahusika wa serikali wende huko wakaone washirikiane na Wajumbe, ikaonekane hali halisi.

Lakini hatuna tatizo la kwamba Waheshimiwa Wajumbe wasiende na maafisa husika wa serikali wasiende na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa itabidi iratibu jambo hilo twende *physically*, tupate hali halisi ilivyo. Naomba kuwasilisha Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu Mhe. Waziri, kwamba serikali itajipanga kesho twende isipokuwa yeye ana majukumu mengine, nakubaliana na hilo. Naomba Jumamosi ya kesho *Inshaallah* tupange utaratibu twende tukaone hali ili tupate taarifa ya kuanzia kwa ajili ya manufaa yetu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na serikali. Kwa hivyo, baada ya hapo kwa sababu yeye amedharurika, naomba aende na shughuli nyengine, lakini atupangie timu ya serikali na Wawakilishi wateuliwe tukaone hiyo hali kesho asubuhi *Inshaallah.*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Mhe. Hija Hassan Hija, mimi nafikiri hiyo kamati ambayo itateuliwa kwenda ningelipendekeza utaratibu, ile Kamati ya Sekta ya Baraza nayo ishirikishwe. Kwa sababu badala ya kuunda hizo kamati teule, basi ile Kamati ya Sekta ndio itakuwa vizuri kupewa suala hili wakalishughulikia hapo baadae kama kutakuwa na lolote lile kuliko kuunda kamati teule.

Kwa hivyo, nafikiri Mhe. Mwenyekiti, ni vyema kama walivyosema hivyo, lakini tuishirikishe Kamati ya Sekta ambayo kwa mujibu wa kanuni zetu kamati hiyo inaweza ikateuwa wajumbe wengine zaidi ya wale ambao wako katika kamati hasa wale ambao wametoa hoja. Hivyo, Kamati ya Sekta itamshirikisha Mhe. Hija Hassan Hija, na Mheshimiwa mwengine yeyote ambaye alizungumzia suala hili kwa mujibu wa kanuni zetu zinavyotaka. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante kwa ushauri mzuri, Mhe. Hija Hassan Hija, kuna lolote?

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi Wawakilishi wote nawaamini.Kwa hivyo, mimi nategemea maamuzi yako sasa.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Waheshimiwa Wajumbe niwaulize kuhusiana na taarifa pamoja na uchambuzi wa masuala mbali mbali ya mawaziri waliyotoa hapa pamoja na mwenyekiti kama wamekubaliana taarifa hizo, naomba waliokubali wanyooshe mikono. Waliokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Afya: Naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuakhirisha kikao ningependa kidogo kuwapa taarifa ya ushauri kutoka kwa Mwenyekiti wa *PAC*. Natarajia Waheshimiwa Wajumbe wote tayari mmepata Ripoti ya *PAC* hivyo, Mwenyekiti wa *PAC* anaomba katika mapumziko yenu ya Jumamosi na Jumapili muipitie vizuri ripoti ile ili muweze kuja kuichangia siku ambayo itawasilishwa rasmi hapa Barazani.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wajumbe, nachukua nafasi hii kuwashukuru nyote kwa utulivu wenu na vile vile naakhirisha kikao hiki hadi siku ya tarehe 03/02/2014 saa 3:00 asubuhi. Nawashukuru sana.

(Saa 2:17 Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 03/02/2014. Saa 3:00 asubuhi)